

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Ishirini na Nne - Tarche 15 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianze Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):**

Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi) kwa mwaka wa Fedha 2003/2004.

**MHE. RAMADHANI H. KHALIFAN (K.n.y. MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA):**

Taarifa ya Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Rais (Utumishi) katika mwaka uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka 2003/2004.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 229

**Utoaji wa Vibali vya Kukata Miti ya Kuchoma Mkaa**

**MHE. LEKULE M. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali za Vijiji zinajitahidi sana kulinda mazingira kwa kukataza watu wasikate miti kwa ajili ya kuchoma mkaa lakini baadhi ya Maafisa wa Wilaya hutoa vibali kwa watu kukata miti kwa ajili ya shughuli hiyo na wakati huo huo kuhariblu misitu. Je, kwa nini utaratibu wa kutoa vibali kwa ajili ya shughuli hiyo usifanywe na wenye ardhi ambao ni Serikali za Vijiji badala ya kutolewa na Maafisa wa Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**  
aliijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lekula Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Serikali za Vijiji zinajitahidi sana kulinda mazingira kwa kukataza watu wasikate miti hovyo kwa matumizi mbalimbali. Aidha, kwa kuwa misitu ni muhimu kwa uhai wa binadamu, jukumu la kutunza misitu ni la kila raia wa Tanzania japokuwa mwenye mamlaka ya kisheria kusimamia raslimali za misitu ni Afisa Misitu. Hata hivyo inapolazimu, Maafisa Misitu wanaweza kukasimu kwa wanavijiji mamlaka ya kusimamia maliasili misitu kutokana na utaratibu maalum utakaokubalika kati ya pande hizo mbili. Vile vile kwa mujibu wa Sera ya Misitu ya mwaka 1998 na Sheria ya Misitu ya mwaka 2002, wananchi wanaruhusiwa kujitengea maeneo ya misitu kuwa chini ya usimamizi wao. Kwa sasa utaratibu maalum umeandaliwa ili kusimamia misitu ya aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi ukataji wa miti kwa ajili ya kuchoma mkaa unatakiwa ufanyike bila kuharibu mazingira kwa kuhakikisha kuwa unapandwa mti kabla ya kukata mti. Aidha, utafiti umeonyesha kuwa uharibifu wa mazingira unaotokea katika misitu mingi hausababishwi na vibali vinavyotolewa na Maafisa Misitu, bali ni ukataji wa miti kiholela unaojitokeza baada ya vibali kutolewa kwa waombaji. Hivyo, Ofisi yangu itahakikisha Uongozi wa Vijiji unashirikishwa kikamilifu ili kuhakikisha kuwa uharibifu wa mazingira unaoweza kujitokeza unadhibitiwa ipasavyo. Vile vile wananchi wanashauriwa kutumia teknolojia rahisi ya majiko yanayotumia mkaa kidogo au pumba kwa ajili ya chakula. Hii itasaidia sana kupunguza uharibifu wa misitu. (*Makofî*)

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa maeneo mengi hayakutengwa na waliokabidhiwa mamlaka ya kusimamia maeneo hayo hawana uchungu na misitu iliyoko Vijiji na wale wenye uchungu na misitu hawana haki au hawana mamlaka; je, kwa nini Serikali za Vijiji zisipewe moja kwa moja zisimamie maeneo haya kuliko kuwakabidhi watu ambao hawana huruma na misitu? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana katika maelezo tumeeleza kwamba, utaratibu ulivyo hivi sasa baada ya sera na sheria ya mwaka 2000 kuwa zimepitishwa, Serikali za Vijiji sasa zinaruhusiwa kumiliki misitu kwa kadri inavyowezekana. Kwa hiyo, chini ya utaratibu huu ndio tunadhani tutaweza pengine kudhibiti vizuri zaidi uharibifu wa ukataji miti ambao hivi sasa unaendelea.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kutegemeana na Katiba yetu kila Mtanzania ana uhuru wa kuishi mahali popote mradi asivunje sheria na kwa kuwa hao ambao wanakwenda mahali popote hawajui hiyo sheria wanaingilia misitu, wanafyeka, wanachoma mkaa; je, Serikali sasa iko tayari kutoa ufanuzi bayana kwa kila Mtanzania kuelewa kwamba hawezikwenda kuishi mahali popote bila kupata utaratibu uliowekwa na Katiba ili uharibifu wa mazingira uweze kukomeshwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, wapo Watanzania kulingana na utaratibu tulionao hivi sasa, ambao wanahama kutoka eneo moja hadi lingine na taratibu zetu zinaruhusu. Lakini nataka nisisituze tu kwamba, popote atakapokwenda atakuta iko Serikali ya Kijiji na Serikali ndio yenyewe mamlaka kamili kwa kila mgeni anayeingia katika eneo lake. Serikali za Vijiji ndiyo zinatakiwa kumwambia akae wapi na afuate utaratibu upi. Kwa hiyo, hata kama hajui sheria, lakini pale anapokwenda atakuta mamlaka ambayo itamsaidia kumwelewesha juu ya taratibu zilivyo. (*Makofî*)

Na.230

#### **Zahanati ya Mbuyuni**

**MHE. PAUL E. NTWINA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wameonyesha nia ya kusaidiana na Serikali na Halmashauri ya Wilaya katika kuipanua Zahanati ya Mbuyuni ili kuipa uwezo wa kupokea wagonjwa wa kulala ambao wameongezeka kuliko uwezo wa Zahanati hiyo wa kulaza wagonjwa:-

(a) Je, Serikali iko tayari kusaidiana na wananchi katika upanuzi huo kwa kutoa msaada utakaokidhi azma hiyo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo kama hilo kwenye Zahanati zote nchini na ni kigezo gani kinachotumika ili Zahanati iweze kujengwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumbukumbu tulizonazo eneo la Mbuyuni kuna Kituo cha Afya na sio Zahanati. Kituo cha Afya Mbuyuni kilijengwa mwaka 1983 na Mhisani kutoka Taasisi ya Dini ya Katoliki aitwaye *Sister Tarcisia*. Kituo cha Afya Mbuyuni kinahudumia Kata za Kanga, Galula, Mbuyuni, Totowe na Namkukwe. Kituo kinahudumia wakazi wapatao 51,652 na kina vitanda vya kulaza wagonjwa 24. Kituo hiki kilikabidhiwa Serikalini mnamo mwaka 1985 na kikafanyiwa ukarabati mwaka 2002 ambao uligharimu kiasi cha Shilingi milioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuptitia Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, ipo tayari kusaidiana na wananchi katika upanuzi wa Kituo cha Afya cha Mbuyuni kwa kutoa msaada utakaokidhi azma hiyo kwa kuzingatia uwezo wa kifedha uliopo na vipaumbele vya Halmashauri ili kukabiliana na ongezeko la wagonjwa. Aidha, gari la wagonjwa kwa ajili ya Kituo cha Afya Mbuyuni (*Toyota Hard Top*) limeagizwa Japan kuptitia *UNICEF* baada ya fedha zilizotengwa Shilingi milioni 30 mwaka 2003/2004 kupatikana mwishoni mwa mwezi Juni, 2003. Gari litawasilishwa nchini mwezi Agosti, mwaka huu 2003.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafahamu umuhimu wa kuboresha hali ya huduma zitolewazo kwa wananchi. Hivyo Serikali imekuwa wakati wote ikishirikiana na wananchi, Serikali za Mitaa na Wahisani katika kuboresha huduma zitolewazo na Zahanati na Vituo vya Afya kwa kutoa huduma au kuongeza vitendea kazi kulingana na vipaumbele vya wananchi wenye na kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa. Baada ya wananchi kutoa maamuzi ya kupanua Zahanati au Kituo cha Afya wanashauriwa kuptisha mapendekezo yao katika Vikao husika kama taratibu za Halmashauri zilivyo ili kuweza kupata mgao wa Bajeti ya Serikali. Kuhusu, vigezo vinavyotumika ili Zahanati au Kituo cha Afya kiweze kujengwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kwanza ni wananchi kutambua tatizo lao na kuwa tayari kushirikiana na Serikali katika kujenga Zahanati au Kituo cha Afya kinachohusika;

(ii) Umbali kutoka Zahanati, pale inapokuwa ni Zahanati usiozidi kilomita kumi kwenda na kurudi.

(iii) Wingi wa watu. Zahanati moja inatakiwa kuhudumia watu wapatao 10,000 na Kituo cha Afya watu wapatao 50,000.

(iv) Mwisho, ni hali ya kijiografia ya eneo hilo kama itaonekana kwamba si rahisi kuwezesha watu kupata huduma ya afya bila matatizo, Kituo cha Afya au Zahanati inaweza vile vile ikakubaliwa katika eneo kama hilo.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa Kituo hiki cha Afya cha Mbuyuni kilijengwa na Taasisi ya Kidini na Waziri amekubali kuwa kilijengwa na Taasisi; na kwa kuwa katika Jimbo la Songwe kuna Zahanati zilizojengwa na Taasisi hizi za Kidini kwa mfano Galula, Kanga, Magamba, Mbangala na Udindi; sasa hivi karibuni Taasisi hizi za Kidini zinataka zirejeshewe zile huduma waziendeshe wao; je, Waziri atasema nini juu ya hili?

Pili, kwa kuwa kumekuwa na huduma tofauti kati ya Serikali hasa ukizingatia juu ya mambo ya Ukimwi au wenzetu wanatumia Uzazi wa Mpango, sasa katika hilo kama watazichukua, je, Serikali itakuwa tayari kuongeza na Taasisi hizi ili huduma zile za kawaida ziendelee kuwepo? (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nafikiri, hata Ofisi yangu kwa ujumla hatuna taarifa hiyo kwamba, Vituo vya Afya na Zahanati ambavyo vilikuwa chini ya Taasisi hizo lakini zikarejeshwa Serikalini kwamba wanazitaka zirejeshwe. Kama ipo taarifa hiyo, basi tuna hakika tutapata maelekezo kutoka Wizara ya Afya na utaratibu utakaofaa. Lakini hata kama zitachukuliwa na Taasisi hizo, hilo haliwezi kuzuia hata kidogo matibabu na huduma nyingine zinazotolewa ikiwa ni pamoja na hizo za Ukimwi na nyinginezo kutotolewa katika Vituo hivyo kwa sababu taratibu zipo ambazo zimewekwa na jana Waziri wa Afya amelielea vizuri iwe ni chini ya Mfuko wa Afya au mifuko mingine, lakini bado Vituo hivi vinaweza kabisa vikaendelea kutoa huduma hiyo.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa jicho lako zuri limeniona. Kwa kuwa kumetokea mtindo sasa hivi Serikalini karibu Wizara zote au Idara zote zinaagiza magari ya bei ya ghali sana (*VX*) kila baada ya miaka mitatu na kuviacha Vituo vya Afya, Zahanati na Hospitali nyingine hazina magari; je, Serikali iko tayari kukubali kuagiza magari ya bei nafuu ili angalau hizi Zahanati na Vituo vya Afya ambavyo havina usafiri na akina mama wanahangaika wapate hata *Land Rover?* (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda niamini kwamba, magari anayozungumza ni yale yanayohusiana na Serikali za Mitaa. Siwezi kuwa *Spokesman* wa Serikali Kuu hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, ninachoweza kusema ni kwamba, maamuzi ya kununua magari ya aina gani, katika Halmashauri zetu yanafanywa na Mabaraza ya Madiwani katika maeneo husika. Kwa hiyo, mimi rai yangu kwa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba tunaposhiriki katika Vikao hivyo, sisi tunawategemeeni sana muwe chachu katika kubana, kuongoza na kuelekeza mambo ambayo tunaona ni kwa manufaa ya umma. Kwa msingi huo basi, mimi naomba nitoe rai tu kwamba, wote tushirikiane ili tuweze kufanya kazi hiyo vizuri. (*Makofit*)

Na.231

#### **Mkakati wa Kupambana na Umaskini**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ni kufuatilia utekelezaji wa mikakati ya kupambana na umaskini katika Wizara, Idara mbalimbali, pamoja na Mashirika Binafsi:-

- (a) Je, utekelezaji huo unakwenda kwa pamoja na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 na kwamba yale yote yaliyopangwa yatakamilika na kutufikisha tulikokusudia kwa kipindi hicho?
- (b) Je, ni utaratibu gani unaotumika katika kufanya tathmini ya utekelezaji huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye sehemu ya (a) na (b) pamoja na masahihisho aliyoyafanya, kama ifuatavyo:-

Ni matarajio ya Serikali kwamba, utekelezaji wa mikakati ya kupambana na umaskini utakwenda sambamba na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na tunategemea mwaka 2025 yale yote yaliyopangwa yatakamilika na kutufikisha tunapotaka. Dira ya Maendeleo ya Taifa (*Tanzania Development Vision*),

Mkakati wa Kusimamia Sera za Kuondoa Umaskini, Mkakati wa Kupunguza Umaskini na Mkakati wa Serikali wa Kusimamia Fedha za Misaada kutoka kwa Wahisani, zimekusudiwa kutoa mwongozo katika masuala ya kupambana na umaskini nchini. Lengo ni kuhakikisha tunapunguza umaskini kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2010 na kuondoa kabisa umaskini uliokithiri mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi uliofanyika kwa kutumia takwimu za utafiti wa majumbani (*House on Budget Survey*), umesaidia kufanya marekebisho katika kuweka malengo na kubainisha uwezekano wa kupunguza umaskini kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2010. Aidha, kulingana na Taarifa ya pili ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini ya mwaka 2001/2002, Serikali imejiwekea malengo katika kila Sekta ya kipaumbele kama ilivyoinishwa katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini mwaka 2000. Kwa mfano, katika kupunguza umaskini wa kipato, lengo ni:-

- (i) Kupunguza uwiano wa watu walio na umaskini wa chakula kutoka asilimia 35.7 mpaka 17.8 mwaka 2010;
- (ii) Kupunguza uwiano wa watu walio na umaskini wa mahitaji muhimu kutoka asilimia 18.7 mwaka 2000 mpaka 2001 kwenda *percent* 9.3 mwaka 2010; na
- (iii) Kukuza uchumi kutoka asilimia 4.9 mwaka 2000 kufikia asilimia sita mwaka 2003. Uchumi ulikua kwa asilimia 5.6 mwaka 2001 na asilimia 5.9 mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, nguvu nyngi sasa zinaelekeza kwenye Sekta za kukuza Ustawi wa Jamii na kuboresha mazingira yatakayochangiwa kuongeza vipato vya wananchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu unaotumika kufanya tathmini ni kupitia mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini yaani *Poverty Monitoring Master Plan*. Mfumo huu utasaidia ukusanyaji wa takwimu mbalimbali katika muda uliopangwa, utachambua pia na kusaidia katika kutathmini jithada zinazofanyika kama zinaleta mafanikio au la. Kwa mfano, kama nilivyo sema utafiti wa vipato vya majumbani 2000 mpaka 2001, Sensa ya Watu na Makazi na tafiti nyingine zinazofanyika nchini chini ya usimamizi wa Serikali, ni hatua ya utekelezaji wa mfumo wa ufuatiliaji. Pamoja na tafiti hizi kuna utaratibu shirkishi pia wa ukusanyaji taarifa, yaani *Participatory Poverty Assessment*, ambao una lengo la kuwashirikisha wananchi kutoa maoni ili kutathmini mafanikio ya utekelezaji wa mkakati wa kupambana na umaskini.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kufanya mikakati ya kuondoa umaskini na maendeleo tangu mwaka 1985, hali ya uchumi ilikuwa inapanda inashuka, inapanda inashuka, mpaka sasa tunakwenda *under deficit budget* na watu bado masikini; je, Waziri au Serikali itafanya mikakati gani sasa hivi uchumi wetu usishuke uendelee kupanda tu? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyo sema kwenye jibu la msingi ni kwamba, Serikali sasa ili kutimiza malengo yake iliyojiveke, itatoa mkazo kwenye kuboresha maendeleo na ustawi wa jamii ikiwa ni pamoja na kukuza kipato cha kila mmoja kwa maana ya kwamba wananchi wenyewe watasaidiwa katika kutekeleza miradi yao ya kuondoa umaskini. Kwa mfano, hivi karibuni nimehudhuria Mkutano huko Geneva, ambao unahusika na kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Kimataifa uliofanywa na Wakuu wa Nchi huko Johannesburg katika kuhakikisha kwamba, wananchi wanasaidiwa kukuza kipato chao na kwenye Mkutano huo ambao uliandaliwa na Umoja wa Mataifa, tumekubaliana kwamba, nchi katika kuwasaidia kuondoa umaskini lazima tutilie mkazo katika suala zima la kukuza kilimo na ndiyo maana hapa Tanzania Serikali kwa kupitia Wizara ya Kilimo, inaweka mikakati mbalimbali ambayo itahakikisha wananchi mazao yao yanapata soko na hivyo kuwasaidia kuondokana na umaskini wa kipato.

Na.132

#### **Mchanga wa Dhahabu Kupelekwa Nje**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Serikali inawaruhusu wachimbaji wa madini ya dhahabu kusafirisha nje mchanga wa dhahabu kwa ajili ya kusafisha?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** aliijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Paul Ng'wala Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeruhusu Kampuni ya *Kahama Mining Corporation Limited*, inayomiliki mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu, kusafirisha mchanga ambapo kitaalam unaithwa *gold copper concentrate* kwenda nchini Japan kwa ajili ya kutenganisha dhahabu na shaba kwa sababu *concentrate* inayozalishwa haitoshi kuanzisha mtambo ambao utajiedesha kibiashara. *Concentrate* inayosafirishwa na mgodi wa Bulyanhulu ni takriban tani 25,000 kwa mwaka na ambayo huzalisha kiasi cha tani 3,000 hadi 5,000 za shaba na wakia 230,000 za dhahabu. Ili mitambo ya kusafisha *concentrate* iweze kuendeshwa kwa faida, inahitaji kuzalisha si chini ya tani 150,000 za shaba au *copper concentrate* kwa mwaka kiasi kwamba, mgodi wa Bulyanhulu hauwezi kufikisha. Kwa mantiki hiyo, wenye mgodi hawawezi kujenga mtambo hapa nchini, kwani utawatia hasara na ni vyema kusafishia *copper concentrate* hiyo kwenye mitambo ambayo ipo tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile zipo nchi nyingine hapa duniani ambazo zimeendelea kupeleka mchanga nje kusafisha kama hivi na zimeona sio busara kujenga viwanda vyao wao wenyewe kutokana na hoja hiyo hiyo kwamba, mitambo ya kujiendesha kwa faida inahitaji kiwango kikubwa cha uzalishaji ambacho kwa sasa hakijafikiwa. (*Makofî*)

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swal moja la nyongeza. Kwa kuwa ni mchanga mwangi sana unaopelekwa Japan kutoka *Kahama Mining*; na kwa kuwa mchanga ni maliasili kama madini mengine; Waziri anaweza kutuambia baada ya miaka 20 au 30 hayo mamilioni ya tani yatarudi vipi na kama hayarudi yatalipiwa Shilingi ngapi kwa tani? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchanga niliosema unasafirishwa nje ni tani 25,000 na napenda nirudie kwamba, mchanga huu hautoshi kuanzisha kiwanda cha kusafisha na kutenganisha madini haya hapa nchini hasa ikizingatiwa kwamba, kazi kama hiyo kwa kuwa Serikali imeshajitoa katika shughuli za kibiashara, itabidi iwekezwe na wawekezaji binafsi. Mchanga huu ni mwangi kwa maana ya tani hizo ambazo zimepelekwa na hautegemewi kwamba mchanga huu ukienda kule utarudishwa. Kinachopelekwa kule ni kwenda kutenganisha, hauendi ili mchanga huu urejeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu faida ambayo nchi inaipata kutokana na mchanga huu unapokwenda kusafishwa na kurejeshwa hapa, napenda nitoe takwimu kidogo tu kwamba, mwaka 2001 kiasi cha fedha ambacho kilipatikana ni kama Dola milioni 4.7 na mwaka 2002 ni kama Dola milioni 7.7. Lakini nataka niongeze hivi, kama ambavyo alisema Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anatoa *budget speech* hapa Bungeni, Serikali inatambua umuhimu wa kuweka utaratibu wa kusafisha mchanga huu hapa kama ingelikuwa tuna mchanga wa kutosha. Lakini kwa kuwa kwa sasa hivi hatuna uwezo huo, ndio maana Serikali imehakikisha kwamba, inateua tathmini au mtu ambaye ni *consultant* anaitwa *ASEA* na huyu ameshapatikana na Mkataba umeshaingia baina yake na Benki Kuu na ameanza kazi mwezi huu wa Julai, 2003. Kutokana na hali hiyo basi, tutakuwa katika hali nzuri zaidi ya kuhakikisha kwamba, hatudanganywi kuhusu madini yanayoweza kuwa yamechanganywa katika hii *copper concentrate* ili kuweza kuiletea faida nchi yetu. (*Makofî*)

Na.233

**Kukatika kwa Umeme Mara kwa Mara**

**MHE. MWAKA ABRAHMAN RAMADHANI** aliuliza:-

Kwa kuwa lengo la ubinafsishaji/ukodishaji wa Mashirika ya Umma ni kuleta ufanisi katika utendaji, utoaji wa huduma bora na kuwezesha Shirika/Kampuni kupata faida:-

- (a) Je, kwa nini tangu Shirika la Ugavi wa Umeme (*TANESCO*) liuzwe/likodishwe, tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara limekuwa ni jambo la kawaida na je, huo ndio ufanisi?
- (b) Je, ni sababu zipi zinazofanya umeme ukatike mara mara?
- (c) Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge hili kuwa ni kuanzia lini wananchi wataondokana na adha hiyo?

#### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mwaka Abraham Ramadhani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali kukodisha Menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) ambaa Mkataba huo ulianza mwezi Mei 2002, ili kuondokana na matatizo ambayo *TANESCO* ilikuwa nayo ilikuwa ikijiendesa kwa hasara na matatizo mengine ya kiufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kukatikakatika umeme mara kwa mara linatokana na uchakavu wa mfumo mzima wa umemekatika uzalishaji na haswa katika usafirishaji na usambazaji, ukachavu wa vifaa kwa mfano katika mfumo wa kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme, ukosefu wa matengenezo ya uhakika katika mifumo ya umeme kwa wakati unaofaa yaani *preventive maintenance*, wizi wa vifaa vya umeme kama nyaya au waya, mafuta ya *transformer* na kadhalika. Vile vile matukio ya dharura ambayo yako nje ya uwezo wa Shirika yaani *natural calamity* na natural disasters, kama mvua kubwa inayoambatana na upepo mkali na matawi ya miti ambayo yanagusa laini za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuleta ufanisi na kuondokana na adha ya kukatikakatika kwa umeme, Wizara yangu ikishirkiana na *TANESCO* imefanya mambo yafuatayo:-

- *TANESCO* chini ya Menejimenti mpya imeandaa utaratibu wake kufanya matengenezo na baadhi ya matengenezo yameshaanza, matengenezo muhimu katika mifumo ya umeme kama nilivyosema awali;
- Imeanza kununua vifaa muhimu kwa ajili ya kukarabati mifumo ya kusafirisha na kusambaza umeme;
- Inafanya matengenezo muhimu katika mfumo wa umeme ikiwa ni pamoja na kubadilisha nguzo zilizooza, vikombe vichakavu, *transformers* na kadhalika; na
- Kwa hivi sasa kuna mradi mkubwa unaoendelea kutekeleza ukarabati kwenye vituo vyote vya Gridi ya Taifa katika Mikoa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizotajwa hapo awali zitakapokamilika, tunataraji kwamba tatizo hili la kukatikakatika umeme litapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, suala la kukatikakatika umeme linatokana haswa na matatizo yaliyo katika mfumo mzima wa umeme katika sehemu zake tatu kuu nilizotaja awali, yenye kuzalisha, kusafirisha na kusambaza.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa katika jibu lake la msingi alisema kwamba *TANESCO* haikubinafsisha ila wamekodi menejimenti kuondoa hasara iliyokuwa inapatikana. Je, ni sababu zipi zilifanya Idara za Serikali zilipe madeni yao sasa na hawakulipa wakati kuna uongozi wa Kitanzania? (*Makofî*)

Pili, kwa kuwa tatizo la kukatikatika umeme...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Watondoha acha!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Idara za Serikali na Wizara za Serikali zimekuwa baadhi yake zikilipa kikamilifu bili za *TANESCO* hata kabla menejimenti ya *NET GROUP* kuingia na mfano, ni Wizara ya Nishati na Madini, ambayo yenye imekuwa ikilipa kikamilifu bili zake *TANESCO*.

Nakubali kwamba, kuna baadhi ya Wizara na Idara ambazo zilikuwa na matatizo ya ulipaji, lakini hii ilitokana na uwezo mdogo wa Serikali wa fedha, lakini kadri uwezo wa fedha ulivyoongezeka, Wizara hizi na Idara hizi sasa zimeweza kulipa madeni haya kikamilifu. (*Makofî*)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa *Net Group* tayari wameanza kujilipa *bonus* kubwa kubwa zaidi ya bilioni moja na wakati huo huo bado kunaonekana kuna matatizo ya umeme kukatikatika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni kwamba kuna *contradiction* hapo ya kulipana *bonus* na huku umeme bado unakatikatika badala ya kuboresha miundombinu? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda niseme kwamba, malengo ambayo *Net Group* wamepewa au kazi wamepewa ni kurekebisha matatizo yaliyo katika Shirika katika eneo la fedha, eneo la kiufundi na eneo la kiuongozi yaani kiutawala kwanza.

Katika mkataba huu, yaani *Management Contract*, kuna aina mbili za malipo, kuna *First Retainer Fee*, yaani kwa sababu ya wao kuwa wamekodishwa na pia kuna *Success Fee*, yaani hii ni ada au ni *fee* inayolipa kutokana na faida inayopatikana.

Wakati hauturuhusu hapa, lakini niko tayari kumpa Mheshimiwa Mbunge, baadaye ufafanuzi zaidi kuhusu maeneo ambayo wakitenda vizuri basi wao wanaweza kutokana na tathmini ambayo inafanyika inayotokana na ushauri wa Mshauri yaani *Consultant* aliyeajiriwa na pia baada ya kushauriana na Wizara ya Nishati na Madini, *PSRC* na *TANESCO* wenye na kadhalika kuweza kulipa kutokana na eneo ambalo wamefanikiwa.

Kwa hiyo, si kweli kwamba, wanalipwa tu na nataka niseme pia kwamba, tangu wameingia katika menejimenti, imefanyika kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba, mfumo wetu wa umeme unaanza kurekebishiwa na tatizo la kukatikatika umeme pia linapungua na kwa kweli mimi mwenyewe nilizindua mradi mmoja pale Ubungo mwezi Aprili, 2003 wa kuunganisha umeme wa Kihansi na Kidatu, ambao ulitarajiwa kupunguza kukatikatika kwa umeme kwa asilimia 30 na katika maeneo mengi kukatikatika kwa umeme kutokana na matatizo ya kiufundi kumepungua kwa kiasi fulani. (*Makofî*)

Na. 234

#### **Ucheleweshaji wa Upelelezi wa Polisi**

**MHE. MGANA I. MSINDAI (k.n.y. MHE. LEONARD M. SHANGO)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi watuhumiwa wa kesi za makosa ya jinai wanacheleweshwa kupata haki zao Mahakamani kwa sababu za kuchelewa kukamilishwa kwa upelelezi wa Polisi ambao ndiyo msingi wa mashtaka:-

(a) Je, Serikali imewahi kufanya utafiti wa kutosha ili kuona kama kweli sababu za kuchelewesha uchunguzi zinazotolewa na Jeshi la Polisi ni za kweli au ni sababu za uzembe, kutokuwajibika, uvuvi au mianya ya rushwa?

(b) Je, Serikali imewawajibisha Maafisa Polisi wangapi wanaobainika kuwa wanachelewesha kukamilisha upelelezi kwa sababu za uzembe, uvuvi, kutokuwajibika au mianya ya rushwa?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kurekebisha au kuimarisha taratibu za kikazi za kuwasimamia Maafisa Polisi wanaotekeleza upelelezi wa makosa ya jinai?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sababu za msingi kabisa ambazo huchangia kuchelewesha ukamilishaji wa upelelezi wa kesi. Sababu hizo zinajulikana na hujadiliwa na kutafutiwa ufumbuzi kwenye vikao vya kazi ndani ya Jeshi la Polisi. Vikao hivyo ni pamoja na vile vya Kamati za Mikoa na Wilaya za Kusukuma Kesi Mahakamani (*Case Flow Management Committee*), zenye wajumbe kutoka Idara za Mahakama, Polisi, Magereza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Utafiti mdogo tu unaweza kwa urahisi kubainisha sababu hizo zikiwemo zifuatazo:-

- (i) Kutopatikana kwa watuhumiwa wote au baadhi ya wanaotafutwa;
- (ii) Kutopatikana kwa mashahidi muhimu;
- (iii) Kutopatikana kwa vielelezo muhimu kama taarifa za *postmortem* kutoka kwa Mkemia Mkuu na taarifa zingine za kitaalam;
- (iv) Ukosefu wa vitendea kazi vya aina mbaimbali ili kukamilisha upelelezi kwa wakati muafaka;
- (v) Uwiano mdogo wa kesi nyingi zinazopelekwa Mahakamani ikilinganishwa na idadi ndogo ya wapelelezi waliopo; na
- (vi) Ushirikiano mdogo unaotolewa wakati mwengine wakati wa upelelezi na mashahidi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiwajibisha Askari Polisi wanaobainika kuwa wanachelewesha kukamilisha upelelezi kwa sababu za uzembe, uvivu, kutokuwjibika au mianya ya rushwa. Kwa mfano katika kipindi cha Januari 1999 hadi 29 Mei, 2003, Maafisa Wakaguzi na Askari wa kawaida 75 waliondolewa katika Idara ya Upelelezi na kurejeshwa katika shughuli za kawaida yaani *General Duties*. Aidha, katika kipindi hicho askari 22 wamefukuzwa kazi kwa sababu hizo hizo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, zipo taratibu za kikanuni za kuwasimamia Maafisa wa Polisi wanaopewa kazi za kufanya upelelezi wa makosa ya jinai. Taratibu hizo zimeainishwa vizuri katika *Police Orders No. 3*. Hata hivyo, Serikali ipo tayari kufanya marekebisho wakati wowote ule itakapoonekana upo umuhimu wa kufanya hivyo ili kupunguza zaidi ucheleweshaji wa upelelezi wa makosa ya jinai.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Nashukuru Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa sababu moja inayofanya upelelezi uchelewe kukamilika ni usafiri; na kwa kuwa Wilaya ya Iramba imekuwa haina gari kwa muda mrefu na vile vyle Wilaya hiyo ni kubwa na usafiri haina; je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa kutafuta magari ya kutosha Makao Makuu ya Wilaya na vile vyle Iramba Mashariki na sehemu za Ndago ili upelelezi uwe unakwenda kwa kasi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya awali kwamba moja ya sababu ambazo zinachelewesha upelelezi ni hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ya kukosekana kwa usafiri. Kwa kweli si tu kwa Iramba peke yake, ambayo amesema Wilaya kubwa na mimi nathibitisha hivyo kwa sababu nilishapata heshima kuwa Mkuu wa Wilaya ya Iramba, najua kabisa anachokisema Mheshimiwa Msindai. Tatizo la Iramba liko katika Wilaya nyingi.

Mwaka 2001 tulianza kugawa magari kwa Maofisa Upelelezi wa Wilaya Ofisi za *CID*, lakini hayakutosha. Kwa hiyo, Wilaya karibu asilimia 60 zilipata, asilimia 40 zilikosa pamoja na Wilaya ya Iramba. Katika mwaka huu wa fedha kama hali itakwenda vizuri, tulisema tutanunua magari machache na katika eneo ambalo tutatoa kipaumbele ni katika zile Wilaya ambazo Maafisa Upelelezi hawana magari, ili magari hayo wapate yawasaidie katika kufanya upelelezi wa kesi.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, amejaribu kuelezea hali halisi ya utaratibu wa mashtaka ya kawaida. Lakini naona tatizo hili la kesi zisizopelekwa Mahakamani ni kesi ambazo wananchi wanabambikizwa na Polisi. Je, amejaribu kuangalia kwa undani na kuzifutilia hizi kesi kwamba zimechukua muda gani na raia hawa wanaumia kiasi gani katika hizo kesi kucheleta kwa kiwango hicho? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kiutaratibu kila shauri ambalo linafika katika Kituo cha Polisi, kesi yoyote ya jinai inayofika katika Kituo cha Polisi, kwa utaratibu lazima iende Mahakamani tena mapema iwezekanavyo si zaidi ya saa 24, hilo shauri lazima liwe limepelekwa na ndiyo utaratibu. Sasa kama kuna kesi ambazo hazipelekwi Mahakamani kwa sababu moja au nyingine, ningependa kwa kupitia Bunge lako Tukufu, tuwaeleze wananchi kwamba, wanapokuwa na mashauri ya jinai katika Vituo vya Polisi wahakikishe kwamba zinakwenda Mahakamani mapema iwezekanavyo na kama zinacheleweshwa watoe taarifa.

La kubambikizwa kesi hili nalo siyo utaratibu na tumeshawaambia Polisi wote nchi nzima kwamba, tukikuta kuna ushahidi wa kutosha, Polisi kwa kutumia madaraka yake amembambikizia kesi mwananchi ili kumkomoa, huyo tunamfukiza kazi. Kwa sababu ni matumizi mabaya ya madaraka.

Na. 235

#### **Kituo cha Polisi Kata ya Malolo**

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Kata ya Malolo iliyoko Jimbo la Mikumi kuna mradi wa Kilimo cha umwagiliaji; na kwa kuwa Kata hiyo ina watu wengi na iko mbali na Kituo cha Polisi Mikumi; na kwa kuwa tayari majengo ya Kituo cha Polisi yamejengwa; je, ni lini kituo hicho kitafunguliwa ili kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao katika mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Wegga, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa wakati mradi wa umwagiliaji ulipoanza katika Kata ya Malolo, lilijengwa jengo dogo la ulinzi ambalo lingeliweza pia kutumiwa kama Kituo kidogo cha Polisi. Hata hivyo, kwa sasa hatuna mipango ya kufungua Kituo cha Polisi katika Kata ya Malolo kwa hakuna nyumba hata moja ya kuishi Askari. Wakati huo huo sio rahisi kwa Askari wa Mikumi kusafiri kila siku kwenda Malolo kufanya kazi na kurudi Mikumi kutoekana na umbali ambao ni karibu kilomita 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuwa na Kituo cha Polisi katika Kata ya Malolo. Hata hivyo, kwa sasa Serikali haina fedha kwa ajili ya kujenga majengo yote yanayoendana na uanzishwaji wa Kituo cha Polisi. Hivyo kupitia Bunge lako Tukufu, namwomba Mheshimiwa Mbunge na viongozi wa Mikumi na wananchi wenywewe wa Malolo, washirikiane kujenga nyumba za kuishi Askari ili Kituo cha Polisi kiweze kufunguliwa kwa madhumuni ya kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao katika eneo hilo.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa jibu zuri. Kwa kuwa

Naibu Waziri amekubali kwamba kuna majengo tuliyopewa na mfadhili na sasa tunahitajika tuhamasishe wananchi tujenge. Je, yuko tayari kutoa mabati 150 yenye thamani ya shilingi milioni mbili na laki tano pamoja na *cement* mifuko 300 na sisi tukajenge? (*Makofsi*)

**NAIBU SPIKA:** Hilo limeeleweka Mheshimiwa Mbunge. (*Kicheko*)

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitazama kwa majibu mepesi mepesi, miradi mikubwa kama mradi wa umwagiliaji wa shilingi bilioni 7.5, leo tunaangalia tu tunasema uachwe pale uibiwe hivi hivi. Hivi Serikali inatenda haki wafadhilli wanapotupa miradi mikubwa kama hii halafu Serikali iseme haina shilingi milioni mbili, je, wafadhalii wakitusikia tutakuwa tunaitendea haki Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali, tunatambua umuhimu wa kuwepo Kituo cha Polisi katika eneo lile kwa sababu ile aliyotaja Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari kuna uwekezaji mkubwa pale ambao alisema kuna gharama karibu shilingi bilioni saba. Lakini kwamba tuna miradi kama hiyo pia ipo katika majimbo mengi sana, uwekezaji wa namna hiyo, uwezo wa kujenga vituo vyote mahali pote penye uwekezaji mkubwa kama huo, Wizara yetu na ninyi wenyewe ni mashahidi, hata juzi mmetupitishia Bajeti ya Maendeleo ya Jeshi la Polisi ya shilingi bilioni 5. Sasa hizo hizo ndiyo zifanye kazi ya magari, *communication*, zijenge majengo yote, vituo vyote, kusema kweli hilo ndiyo tatizo. Ndiyo maana tunasema hivi, tushirikiane sisi hatukatui kuchangia kama wataanza ujenzi pale Malolo na sisi Wizara tunaangalia namna ya kuchangia na kwa hiyo Mheshimiwa Wegga, anza ujenzi, njoo Wizarani tuzungumze namna ya kushirikiana kati ya wananchi wa Malolo na Wizara yetu ili mpate Kituo katika eneo hilo. (*Makofsi*)

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swalii moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hata sisi kule kwetu tunajiandaa kujenga vituo vinya pale Lukozi na pale Lutai. Lakini nauliza kwamba kuna faida gani kupewa Kituo Kidogo cha Polisi kama Kituo Kidogo cha pale Mnazi kwenye Jimbo langu kilometa 100 kutoka Makao Makuu ya Wilaya, mpaka mrefu sana na nchi jirani ya Kenya, iko katika Mbuga ya Umba ya wanyamapori, Askari watano, sita, wako pale miaka kumi sasa vijana wale hawana silaha hata kisu. Vijana wale hawana usafiri hata wa baiskeli. Kuna faida gani kupewa vituo kama hivi na hii inasaidia nini ulinzi na usalama wa mali na raia wale ambapo vijana hawa wapo, Wizara haionti kuna kasoro kubwa katika eneo la namna hii, tunaomba silaha pale Mnazi inasema nini? (*Makofsi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Vituo Vidogo nya Polisi una umuhimu mkubwa sana katika maeneo mbalimbali na hasa pale katika Kituo cha Mnazi ambacho kiko mpakani. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ya kupata kile kituo ni hatua kubwa sana hiyo. Sasa inayofuata ni kukiimarisha hicho kituo kiweze kufanya kazi kwa ufanisi. Tayari tumeshapeleka Askari na bado tutaimarisha kituo hicho kwa kupeleka redio ya mawasiliano, kwa sababu sasa hivi haipo, baada ya hapo masuala ya silaha tutazama vile vyle kwa sababu ni mpakani na mpaka ni mrefu na suala la usafiri. Si lazima iwe gari. Hali ikiruhusu tukipata usafiri wa aina yoyote vile vyle tutasaidia.

Kwa hiyo, kwa kweli ni kuboresha kile kituo kifanye kazi kwa ufanisi zaidi. Kwa sababu kuwepo kwa kituo ni hatua kubwa sana. Tutashirikiana kukiimarisha ili kifanye kazi kwa ufanisi pamoja na Askari kupelekewa silaha.

Na. 236

#### **Mfuko Maalum wa Vijana**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mfuko wa Vijana ambao unachangiwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Halmashauri/Manispaa hapa nichini ni mkakati wa uhakika na endelevu wa kupunguza umaskini mionganii mwa vijana wa kiume/kike wenye ulemavu ambao wengi wao ndio wanaoathirika zaidi na umaskini hapa nichini. Je, ni vijana wangapi na wenye ulemavu wa jinsia zote wamefaidika na mikopo hiyo toka kwenye mfuko kati ya mwaka 2001 - 2003?

### **NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** aliibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna vijana wenyewe ulemavu au wasiokuwa na ulemavu waliopata mikopo kutoka katika Mfuko wa Vijana kuanzia mwaka 2001 - 2003 kwa sababu Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na mifuko mingine ilisimamishwa kuanzia mwaka 2001. Mifuko hiyo ilisimamishwa na Serikali ili kubuni utaratibu wa utoaji na usimamizi mzuri zaidi wa mifuko hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2002/2003, ilianza tena utaratibu wa kutoa fedha kwa ajili ya miradi ya vikundi vya vijana katika Wilaya zote. Aidha, tunaelekeza na kukumbusha Kamati zinazohusika na utoaji wa mikopo hiyo Wilayani kuzingatia na kutambua kuwa wenyewe ulemavu pia wanahitaji kupewa nafasi ya kujajiri kwa kupatiwa mikopo kutoka mfuko huu.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba utaratibu huu ulisitishwa kidogo ili utaratibu mpya uweze kubuniwa, je, huo utaratibu mpya unaendelea kubuniwa mpaka lini kusudi vijana hawa waweze kupata mikopo hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa atakumbuka nilipokuwa natoa jibu la swali la msingi nilisema utaratibu ule ambaa ulisimamishwa ulishaanza tena katika mwaka wa fedha 2002/2003, mwaka ulioishia juzi tarehe 30 Juni, 2003. Kwa hiyo, tayari tumeshaanza. Lakini utaratibu wa kikundi gani kipewe, kipi kisipewe, upo katika Wilaya ambako sisi ndiyo tunapeleka pesa hizo. Kwa hiyo, ni jukumu la kila Kamati inayohusika katika Wilaya zetu kuhakikisha kwamba ikiwa kipo kikundi cha vijana walemovu, basi na wao wenye wanstahili kupata haki hiyo. Kwa bahati mbaya mtu mmoja mmoja hapati mkopo huu kwa mujibu wa taratibu tulizonazo.

Na. 237

### **Fedha zinazotengwa kwa kazi za ziada kwa kila Wizara**

#### **MHE. ERNEST G. MABINA (k.n.y. MHE. KABUZI F. RWILOMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kila mwaka katika Bajeti ya Serikali, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya malipo ya kazi za ziada kwa kila Wizara; na kwa kuwa walimu wanakuwa wakifanya kazi za ziada kutokana na ongezeko la wanafunzi; je, ni walimu wangapi na wa shule zipi ambaa wanafundisha darasani wameshalipwa kutokana na kazi za ziada kama wanavyofanyiwa watumishi wa Idara nyininge?

### **WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** aliibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Kabuzi F. Rwiomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mwalimu hata mmoja anayefundisha darasani aliyelipwa kwa ajili ya kazi ya ziada ya kufundisha, kwa sababu msingi wa ajira katika taaluma ya walimu siyo idadi ya wanafunzi, muda au saa za kazi, bali ni kufundisha wanafunzi mpaka waelewe. Kwa hiyo, kutokana na msingi huo wa ajira, hakuna fedha yoyote ambayo huwa inatengwa katika Bajeti ya Serikali kwa ajili ya malipo ya ziada kwa walimu wanafundisha darasani.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa watumishi wengi wa Serikali huwa wanalipwa posho wanapotoka katika vituo vyao vya kazi kama kutoka kituo kidogo kwenda mji mkubwa na walimu huwa wanatoka vijijini kwenda Wilayani kufuata mshahara. Je, Serikali itawalipa posho walimu ambaa wanafuata mishahara yao katika Wilaya?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ni kwamba, walimu hawana malipo yoyote ya ziada ama *overtime* kwa sababu mwalimu hufanya kazi wakati wowote. Kazi ya kufundisha hutanguliwa na kazi ya kuandaa mafunzo, *lesson notes, scheme of work* na pia utaona ni jambo la kawaida kuona kila mwalimu baada ya kazi amebeba madaftari ya kwenda kusahihisha. Hiyo ndiyo *nature* ya kazi ya ualimu.

Suala la walimu wanapokwenda kufuata mishahara hilo halina uhusiano wowote na *overtime*, ni utaratibu uliowekwa wa kupokelea mshahara Wilayani na hakuna utaratibu wowote wa kumlipa mtu anayefuata mshahara wake kwamba alipwe gharama ya kusafiri. Isipokuwa pale walimu ambapo wamepangana wenyewe, kwamba yuko mmoja anakwenda kuwachukulia wenzake mshahara, wana utaratibu wao ambao wameweka katika Wilaya yule mwenzao wamlipa nini aweze kusafiri kwenda kuchukua mshahara na kurudi kuja kuwalipa wenzake.

Na. 238

### **Somo la *Hygiene* katika Shule za Msingi**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni kumetokea milipuko mingi ya maradhi ya kipindupindu na wataalamu wetu wanasema kwamba moja kati ya sababu ambazo zinasababisha maradhi hayo ni uchafu. Je, Serikali haioni kwamba ni vizuri kuanzisha somo la usafi (*Hygiene*) katika Shule zetu za Msingi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwijuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, somo la usafi (*Hygiene*), hufundishwa kuanzia katika madarasa ya Elimu ya Awali na Shule za Msingi. Katika Mtaala wa Shule za Msingi, masomo yanayofundishwa kwa madarasa yote ni Kiswahili, Kiingereza, Hisabati, Maarifa ya Jamii, Afya/Sayansi, Stadi za kazi na Dini.

Mheshimiwa Naibu Spika, somo la Afya linafundishwa kwa darasa la I na II ambapo wanafundishwa mambo yote yanayohusu usafi wa mwili, nguo, vyombo na hata usafi katika kazi zao darasani. Kuanzia darasa la III hadi VII wanafunzi hawa hujifunza somo la sayansi ambapo kipengele cha usafi (*Hygiene*) hufundishwa kwa undani zaidi kwa kuwa wamekuwa wakubwa kwa umri. Kwa hiyo, somo la usafi tayari linafundishwa katika shule zetu za msingi kwa ukamilifu unaotakiwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na maswali yamekwisha lakini nina matangazo kadhaa, lakini kabla ya matangazo naomba niseme kwamba, wakati ule Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, alipokuwa anajibu swali la Mheshimiwa James Musalika, alisema James Musalika Msabaha, nadhani alikuwa anajifikiria mwenyewe kwa hiyo, akateleza akataja jina lake mwenyewe. Kwa hiyo, kwa *record* anaitwa Mheshimiwa James P. Musalika, hilo la Msabaha nadhani aliteleza. (*Kicheko/Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo yafuatayo ni ya Mikutano ya Kamati. Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo Jumanne, tarehe 15 Julai, 2003, saa tano asubuhi, kikao kitafanyika chumba Na. 54. Kikao kingine ni Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, anawaomba Wajumbe wake wakutane katika chumba Na. 81, saa saba alasiri baada ya kuahirisha Bunge, wote wanaombwa wahudhurie. Saa saba adhuhuri ni Kiswahili cha Zanzibar au Tabora. (*Makofî*)

Tangazo lingine ni kwamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William H. Shellukindo, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane chumba Na. 58, saa tano na nusu asubuhi hii.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mwisho wa matangazo. Sasa kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri asome hotuba yake, ningependa kueleza kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambaa wangependa kujadili hoja hii. Mheshimiwa Waziri, Dr. Mary M. Nagu, atasoma hotuba lakini pia Wizara hii inajumuisha kama mnavyojua na Utawala Bora. Kwa hiyo, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, pia atashiriki katika kujibu, atajibu siyo kama Naibu Waziri, hapana, atajibu kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, kwenye Ofisi hiyo. (*Kicheko/Makofit*)

Baada hayo sasa namwita Mheshimiwa Waziri, Dr. Mary M. Nagu. (*Makofit*)

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 Ofisi ya Rais (UTUMISHI)**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutohana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Rais - Ikulu (Fungu 20 na 30), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33) na Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 36), Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa kazi kwa mwaka wa fedha 2002/2003. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuitisha Makadirio ya Fedha ya Ofisi ya Rais - Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Athuman S. M. Janguo, Mbunge wa Kisarawe, akisaidiwa na Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotupatia wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2003/2004, hatua ambayo imetuwezesha kuandaan na kuwasilisha Bungeni hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuitia Bunge lako Tukufu, naomba kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuongoza na kusimamia mabadiliko makubwa ya kiutawala, kijamii na kiuchumi katika Taifa letu. Kutohana na uongozi wake wa uwazi na ukweli amefanikisha ujenzi wa Demokrasia ya Vyama Vingi nchini kwa kuhimiza umoja kwa njia ya majadiliano na maafikiano, jambo ambalo limeifanya nchi yetu iendelee kuonekana kisiwa cha amani Barani Afrika. Pia, chini ya uongozi wake, uchumi wa nchi yetu umeweza kukua kwa kiwango ambacho kimeyavutia Mataifa ya nje na kuwafanya wawekezaji kutoka Mataifa hayo waendelee kuja nchini kwa minajili ya kuwekeza vitega uchumi na kufanya biashara. Tunatarajia kwamba mafanikio haya yatawezesha utekelezaji wa mipango mizuri itakayolenga kumwongezea Mtanzania wa kawaida pato na huduma bora ili hatimaye kuboresha hali yake ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, naomba pia nikupongeze wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa busara na hekima kubwa. Chini ya uongozi wenu mmeweza kuboresha mfumo wa kuendesha shughuli za Bunge letu Tukufu kwa kutoa nafasi zaidi kwa Waheshimiwa Wabunge kuweza kushiriki kikamilifu katika mijadala ya kiuchumi, kijamii, kisheria na kifedha, kuitia Kamati mbalimbali za Bunge. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Mbunge wa Hanang, kwa hotuba yake yenye upeo mpana, ambayo imetoa dira ya utekelezaji wa malengo ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha. Aidha, nawapongeza pia Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba zao ambazo zimebainisha misingi na mwelekeo wa Bajeti na uchumi nchini kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Ninapenda vile vile kutumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri waliotangulia kwa hotuba zao ambazo pia zimeonyesha mchango wa Wizara zao katika kulijenga Taifa letu. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya, walioshinda katika chaguzi ndogo na wanahudhuria hapa Bungeni kwa mara ya kwanza, Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga, Mbunge Jimbo la Kilombero, Mheshimiwa Edward N. Ndeka, Mbunge Jimbo la Kigoma Kusini, Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi, Mbunge Jimbo la Bukoba Vijijiini, Mheshimiwa Sumri Abdallah Salum Mohamed, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Magharibi, wote hao kutoka CCM. Vile vile napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wa *CUF* kwa ushindi wao ambao umewawezesha kuingia Bungeni. Aidha, nachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum (*CUF*), ambao wamerejeshewa uwakilishi wao Bungeni na Mahakama. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa salamu za rambirambi kwa ndugu na jamaa za Marehemu Jaji Kahwa Lugakingira, aliyekuwa Jaji wa Mahakama ya Rufaa. Kifo chake, siyo tu kwamba kimeleta majonzi kwa ndugu, jamaa na marafiki, bali pia ni pigo katika utendaji kazi wa Mahakama ya Rufaa, ambapo alikuwa anafanya kazi hadi mauti yalipomkuta. Tunamwombea Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi. (*Amin*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ninayoitao inahusu Ofisi ya Rais ambayo inajumuisha Ikulu, Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma. Nitaanza maelezo yangu kwa kutoa majukumu na mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka wa fedha 2002/2003 na baadaye nitaelezea mpango wetu kwa mwaka huu wa 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais Ikulu imeendelea na wajibu wake wa kuongoza, kufuatilia, kuratibu uendeshaji bora wa Serikali, kuchambua nyaraka na Miswada ya Sheria mbalimbali kwa lengo la kutoa ushauri kwa Rais na Baraza la Mawaziri na kusimamia utekelezaji wa maamuzi mbalimbali yanayotolewa na Rais na Baraza la Mawaziri. Kazi nyingine zilizotekelzwa ni pamoja na kusimamia Wizara katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuziba mianya ya rushwa, vile vile Ofisi iliendelea kusimamia Utawala Bora, Usalama wa Taifa, kuratibu masuala yanayohusiana na utandawazi na kushughulikia makaribisho ya viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Utawala Bora ambacho kilianzishwa mwaka 2001, kina majukumu ambayo ni kuratibu, kusimamia na kupima utekelezaji wa programu ya kujenga Utawala Bora nchini na hasa kuhakikisha kwamba, Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa unatekelezwa ipasavyo. Katika mwaka 2002/2003, yafuatayo yalifanyika:-

- Watumishi wa Kitengo wamehudhuria na kushiriki katika Warsha/Semina/Makongamano kuhusu rushwa na mbinu za kusimamia utekelezaji wa mipango ya kupambana na rushwa ndani na nje ya nchi ili kuwapatia uwezo na kuwaimarisha kiutendaji;
- Uteuzi wa Maafisa Mahsus (*Focal Persons*) wa kushughulikia masuala ya rushwa katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, umefanyika na Maafisa hao wamepatiwa mafunzo ya kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na Rushwa katika maeneo yao;
- Kusimamia urekebishaji na uboreshaji wa Mkakati wa Kupambana na Rushwa katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali ili uende na wakati;
- Kutayarisha na kuchapisha mwongozo wa matumizi ya fedha zinazotengwa kwa madhumuni ya kupambana na rushwa Wizarani (*The National Integrity Fund Manual*).
- Kusimamia utafiti na utayarishaji wa Taarifa ya Hali ya Rushwa Nchini kwa mwaka 2002 (*The Annual State of Corruption in Tanzania*) kwa kushirikiana na wahisani na Taasisi ya kuzuia rushwa; na
- Kuendesha warsha juu ya Utawala Bora kwa wamiliki wa vyombo vya Habari na Wahariri wa Habari kwa lengo la kuwaelewesha na kuwashirikisha katika kutekeleza mpango wa kupambana na rushwa na kujenga uwezo wao wa kuanzisha (*Investigative Journalism*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2002/2003, Taasisi ya Kuzuia Rushwa iliendelea na kazi ya kuelimisha wananchi juu ya madhara ya rushwa kwa njia ya mafunzo, mikutano, matangazo kupitia vyombo vya habari (redio, luninga, vipeperushi, magazeti na kadhalika). Vile vile Taasisi ya Kuzuia Rushwa ilipokea na kuchunguza tuhuma mpya 1,103 na iliendelea na uchunguzi wa majalada ya miaka ya nyuma 2,633. Majalada 467 yalifungwa baada ya kukosekana ushahidi, majalada 22 yalielekezwa kwa waajiri husika kwa hatua za nidhamu, majalada 15 yalipelekwa kwenye Idara nyingine ili yashughulikiwe na majalada 179 yalipelekwa Mahakamani ambapo kesi 11 zilitolewa adhabu na kesi 26 zilishindwa na watuhumiwa kuachiwa huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Taasisi iliandaa marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Rushwa Na. 16/1971, pamoja na kufanya utafiti katika maeneo ya utoaji leseni za biashara, ajira ya utoaji huduma katika Shirika la Nyumba la Taifa kwa lengo la kubainisha mianya ya rushwa. Juhudi zote hizi zimewesheza kuhamasisha wananchi wasitoe na kupokea rushwa. Pia Taasisi imeimarisha Ofisi zake za Mikoa na Wilaya ambapo katika kipindi hicho watumishi wapya 159 walajiriwa na imefungua Ofisi katika Wilaya 46. Maafisa wa Taasisi wamepewa mafunzo ya ujuzi na kujiendeleza ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo na mbinu za kisasa za kiuchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, *Tanzania Social Action Fund (TASAF)*, ambao ulianzishwa mwaka 2000 ili kujenga uwezo wa jamii katika kupanga, kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo, inayolenga kuondoa kero za wananchi na kuwaondolea umaskini, miradi 469 ya huduma za jamii na miradi 65 ya ujenzi ilitekelezwa na kukamilishwa. Ukarimilishaji wa miradi hiyo umewezesha upatikanaji wa huduma zilizokusudiwa kwa wananchi. Pia, wananchi Vijijini wamedhihirisha uwezo mkubwa wa kusimamia kazi za maendeleo yao kwa kutekeleza miradi hiyo kwa viwango vya ubora ulioainishwa na sekta husika. Tunawapongeza wananchi hao kwa kazi nzuri. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ilipanga na kutekeleza shughuli zinazolenga kujenga uwezo wa watumishi wa Taasisi za umma ili kuboresha utoaji huduma, tija, uwajibikaji, usimamizi wa kazi na uendelezaji wa raslimali watu katika utumishi wa umma kama ifuatavyo:-

- Kuwezesha Wizara kumi na moja, Idara zinazojitegemea mbili na wakala tatu za Serikali kuandaa mipango ya mikakati ya utekelezaji kazi (*Strategic Plans*), kuandaa Bajeti inayolenga kwenye matokeo (*Performance Budget*) na kuwawezesha baadhi ya watumishi waandamizi katika asasi hizo kuingia mikataba ya utendaji (*Performance Agreements*) na wasimamizi wao wa kazi;
- Kuzindua Mikataba ya Huduma kwa Mteja katika Wizara 10, Wakala tatu za Serikali na Idara zinazojitegemea moja;
- Kuzindua Wakala tatu za Serikali na hivyo kufanya idadi ya Wakala zilizokwisha zinduliwa kufikia 21;
- Kushirikisha Sekta Binafsi katika kutoa baadhi ya huduma zilizokuwa zinatekelezwa na Serikali. Mpango huu umetekelezwa katika Wizara nane, Wakala mbili za Serikali na Mikoa miwili;
- Kukamilisha uanzishwaji rasmi wa Tume ya Utumishi wa Umma kulingana na Sheria Na. 8 ya 2002, kuandaa Kanuni za Utumishi wa Umma, taratibu za uendeshaji wa utumishi wa umma na taratibu za uendeshaji wa utumishi Serikalini;
- Kusimamia ajira Serikalini ambapo hadi Mei, 2003 jumla ya vibali 21,384 vilitolewa kwa ajili ya kuajiri watumishi wapya na wa mbadala. Kati ya vibali hivyo, 14,334 ni kwa ajili ya kuajiri walimu wa shule za msingi na sekondari;
- Kuratibu upandishwaji vyeo na uthibitishaji kazi watumishi wa kada ambazo miundo yao ya utumishi inasimamiwa na Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

- Kuelimisha umma kuhusu maadili, sheria, kanuni na taratibu za utendaji kazi katika utumishi wa umma kupitia redio, luninga, magazeti, vipeperushi na semina/warsha;
- Kupokea na kushughulikia malalamiko yanayotolewa na wananchi dhidi ya utendaji kazi katika utumishi wa umma;
- Kukamilisha miundo 129 ya maendeleo ya watumishi wa Serikali;
- Kuhuisha miundo na majukumu ya kazi ya Wizara na Idara zinazojitegemea nane;
- Kuhuisha taratibu za ajira ya wataalam wa kigeni;
- Kufanya uchambuzi wa kumbukumbu katika Wizara tisa na kutenganisha kumbukumbu hai na zile ambazo hazitumiki kila siku;
- Kuandaa Sera ya Mafunzo ambayo inatoa mwongozo na mikakati sahihi ya mafunzo kwa waajiri katika utumishi wa umma; na
- Kuwapatia Watendaji Wakuu wa Serikali mafunzo ya kusimamia utekelezaji wa Sera za Serikali hasa ile ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Sera ya Serikali Elektroni (*e-Government*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendeleza uwezo wa kuutendaji wa watumishi wa umma (*Capacity Building*), ikiwa ni moja ya njia muhimu ya kuchangia katika ukuaji wa uchumi wetu, Chuo cha Tanzania cha Utumishi wa Umma, kiliendesha kozi 87 zilizojumuisha washiriki 3,609. Kozi 41 kati ya hizo zilikuwa za uongozi, utawala na menejimenti ambazo zilikuwa na washiriki 944, kozi 30 zilikuwa za mafunzo ya kompyuta na zilishirikisha watumishi 965, kozi 16 zilikuwa za uhazili ambapo zilihudhuriwa na washiriki 1,700. Aidha, chuo kiliendelea kutoa mafunzo yanayolenga kuwaendeleza watumishi wa umma katika ajira zao (*Career Development*). Mafunzo haya ni pamoja na:-

- Mafunzo maalum ya kuwaandaa Maafisa Utumishi kufanya mitihani ya Serikali ya kitaaluma;
- Mafunzo maalum ya kuwaandaa Maafisa Tawala kufanya mitihani ya Sheria;
- Mafunzo ya kuwaandaa watumishi kufanya mitihani ya ngazi ya juu na ngazi ya chini ya Uhaisbu Serikalini;
- Mafunzo ya uongozi ya ngazi ya juu ya utumishi; na
- Mafunzo ya awali ya Wasaidizi wa Masjala.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kituo cha Tanzania cha Mafunzo kwa njia ya mtandao ambacho kinaendesha shughuli zake chini ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha, kiliendesha mafunzo kwa viongozi na watumishi mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na kushiriki kwenye midahalo ya Kimataifa na mafunzo yanayotolewa kwa kutumia teknolojia ya Setelaiti. Aidha, mafunzo yaliyoendeshwa yalihusu uongozi bora, mbinu za kuondoa umaskini, maendeleo Vijijini, usimamizi wa fedha, uendeshaji wa Serikali za Mitaa, mazingira, elimu ya Ukimwi na uandishi wa habari. Pia, kituo kiliendesha mafunzo ya kompyuta kwa jumla ya viongozi 43 wakiwemo Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Makatibu Tawala wa Mikoa. Mafunzo yote haya yalilenga kujenga uwezo wa uongozi na uwezo wa utendaji kazi, ubunifu na matumizi ya teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka takriban saba tangu Serikali ya Awamu ya Tatu iingie madarakani, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imeendelea kuboresha uwiano uliopo kati ya wanawake na wanaume walioajiriwa Serikalini. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa ajira ya wanawake Serikalini sasa imefikia asilimia 34 katika ngazi za chini, asilimia 39 katika ngazi ya kati. Kwa upande wa uongozi asilimia 24 ya Makatibu Wakuu ni wanawake, kwa ngazi ya Ukurugenzi wanawake ni asilimia 26 na kwa ngazi ya Wakurugenzi Wasaidizi wanawake ni asilimia 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo huu ni matokeo ya hatua za makusudi za kujenga na kuendeleza uwezo wa wanawake kwa njia ya mafunzo na udhamini ambao Ofisi yangu imekuwa ikiutoa kwa kupitia Mfuko wa Kuendeleza Watumishi Wanawake. Mwaka uliopita Mfuko huu ultumika kuwadhamini wanawake 20 wanaojifunza mafunzo ya stashahada na shahada za uzamili. Pia, Mfuko ulidhamini wanawake 115 katika mafunzo ya muda mfupi yanayolenga kuongeza uwezo na ujuzi wa kazi. Ofisi itaendeleza juhudhi hizi na kutoa fursa sawa kwa watumishi wa jinsia zote, ambayo ndiyo misingi ya Sera ya Menejimenti na Ajira, pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 na nina imani kuwa muda si mrefu, nchi yetu itafikia malengo ya makubaliano ya Beijing (*Beijing Plat-form for Action*) ya kuwa na asilimia 30 ya wanawake katika ngazi ya uongozi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ilichunguza malalamiko 65 yaliyowasilishwa na wananchi juu ya baadhi ya viongozi kukiuka maadili ya uongozi, pia ilipokea na kuhakiki tamko la mali na madeni ya viongozi wa umma kwa mujibu wa Sheria kutoka kwa Viongozi 5,510. Aidha, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, iliendelea kutoa elimu ya maadili ya Uongozi kwa wananchi na Viongozi kwa njia ya redio na semina. Jumla ya vipindi 52 vya redio vilitangazwa na semina kwa Madiwani na Watendaji zilifanyika katika Halmashauri saba za Miji na Wilaya. Halmashauri hizo ni Ngara, Biharamulo, Kilosa, Mwanga, Misungwi, Kwimba na Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilianza kutekeleza Mradi wa Kukuza Maadili (*Ethics Promotion Project*), unaojumuisha mafunzo ya kitaalam kwa watumishi, ununuzi wa vifaa na uhamasishaji wa wananchi kuhusu maadili ya viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2002/2003, Tume ya Utumishi Serikalini, ilitekeleza majukumu yake ya kusaili, kuajiri katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni, kuthibitisha kazini watumishi waliotimiza muda wao wa majoribio vizuri, kupandishwa vyeo na kusikiliza kesi za rufaa za watumishi mbalimbali. Aidha, Tume iliandaa na kuendesha mitihani ya Serikali na vile vile kufanya mikutano na watumishi katika Mikoa sita na Wizara/Idara zinazojitegemea saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha 2003/2004, Ofisi ya Rais - Ikulu, itaendelea kufuatilia na kuratibu Utawala Bora na kusimamia uendeshaji wa shughuli za Serikali. Aidha, Ofisi itaendelea kuchambua mambo mbalimbali ya kisera na kuchambua Miswada ya Sheria kwa lengo la kumshauri Rais na Baraza la Mawaziri. Kazi nyininge zitakazofanywa ni kuendelea kuratibu utendaji kazi wa vyombo vya dola kuhusu Usalama wa Taifa, kuimarisha masuala ya mawasiliano kwa umma na kutoa ufanuzi wa masuala mbalimbali kwa wananchi. Aidha, Ofisi itaanza kukarabati jengo la mapokezi na jengo linalotumiwa na Askari wa FFU.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha majukumu ya kupambana na rushwa nichini, Taasisi ya Kuzuia Rushwa itaendelea na utafiti kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa na kutoa mapendekezo ya namna ya kuiziba hasa katika maeneo yanayolalamikiwa sana. Aidha, Taasisi itaendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi juu ya haki zao, madhara ya rushwa na jinsi ya kupambana na kujiupusha na vitendo vya rushwa. Ili kuhakikisha elimu hii inawafikia wananchi wengi tutatumia njia zote za kutolea habari ikiwa ni redio, luninga, magazeti na vipeperushi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jukumu la kuzuia rushwa, Taasisi pia huchunguza wale wanaoendelea kushiriki katika vitendo vya rushwa. Katika kutimiza jukumu hili Taasisi itatekeleza yafuatayo:-

- Kuimarisha Kitengo cha Upokeaji Taarifa (*Intelligence Unit*), ili kiweze kuchuja malalamiko ya vitendo vya rushwa yanayopokelewa kwa kufanya uchunguzi wa awali kabla ya uchunguzi halisi. Utaratibu huu hupunguza uwezekano wa kuchunguza tuhuma ambazo si za kweli au ni za makosa ambayo hayahusiani na rushwa kwa kuyapeleka kwenye vyombo husika;

- Kufanya uchunguzi wa majalada 3,197 yaliyopo na yatakayofunguliwa kwa kuweka kipaumbele katika uchunguzi wa tuhuma zilizo na maslahi zaidi kwa Taifa; na
- Kuendesha kesi 142 ambazo bado ziko Mahakamani na nyingine zitakazofunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Taasisi itaendelea kuimarisha uendeshaji wa shughuli zake kwa kununua vifaa na nyenzo za kazi, kutoa mafunzo kwa Maofisa na kukamilisha ufunguzi wa Ofisi ya Taasisi katika Wilaya zilizosalia Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, *Tanzania Social Action Fund (TASAF)* katika mwaka huu wa fedha miradi 570 ya jamii na 120 ya ujenzi inategemewa kukamilishwa. Aidha, *TASAF* itaendelea kuwezesha Wilaya kufanya pembuzi shirkishi jamii (*Participatory Rural Appraisal*) na kuainisha mahitaji ya jamii hizo ili kupata miradi mipya. Idadi ya miradi mipya itategemea mahitaji halisi ya wananchi yatakayojoitokeza kutokana na zoezi hilo la upembuzi shirkishi jamii utakaofanywa katika kipindi hicho hicho. Pia, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, maandalizi ya awamu ya pili ya *TASAF* yataanza katika mwaka huu wa fedha ili awamu ya pili ianze mara tu baada ya kipindi cha awamu ya kwanza kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kila mmoja wetu anaelewa na ameshaona juhudzi zinazofanyika kuboresha utumishi wa umma nchini. Msimamizi Mkuu wa utekelezaji wa shughuli hizi ni Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kutokana na jukumu hili muhimu, imelazimu kuangalia upya muundo na kazi za Ofisi hii kwa lengo la kuimarisha na kuboresha utendaji kazi wake ili iweze kusimamia vizuri mabadiliko yanayoendelea nchini. Hatua hii imesababisha kubadili jina la Ofisi hii na kuwa Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Mheshimiwa Rais tayari ameridhia muundo mpya na jina jipya limeanza kutumika rasmi tokea Julai, Mosi, 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha 2003/2004, Ofisi hii itaendelea na juhudzi za kuboresha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma. Nguvu zetu zitaelekezwa katika maeneo yafuatayo: Kwanza, kuboresha mifumo ya usimamizi na utendaji kazi, pili, kupanua utaratibu wa kupima kazi unaozingatia malengo na matokeo ya kazi (*Results-Oriented Management*); tatu, kuongeza ubunifu na kujenga uwezo wa watumishi kwa njia ya mafunzo ya utendaji kazi na nne, ulipaji wa ujira unaozingatia taaluma ya mtumishi na kutoa tuzo kwa watumishi wanaojibidiisha zaidi na kufanya kazi kwa uadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza hapa kwamba, ubora wa utumishi wa umma utatuhakikishia Serikali safi na imara, huduma nzuri kwa wananchi na ukuaji wa kasi zaidi wa uchumi wetu. Serikali safi na imara ni muhimili muhimu wa uchumi wa kisasa, huduma bora na maendeleo ya kisasa yatakayomhakikishia mwananchi maisha bora. Kero zilizopo sasa, vitendo vya utoaji na upokeaji rushwa na utendaji kazi hafifu katika maeneo mbalimbali, yote yanaashiria kwamba bado kuna mapungufu katika

mifumo na katika taratibu za uendeshaji na utendaji kazi katika utumishi wa umma. Hivyo, tunahitaji kurejesha heshima na hadhi ya Utumishi wa Umma ipasavyo. Kama ambavyo Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, alivyowahi kusema katika hotuba yake wakati wa kuzindua Awamu ya Pili ya Mpango wa Kuboresha Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma tarehe 20 Juni, 2000, naomba kunukuu na ilikuwa kwa lugha ya Kiingereza: "One wit, who was rather unkind to the public service once said: "Bureaucracy is governmental officialism where the civil servant is the uncivil master. We must through this Public Service Reform Programme, put such derogative remarks to rest". Kwa hiyo, lazima tuyamalize hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002, iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 2002 na kuanza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2003 ni nguzo kuu katika suala la usimamizi na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Sheria hii inawapa Watendaji Wakuu, mamlaka kamilifu katika kusimamia masuala ya kiutumishi na utendaji kazi katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Serikali za Mitaa. Kulingana na Sheria hii Watendaji Wakuu wamepewa madaraka ya kuajiri, kupandisha vyeo, kusimamia mafunzo na kudhibiti nidhamu. Ni matarajio yetu kwamba, maamuzi yote yanayohusu utendaji kazi katika utumishi wa umma sasa yataamuliwa na kutekelezwa sehemu za kazi moja kwa moja bila kungojea maamuzi kutoka kwagineko. Kwa maana nyingine mapungufu na udhaifu wa baadhi ya watumishi kama vile uzembe, utoro, kukosekana kwa uadilifu, ufuutiliaji hafifu na kutowajibika ni mambo ambayo yataweza kudhibitiwa kwa kutumia Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ni juu ya Watendaji Wakuu kuhakikisha kuwa wanaielewa Sheria hii vizuri katika kusimamia kazi bila kuwaonea au kupendelea watumishi. Sheria hii itumike bila ya woga kusimamia uendeshaji wa utumishi wa umma. Ni wajibu wa waajiri na waajiriwa katika utumishi wa umma kutambua kuwa kila mmoja anao wajibu wa kutoa mchango wake katika kuendeleza nchi yetu. Kila mtu akifanya kazi kwa bidii kwa kuzingatia Sheria na taratibu zilizowekwa tutaweza kupiga hatua nzuri katika juhudzi za kuwaletaa Watanzania hali nzuri ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tayari Ofisi yangu imekamilisha uandaaji wa Kanuni za Utumishi wa Umma na Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria hii. Ningependa kusisitiza kwamba, waajiri na watumishi wote wazisome na kuzielewa kwa kina na wazitekeleze ili kila mmoja katika nafasi yake aelewé ni nini mchango wake, stahili yake na wajibu wake katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha Serikali kujimarisha na kujikita zaidi katika kutekeleza majukumu yake muhimu (*Core Activities*) kuhusu kutunga sera, kusimamia sheria, amani, Utawala Bora na kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya ustawi wa sekta binafsi, katika mwaka huu wa fedha tutatekeleza mipango inayolenga kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na uwajibikaji kama ifuatavyo:-

- Kuendelea kuiwezesha Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa kuandaa Mipango ya Mikakati ya Utekelezaji kazi (*Strategic Plans*), kwa kuzingatia dira za sekta zao. Mikakati hii ndiyo itakayokuwa msingi wa kuweka malengo ya kazi, kufanya makisio ya fedha za utekelezaji wa mipango hiyo na upimaji utendaji kazi. Aidha, masuala ya ajira, upandishwaji vyeo, nyongeza ya kila mwaka ya mshahara na ulipaji wa ujira vitategemea matokeo ya kutekeleza malengo ya kazi;

- Kuendelea kuanzisha Wakala wa Serikali ili ziweze kutekeleza majukumu yale ambayo yana mwelekeo wa kuiyendesha na kujitegemea kwa lengo la kuipunguzia Serikali gharama za uendeshaji. Kwa mwaka 2003/2004 tumepanga kuanzisha Wakala nane;

- Kushirikisha sekta binafsi kufanya baadhi ya shughuli zilizokuwa zinafanywa na Serikali kama njia mojawapo ya kuboresha utendaji kazi na pia kuongeza ajira ili kupunguza umaskini. Tunayo malengo ya kuiwezesha Wizara na Idara zinazojitegemea 16 kuingia katika mpango huu katika mwaka 2003/2004;

- Kuimarissha demokrasia ndani ya nchi yetu kwa kuendelea na uzinduzi wa mikataba ya huduma kwa mteja kwa Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali ili kuwapatia wananchi vigezo wanavyoweza kutumia kupima utendaji kazi katika Ofisi za Utumishi wa Umma;

- Kufuatalia utekelezaji wa mikataba ya utendaji kazi ambayo kila mtumishi wa umma atatakiwa kusaini na mkuu wake wa kazi ili kuwezesha upimaji mzuri wa utendaji kazi wake. Wizara zote, Idara zinazojitegemea na Mikoa watatakiwa kuanza kutekeleza utaratibu huu; na

- Kutengeneza taratibu za utendaji kazi (*Codes of Good Practice*) katika nyanja muhimu na nyeti kama vile ajira, nidhamu, upunguzaji wa watumishi na kushughulikia kero zinazowasibu watumishi kazini na kadhalika ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria Mpya ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuimarissha ajira katika sekta nyeti na kuwapandisha vyeo watumishi wenye utendaji mzuri wa kazi, Ofisi itaendelea kutoa vibali na kuratibu ajira za watumishi wapya na mbadala kwa ajili ya kujaza nafasi katika Sekta za Elimu, Afya, Mahakama, Polisi, Magereza, Sheria na Uhaisi. Tutashirikiana na Tume ya Utumishi wa Umma kuhakikisha kuwa waajiri wote wanatekeleza majukumu yao ya ajira na upandishwaji vyeo kwa misingi ya haki na ushindani (*meritocracy*). Aidha, Ofisi yangu inaangalia uwezekano wa kuwapangia kazi moja kwa moja wahitimu wa fani ambazo waajiri wanashindwa kupata wataalam kwa njia ya kutangaza nafasi hizo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuhakikisha kuwa ajira na upandishwaji vyeo vinafanyika kwa haki na ushindani, utaratibu wa kutangaza nafasi za kazi Kitaifa na kutoa muda wa kutosha kwa waombaji kuwasilisha maombi yao, kuweka vigezo vinavyooleweka na kupimika katika usaili na utaratibu mzuri na wa wazi wa uteuzi wa washindi kwa nafasi husika vinasisitizwa sana ili kudhibiti ajira zenye

mwelekeo wa kikabila, kindugu au kirafiki. Hili linafanyika kwa madhumuni ya kulinda umaja wa Taifa letu. Lengo la Sheria mpya ya Utumishi wa Umma ni kukasimu madaraka bila kukwepa wajibu wa kuhakikisha kuwa Utaifa unapewa kipaumbele katika kanuni na taratibu zetu za utendaji na uendeshaji wa utumishi wa umma. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jithada zinazoendelea kuboresha utendaji kazi katika utumishi wa umma lipo suala la kujenga uwezo wa kuitendaji wa taasisi na watumishi wa umma. Mfumo wa sasa wa demokrasia ya vyama vingi vyenye itikadi tofauti, kasi ya uvumbuzi wa teknolojia mpya inayopokelewa na kutumiwa katika nyanja zote za utendaji kazi na kusambaa kwa uchumi wa soko huria vinahitaji kuendeshwa na kusimamiwa na watu wenye uwezo mkubwa wa kuelewa na kuamua. Hivyo, suala la kuendeleza na kujenga raslimali watu katika utumishi wa umma lina umuhimu wa pekee.

Kutokana na kutambua umuhimu huu Ofisi ilitoa mwongozo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa na kuagiza kwamba waandae mipango ya mafunzo kwa watumishi wao na kuhakikisha kwamba kila mwaka wanatenga fedha katika Bajeti zao kwa ajili ya kutekeleza mpango huo. Tutaendelea kufuatilia utekelezaji wa maagizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuhimiza mipango ya mafunzo kwa watumishi wa umma, jithada zinafanywa pia kuimarisha Chuo cha Tanzania cha Utumishi wa Umma na Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo Duniani (*Tanzania Global Development Learning Center*), ili kwa pamoja wawe na uwezo wa kutoa mafunzo ya ujuzi ya muda mfupi kwa Watendaji Wakuu kutoka Serikalini na taasisi mbalimbali.

Aidha, katika mwaka huu wa fedha, tunaendelea kukipatia Chuo cha Utumishi wa Umma, walimu, vifaa na kukifanyi ukarabati kwa lengo la kukipa hadhi ya kuweza kufanya tafiti ambazo matokeo yake yanaweza kuboresha na kukidhi mahitaji ya mafunzo hapa nchini kuliko kuendelea kutegemea vyuo vya nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo Duniani kilianzishwa Juni, 2000. Hiki ni moja ya vituo vya kwanza duniani vinavyotumia teknolojia ya kisasa ya mawasiliano na habari kwa njia ya Setelaiti. Kwa kupitia kituo hiki, viongozi na wataalam mbalimbali katika utumishi wa umma wamepata nafasi ya pekee ya kuweza kushiriki kwenye midahalo ya Kimataifa, mafunzo na kubadilishana mawazo na wataalam wengine nje ya nchi.

Hivi sasa majadiliano yanaendelea na wafadhili ili kuona uwezekano wa kusambaza teknolojia ya mafunzo ya aina hii katika maeneo mbalimbali nchini ili watumishi, wataalam katika nyanja tofauti na wananchi kwa ujumla, waweze kunufaika na kituo hiki cha mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo ya kina kuhusu jithada zinazofanywa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kujenga uwezo wa taasisi zetu na ule wa watumishi wa umma, naomba sasa nitoe kwa muhtasari yale ambayo tumepanga kuyatekeleza katika eneo hili kwa mwaka 2003/2004:-

- Kufuatilia na kutathmini wajibu wa wataalam wa kigeni wanaoajiriwa kwenye utumishi wa umma, kuhakikisha ajira hizi zinaenda sambamba na kujenga uwezo kwa watalaam wetu wanaofanya kazi nao;

- Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya kuandaan mipango ya mafunzo kwa watumishi kwa kila Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea na kutenga fedha za mafunzo katika Bajeti za kila mwaka; na

- Kuendesha mafunzo kwa ajili ya wataalam wa Sekretarieti za Mikoa na Wakuu wa Wilaya, Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, haitakuwa vyema kusitiza juu ya umuhimu wa kuwaendeleza watumishi wa umma, bila ya kuzungumzia tatizo la janga la UKIMWI ambalo linagusa kila sehemu ya

utumishi wa umma. Kwa kutambua athari kubwa itokanayo na janga la UKIMWI hasa tukizingatia kuwa UKIMWI si tu unapunguza idadi ya watumishi bali pia unachukua watumishi wenyе vipaji na uzoefu mkubwa. Ofisi yangu inajumuika na wadau wengine kupanga na kutekeleza mikakati ya kupambana na janga hili. Tunao mpango wa kuhimiza utekelezaji wa maadili ya utumishi wa umma ambayo yakizingatiwa yatawaepusha watumishi kwa kiasi kikubwa kuijingiza katika vitendo na tabia zinazoweza kuwasababishia maambukizi. Nichukue nafasi hii kwa mara nyininge kuwaasa watumishi wa umma kujiepusha na tabia na mienendo ya maisha inayohatarisha afya zao hasa kutokana na janga hili la UKIMWI.

Mojawapo ya mambo muhimu katika kujenga Utawala Bora ni ulipaji wa mishahara mizuri kwa watumishi wa umma. Matatizo mengi ya kiutendaji na ambayo yanaathiri Utawala Bora katika utumishi wa umma yanásababishwa na malipo yasiyokidhi gharama halisi za maisha, yasiyozingatia matokeo ya kazi na yenye motisha na vivutio hafifu. Ili kuondokana na tatizo hili, Serikali imekuwa ikitekeleza Sera ya Muda wa Kati ya Malipo ya Mishahara (*Medium-Term Pay Policy*), inayozingatia utaalām wa mtumishi, mchango wake katika kutekeleza malengo na matokeo ya kazi na pia uwezo wa uchumi wa kumudu ongezeko la mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyokwishatoa maelezo katika Bunge hili, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba katika mwaka huu wa fedha 2003/2004, Serikali imetenga kiasi cha shilingi 34.5 bilioni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara ya watumishi. Kutokana na matokeo ya makubaliano kati ya Serikali na Chama cha Wafanyakazi, TUGHE, kiasi hiki kitatuwezesha kurekebisha viwango vya mishahara ya watumishi kwa viwango vya kati ya asilimia 6 - 10. Watakaofaidika na nyongeza ya asilimia 10 ni Walimu ambao wametengewa asilimia 54.4 ya kiasi hiki wakati wao ni asilimia 49, makundi mengine yatakayofaidika kwa nyongeza ya asilimia 10 ni wataalam wa fani za Umdatari, Wanasheria, Uhaisbu na wataalam wa mifumo ya mawasiliano. Mgawanyo huu unalingana na maelekezo ya Sera ya Kati ya Malipo ya Mishahara kwa watumishi wa umma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Sekretarieti ya Maadili ya Umma itaendelea kutekeleza majukumu iliyopewa kwa mujibu wa sheria na kipaumbele kitawekwa katika maeneo yafuatayo:-

- Kufungua Ofisi nne za Kanda katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya na Mtwara, ili kusogezza huduma karibu zaidi na wananchi. Ofisi za Kanda za Mwanza na Tabora zinatarajiwa kufunguliwa katika mwaka wa fedha wa 2004/2005;

- Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kukuza maadili kwa kutoa mafunzo kwa watumishi, ndani na nje ya nchi. Aidha, mafunzo ya maadili yatatolewa kwa Wakurugenzi wa Utawala na Utumishi wa Wizara na Idara mbalimbali za Serikali. Kazi nyininge zitakazotekelawa ni kuhuishaa sheria, kanuni na taratibu za usimamizi wa maadili na kutoa elimu kwa umma; na

- Kukamilisha uchunguzi wa malalamiko yaliyopokelewa mwaka 2002/2003 na kuanzisha uchunguzi wa malalamiko mapya yatakayopokelewa. Vile vile Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi itaendelea kutoa elimu ya maadili kwa umma na kwa viongozi kwa njia ya semina, vipindi vya radio, mabango (*posters*) na michezo ya kuigiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Tume ya Utumishi wa Umma itaanza kazi yake rasmi mwaka huu wa 2003, mara tu baada ya Makamishna wake kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. Tunategemea kwamba Tume ya Utumishi wa Umma, katika kuendeleza juhudzi za usimamizi na uwajibikaji wa utendaji kazi, itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa viongozi na watendaji wakuu katika sehemu za kazi wanatimiza malengo yao ya kazi na kuwa wanafuata taratibu na kanuni zilizowekwa katika kushughulikia masuala ya kiutumishi. Kwa maana nyininge Tume itaratibu na kufuatilia utekelezaji wa malengo ya kazi za kiutumishi katika Wizara, Idara, Mikoa na sehemu nyininge za kazi. Kazi za Tume hii zimeainishwa katika Kifungu cha 10 cha Sheria Na. 8 ya mwaka 2002. Natoa wito kwa viongozi wote sehemu za kazi kutekeleza wajibu wao wa kusimamia kazi kwani wasipofanya hivyo itabidi wapishe wengine wenyе uwezo kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais pamoja na Asasi zilizo chini yake na ambazo zimejumuishwa katika hotuba hii, kwa pamoja inalo jukumu maalum la kujenga Serikali madhubuti yenye uwezo wa kusimamia maendeleo ya Taifa hili kwa kuimarisha huduma kwa wananchi na kwa vyombo vingine nya uzalishaji na kwa njia ya kusimamia Utawala Bora, wenyewe haki na usawa na unaojenga mazingira yenye utulivu na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali madhubuti itatokana na watumishi wa umma wanaoaminika, wenyewe kuchukua hatua sahihi pale wanapotakiwa kufanya hivyo kutekeleza wajibu wao kitaalam na kwa moyo na kukumbuka kuwa wapo kazini kutokana na dhamana waliyopewa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwa dhati kuwa Serikali ilio madhubuti na inayoendeshwa kwa misingi ya haki na usawa ni nguzo ya msingi katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Pia ni dhahiri kuwa maendeleo ambayo yameanza kuonekana sasa kama vile ukuaji wa Pato la Taifa la asilimia 6.2 kwa mwaka uliopita ni matokeo ya baadhi ya juhudhi ambazo Serikali imekuwa ikizichukua kujenga utawala madhubuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zote ambazo zimekuwa zikitekelezwa na Ofisi hii na taasisi zake zimelenga kwa njia moja au nyingine katika kujenga Serikali madhubuti yenye uwezo wa kusimamia maendeleo ya Taifa hili na wananchi wake. Pia kazi zote ambazo Ofisi hii na Taasisi zake tumejipangia kuzitekeleza kwa mwaka huu wa fedha zinalenga kuimarisha zaidi uwezo huu wa Serikali ili hatimaye tufikie viwango nya ukuaji wa Pato la Taifa vitakayotuwezesha kuondoa adha ya umaskini kwa wananchi wetu, viwango ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, alivielezea katika hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi ambayo tunatarajia kuyatekeleza kwa mwaka huu wa fedha ni malengo ambayo yamo katika Programu ya Kuboresha Utendaji Kazi na Utoaji Huduma Bora katika Utumishi wa Umma (*Public Service Reform Programme*). Napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru viongozi wote wa kisiasa na kicutendaji na hasa Waheshimiwa Wabunge, kwa kuilewa na kuipa msukumo maalum programu hii na kwa ushirikiano wao mkubwa katika kueneza ujumbe wa programu hii na hivyo kurahisisha utekelezaji wa malengo yake kwa mapana ya nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio katika Ofisi ya Rais na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi Serikalini, kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na misaada toka nchi rafiki na mashirika mbalimbali. Nachukua nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika yafuatayo: Uingereza, Uholanzi, Malaysia, India, Ujerumani, Australia, New Zealand, Singapore, Pakistan, Misri, Thailand, Uswisi, Benki ya Dunia, NORAD, JICA, UNDP, UNIDO, DANIDA, CIDA, SIDA, USAID, ACBF, Jumuiya ya Madola na Jumuiya ya Ulaya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia hotuba yangu, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Wilson Masilingi, kwa ushirikiano wake mkubwa katika kusimamia majukumu tuliyopewa na katika matayarisho ya hotuba hii. Aidha, ninapenda kuwashukuru Katibu Mkuu Kiongozi, Ndugu Matern Y.C. Lumbanga; Katibu Mkuu (Utumishi), Ndugu Jospeh A. Rugumyamheto, Katibu Mkuu (Ikulu), Ndugu Abel W. Mwaisumo, Wenyevit, Makatibu wa Tume na Taasisi mbalimbali na watumishi wote walioko katika Wizara, Mikoa na Wilaya na Idara zinazojitegemea siyo tu kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa wanaotoa katika kufanikisha malengo ya Serikali katika sehemu zao za kazi, bali pia kwa mchango wao uliowezesha matayarisho ya hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Ofisi ya Rais - Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma, ziweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2003/2004, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.54,313,390,600 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.44,459,494,100 kwa ajili ya miradi ya Maendeleo kwa mgawanyo ufuataao:-

(a) Ikulu:-

- Fungu 20: Sh.3,496,209,000 kwa ajili ya matumizi ya Kawaida ya Mfuko Mkoo wa Serikali.

- Fungu 30: Sh.44,748,306,100 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.33,122,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

(b) Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma:-

- Fungu 32: Sh.4,925,170,800 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh.11,337,494,100 kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

(c) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma:-

- Fungu 33: Sh.501,374,900 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

(d) Tume ya Utumishi wa Umma:-

- Fungu 36: Sh.642,329,800 kwa ajili ya Matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninapenda kukushukuru tena na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. RAMADHANI H. KHALFANI (k.n.y. MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na.81(1), ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2003, naomba kuwasilisha taarifa na maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Athumanji Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na mimi ninayewasilisha taarifa hii. Makatibu wa Kamati ni Ndugu Nenelwa Mwihambi na Ernest Zulu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 13 Juni, 2003, Kamati yangu ilipitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2002/2003. Aidha, Kamati yangu ilipokea taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2003/2004, kwa mafungu yafuatayo: Fungu 20 - Mfuko Mkuu wa Serikali, Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Ikulu, Fungu 32 - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Fungu 36 - Tume ya Utumishi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizo ziliwasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi), kama zilivyoiezwa kwa muhtasari katika kitabu chenye kichwa cha habari "Maelezo ya Makisio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2003/2004, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Rais, Ikulu na Baraza la Mawaziri na Taasisi zake cha Juni, 2003" kutoka katika Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilijulishwa kuwa jukumu la Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zake ni kuhakikisha kuwa nchi inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, sheria, kanuni na taratibu

zilizowekwa. Aidha, majukumu ya Ofisi ni kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali kwa misingi ya Utawala Bora, uwajibikaji na utoaji huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilifahamishwa kuwa dira ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni kuboresha utumishi wa umma kuwa chombo chenyehutawala ambacho kitaiwezesha nchi yetu kuwa na uchumi unaokua, wenyekuleta matumaini na unaoweza kutokomeza umaskini katika karne hii. Hii inalenga kutufikisha kwenye ubora katika utoaji huduma, utii, bidii ya kazi, uadilifu, kuheshimu sheria, ubunifi, huduma kwa gharama nafuu na kuzingatia utendaji wenyemkakati na matokeo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya kawaida ya Idara hii ni kujenga mazingira mazuri kuwawezesha watumishi wa umma kufanya kazi zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma. Majukumu haya yana lengo la kuleta ufanisi na nidhamu kazini kwa madhumuni ya kudumisha Utawala Bora ndani na nje ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia lengo hilo, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepewa majukumu kadhaa ikiwa ni pamoa na kuandaa, kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na miongozo ya utumishi na utawala Serikalini na kuhakikisha kuwa inazingatia usawa wa jinsia, kusimamia maadili ya utendaji kazi katika utumishi wa umma ili kuleta ufanisi, uadilifu na heshima kazini na kusimamia ajira katika vyombo vya umma ili zifanyike kwa misingi ya ushindani na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2002/2003, hakukuwa na makusanyoyote ya mapato kwa Ikulu na taasisi zake kwa vile hazina vyanzo vya mapato. Kwa upande wa matumizi ya kawaida kwa mwaka 2002/2003, mafungu 20 na 30 yaliidhinishiwa jumla ya Sh.38,478,735,800/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilijulishwa kuwa katika mwaka uliopita, Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zake zilitkeleza kazi zifuatazo: Kuongoza na kuratibu uendeshaji bora wa Serikali, kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Rais na Baraza la Mawaziri, kukamilisha mkakati wa Taifa dhidi ya rushwa na kuandaa mikakati ya kisekta na ratiba za utekelezaji katika kipindi cha miaka mitano, kuimarisha Taasisi ya Kuzuia Rushwa kwa kuipatia wafanyakazi wapya 159, kuwezesha kufungua Ofisi za Wilaya 45, kufanikisha awamu ya kwanza ya ukarabati wa Ikulu na kutekeleza miradi ya huduma za jamii na miradi ya ujenzi katika baadhi ya Wilaya Tanzania Bara na Visiwani chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka huu wa fedha ni kuendelea kuratibu shughuli za Tume, Sekretarieti na Taasisi mbalimbali za Serikali na kuimarisha Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, kupokea na kuchunguza tuhuma za rushwa na kufuatilia kesi zinazotokana na tuhuma hizo zilizofikisha Mahakamani, kusimamia na kutekeleza mikakati dhidi ya rushwa, kuendelea kuongoza, kufuatilia, kutathmini na kuratibu uendeshaji bora wa Serikali, kuendelea kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Rais na Baraza la Mawaziri, kuendelea na kufanya ukarabati majengo ya Ikulu yaliyobaki na kuendelea kutekeleza miradi ya *TASAF*. Ili kutekeleza kazi hii jumla ya Sh.48,184,515,100/= zinatarajiwakutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilifahamishwa kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2002/2003, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma haikuwa na mapato yoyote kwa vile haina vyanzo vya mapato. Aidha, kwa upande wa matumizi iliidhinishiwa Sh.275,052,300/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka uliopita Sekretarieti ya Maadili ya Uongozi ilitekeleza kazi zifuatazo: Kuhakikisha kuwa tabia na mwenendo wa viongozi wa umma unaridhisha ili kuleta imani ya wananchi kwa Serikali yao hivyo kuimarisha Utawala Bora nchini, kupokea na kuhakiki tamko la mali na madeni ya viongozi 5,510 wa umma, kuchunguza malalamiko 65 ya wananchi dhidi ya viongozi wanaotuhumiwa kukiuka maadili ya uongozi wa umma, kuendesha mafunzo na semina kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili ya uongozi, semina zilifanyika katika Halmashauri za Ngara, Biharamulo, Kilosa, Mwanga, Misungwi, Kwimba, Kinondoni na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha, Kamati yangu ilijulishwa kuwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imejiwekea malengo yenye nia ya kuimarisha utendaji kazi, kupokea, kuchambua na kuchunguza malalamiko ya wananchi dhidi ya viongozi wanaotuhumiwa kukiuka maadili na kutoa elimu kwa umma na utekelezaji wa mradi wa kukuza maadili (*Ethics Promotion Project*) na kutoa mafunzo ya kitaalam kwa watumishi. Ili kutekeleza hayo Sekretarieti inahitaji Sh.501,374,900/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilielezwa kuwa Tume ya Utumishi Serikalini imeendelea kuwepo katika kipindi cha mpito ambapo taratibu za kuanzisha rasmi Tume ya Utumishi wa Umma zinakamilishwa. Kwa mwaka wa fedha uliopita, Tume hii iliidhinishiwa jumla ya Sh.577,155,500 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Mei, 2003, Tume ya Utumishi Serikalini ilishughulikia mapendekezo ya ajira, uthibitisho kazini, upandishwaji vyeo watumishi kadhaa wa umma, kusikiliza kesi za rufaa za watumishi na kuendesha mitihani kwa watumishi wa umma.

Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Tume ya Utumishi Serikalini imepanga kufanya kazi zifuatazo: Kuendesha usaili kwa waombaji wa kazi, kushughulikia ajira, kuthibitisha kazini watumishi, malipo ya uzeeni, kushughulikia kesi za rufaa za watumishi na kadhalika. Ili kutekeleza hayo, Tume ya Utumishi Serikali inaomba Sh.642,329,800/=

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati yangu ilijulishwa kuwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilikusanya jumla ya Sh.2,224,195.05 kutokana na kodi ya nyumba za Serikali. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa Sh.4,547,712,200/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi Mei, 2003 kiasi cha Sh.3,270,360,597/= kilitolewa na kutumika. Kwa upande wa matumizi ya fedha za maendeleo, Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa Sh.11,337,494,500 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilielezwa kuwa mwaka uliopita Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilifanikisha mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na kusimamia Programu ya Uboreshaji Utumishi wa Umma, kuanzisha rasmi Tume ya Utumishi wa Umma, kusimamia ajira Serikalini, kuandaa Sera ya Mafunzo na kuelimisha umma kuhusu maadili, sheria, kanuni na taratibu za utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilijulishwa kuwa kwa mwaka huu wa fedha, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itatekeleza, kukamilisha maandalizi ya kuanzisha Tume ya Utumishi wa Umma, kubadili Idara au taasisi nane za Serikali kuwa Wakala wa Serikali, kuendelea kuzisaidia Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Mikoa, kuingia mpango wa ushirikishwaji sekta binafsi katika kutoa huduma ambazo sio lazima kutolewa na Serikali, kuendelea kukijengea uwezo Chuo cha Utumishi wa Umma, kujenga kituo cha kuhifadhi kumbukumbu na kuwasilisha Bungeni Miswada mitatu ya sheria ikiwemo ya kuhifadhi kumbukumbu za Viongozi Waasisi wa Muungano, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Aman Karume. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha, Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliombwa Kamati yangu iidhinishe Sh.4,925,170,800/= na Sh.11,337,494,100/= kwa ajili ya programu ya kuboresha utendaji kazi katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha Kamati yangu iliombwa iidhinishe jumla ya Sh.98,772,884,700/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kwa ajili ya shughuli za maendeleo kwa Ofisi ya Rais na Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka uliopita, Kamati yangu ilitoa ushauri katika maeneo kadhaa ya Ofisi ya Rais na Taasisi zake na Menejimenti ya Utumishi wa Umma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ofisi ya Rais na Taasisi zake, ushauri wa Kamati yangu ulielekezwa katika ukarabati wa majengo ya Ikulu - Dar es Salaam, Taasisi ya Kuzuia Rushwa, *TASAF*, Usalama wa Taifa na maagizo ya Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa majengo ya Ikulu Dar es Salaam, ushauri wetu kuhusu ukarabati huu umezingatiwa na katika Bajeti ya 2002/2003, Bunge liliidhinisha Sh.2,860,000,000 kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Kamati yangu ilishauri pamoja na mambo mengine kuwa Serikali itoe nyenzo na fedha za kutosha kuimarisha na kuwashirikisha raia wenye uzoefu katika fani mbalimbali. Ushauri huu kwa kiasi kikubwa umezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TASAF*, Kamati yangu ilishauri kuwa Serikali iwe wazi kuhusu vigezo vinavyotumika kwa Wilaya kupata fedha za Mfuko wa *TASAF* na kuhakikisha kuwa Mfuko huu unasambazwa katika maeneo yote nchini. Ushauri huu umefanyiwa kazi kwa kutoa maelezo ya kina kuhusu hoja hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa mwaka 2002/2003, Kamati yangu ilitoa ushauri katika maeneo mbalimbali yafuatayo: Kuhusu ajira za Walimu katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo, Kamati yangu ilishauri kuwa Serikali iendelee kufanya jitihada za kutosha kuongeza ajira za Walimu kwa kuwa na ushirikiano wa karibu na Wizara nyingine. Ushauri huu ulizingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu udhibiti wa ajira, Kamati yangu ilishauri kuwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ijjitahidi kuwa na takwimu za watumishi wote nchini. Serikali ilitoa taarifa kuwa taarifa muhimu za watumishi wa Serikali zimeingizwa kwenye *computer* na kwamba katika kipindi cha 2001/2002 na mfumo huu uliimariswa na maandalizi yanafanya ili uweze kusambazwa kwenye Wizara tano kwa majaribio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwapandisha vyeo watumishi, Kamati yangu ilishauri kuwa zoezi la upandishaji vyeo liangali kwa makini ili vyeo wapate wale wanaostahili. Aidha, Serikali ifanye utafiti wa kina kujua sababu zinazowafanya watumishi wafanye kazi chini ya kiwango kilichowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pensheni kwa wastaa fu, Kamati yangu iliarifiwa kuwa suala hili ni mionganoni mwa mambo yanayoangaliwa upya katika kipindi hiki cha miaka mitano ya mpito. Aidha, udhaifu katika utaratibu wa sasa wa kulipa pensheni unashughulikiwa kwa lengo la kuondoa mapungufu ili kuboresha mfumo mzima wa pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza muhtasari wa taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora wa mwaka 2002/2003, sasa napenda kueleza maoni na ushauri wa Kamati baada ya kuchambua makadirio ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi na ushauri wetu kwa sehemu kubwa unarejea ushauri ambaao tuliutoa mwaka wa fedha uliopita kwa nia ya kurekebisha mapungufu yaliyoonekana katika utekelezaji wake. Aidha, pamoja na ushauri huo, yapo maeneo ambayo Kamati yangu ilitaka ufanuzi zaidi na kutolewa maelezo na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inashauri kuwa kutokana na kuongezeka kwa wimbi la vitendo vya ujambazi wa kutumia silaha nchini, vyombo vyote vya ulinzi na usalama vishirikiane ili kuhakikisha kuwa usalama wa raia na mali zao unaimarishwa kote nchini. (*Makofii*)

Awali ya yote, napenda kupongeza utendaji wa kazi za Mfuko huu wa *TASAF* kwani kwa kiwango kikubwa Mfuko huu umeweza kutumia vema nguvu za wananchi na kuwashirikisha katika miradi ya maendeleo hivyo kuifanya miradi hiyo iwe ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, Kamati yangu inashauri kwamba, ili miradi hiyo iweze kutekelezwa kikamilifu, uongozi wa Mfuko ni vema uzingatia hali ya miundombinu katika maeneo ambayo miradi inatekelezwa. Aidha, shughuli za *TASAF* zifkishwe katika Mikoa mingi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Utawala Bora, Kamati yangu inashauri kuwa litengwe fungu maalum kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za msingi za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imebaini kuwa idadi ya mashauri ya rushwa yanayofungwa kwa madai ya kukosekana ushaidi ni mengi. Hivyo, tunapendekeza mikakati mipyia ianzishwe ili kukabiliana na hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inashauri kuwa Serikali iendelee kuboresha mishahara ya Walimu, kuwapatia marupurupu muhimu ili kuwajengea mazingira ya kuendelea kubaki katika ajira Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inashauri kuwa utaratibu uliotumika katika kuajiri Walimu utumike pia kwa watalaan wa Idara ya Afya ili kuziba mapengo yaliyopo katika Idara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inashauri kuwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma isimamie ajira zinazotolewa kwenye Halmashauri za Wilaya katika jithada za kudhibiti ajira za upendeleo ili kuendelea kujenga Utaifa. Aidha, Kamati inapendekeza ufanyike utafiti wa kina ili kubaini njia za kukabili tatizo la watumishi wa umma kufanya kazi saa chache kwa siku hali ambayo inapunguza tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muhtasari, haya ndio maoni na ushauri wa Kamati yangu, ambao naamini kuwa Serikali itayafanya kazi na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wake wakati utakapowadia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa maeneo mengine ambayo sikuyagusa, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu watajitalidi kuchangia watakapopata nafasi ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii muhimu, aidha, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Mary Nagu na Mheshimiwa Wilson Masilingi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa maelezo yao ya kina na ufasaha mkubwa mbele ya Kamati na kutekeleza vyema ushauri wetu tuliusiwa mwaka wa fedha uliopita bila kuwasahau wataalam wote walioshirikiana nasi katika kikao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, kwa mara nyingine nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao mizuri wakati wote tulipochambua makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi hii ya Rais kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila kama sitamshukuru Katibu wa Bunge na wasaidizi wake hususan Makatibu wa Kamati hii Ndugu Nenelwa Mwihambi na Ernest Zulu, kwa kuihudumia vema Kamati hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. GRACE S. KIWELU - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Rais (Utumishi) kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(b)(c) toleo la 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kuwapongeza sana Wabunge wote wapya kwa kushinda katika Majimbo yao. Nawapa pongezi maalum Wabunge wote wapya kutoka CUF kwa namna walivyoshinda kwa kishindo cha ajabu kule Pemba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika Kambi ya Serikali inayosubiri, kwa kuona ninafaa kuwa msemaji wao katika Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Jimbo la Micheweni, ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), kwa ushiriki wake mkubwa katika uandaaji wa hotuba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wataalam wa mambo ya uendeshaji wa Serikali wamewahi kudai kwamba, Utumishi wa Umma ni nguzo ya nne ya dola, yaani ukiondoa Bunge, Mahakama na mkuu wa kiutendaji wa dola, yaani *the Executive*. Shughuli za kila siku za Serikali haziendi bila warasimu wa Serikali. Watumishi wa umma ndiyo watekelezaji namba moja wa sera zote za kiserikali (*Public Policies*). Ni wataalamu hao hao wa Serikali ambao bila ya kuonekana sana, huhusika sana na uandaaji wa sera za Kiserikali ambazo baadaye hutolewa na wanasiasa kama sheria za Bunge au maelekezo ya kisera au hata amri (*decrees*) na miongozo mbalimbali ya Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hasahasa Serikali kama chombo cha utawala ni watumishi wa umma. Mwendelezo wa kutoka Serikali ya Chama fulani kwenda Serikali ya Chama kingine kabisa, hufanywa na kusimamiwa na watumishi wa umma. Katika mazingira sahihi ya demokrasia iliyokaa kiumakini, watumishi wa umma wenye utaalam toshelevu huwa hawatakiwi kuwa na upande wa kuuegemea kisiasa na hutakiwa kufanya kazi zao bila ya kuhitaji kuonekana wala kutambulika ili kutoa nafasi kwa wanasiasa wa jukwaani kuonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejitahidi sana katika miaka ya karibuni kuifanyia kazi dhana maarufu ya Utawala Bora na kuanzishwa kwa taasisi kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Maadili ya Viongozi, Taasisi ya Kuzuia Rushwa, ikiwa ni pamoja na kuwa na Waziri wa Nchi anayeshughulikia Utawala Bora. Kwa kweli mtandao wa kitaasisi kuhusu Utawala Bora si haba katika Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa taasisi nyingi zinazoshughulikia suala zima la Utawala Bora, bado Tanzania iko mbali sana tu katika kuwa na jamii inayofanana na Utawala Bora na hasa katika nyanya au maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala Bora ni pamoja na utungaji bora wa sera za Kiserikali, pamoja na utekelezaji wa kiumakini wa sera hizo. Sera mbovu zina maana ya matumizi mabovu ya fedha za walipa kodi. Kitendo cha Serikali kuendelea kukumbatia sera ya kuhamishia Makao Makuu yake katika Mji wa Dodoma, huku ikieleweka wazi kwamba, uamuzi huo wa kisera hautekelezeki, ni ufujaji wa wazi wa fedha za umma. Kama ambavyo Serikali imeshauriwa na Waheshimiwa Wabunge, ikiwa ni pamoja na wale wa Chama Tawala, ni wakati muafaka sasa wa kukiria kwamba sera hiyo imeshindwa. Kukiria kushindwa kwa sera kwa lengo la kufanya kitu mbadala cha kuwafaa wananchi ni dalili ya kukomaa kisiasa na ni alama kubwa ya Utawala Bora. Serikali inashauriwa ikubali yaishe kwa kuachana kabisa na uamuzi usiotekelzeza wa kuhamishia Makao yake Makuu Mjini Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inaeleweka pia kwamba, Utawala Bora ni pamoja na kusamehe na kusahau na kupalilia maelewano yanayoruhusu kutofautiana na hata kupingana bila ya kupigana wala kutoana macho. Kuna kila sababu ya kuwa na ule utaratibu wa Tume ya Ukweli na Upatanishi kama ilivyojitekeza kule Afrika ya Kusini na kuna Tume ya aina hiyo katika nchi ya Ghana. Chini ya utawala wa Chama kimoja, wenzetu kadhaa walikumbana na kucha za sheria ya mtu kutupwa kizuizini na wapo wengi walioathirika sana na hilo. Maamuzi kama Operesheni Vijiji na ile Operesheni ya kupambana na wahuju muwa uchumi na walangazi katika miaka ya themanini, yaliwaumiza watu wengi na wapo wengi wanaoendelea kulia kimyakimya na kuugiza majeraha kimyakimya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lengo zuri tu la kusamehe na kusahau, wote walioumizwa na vitendo vya dola visivyo halali wawekwe wazi na waombwe radhi na ikiwezekana wafidiwe. Wengi wao walitupwa ndani kwa kupinga aidha siasa ya Chama kimoja au itikadi ya ujamaa. Watu hawa sasa watambulike rasmi kama watu waliopigania kuwepo kwa demokrasia ya kweli katika Taifa la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, historia rasmi ya Taifa letu isiwafunike kimakusudi tu watu kama Kassim Hanga, Kassanga Tumbo, Joseph Kasella-Bantu, Abdulrahman Mohamed Babu, Oscar Kambona, Othman Sharif Mussa na wengine wengi tu ikiwa ni pamoja na wale waliouawa kule Pemba Januari 26 na 27 mwaka 2001. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima historia rasmi ya Tanzania iandikwe upya kwa lengo la kuwapa nafasi sahihi wale wote wanaostahili nafasi hizo, walio hai na wote waliotutangulia mbele ya haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, iundwe Tume isiyo na utata itakayoanda orodha ya watu wanaotakiwa kufufuliwa kihistoria kwa lengo la kuenziwa rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba pia katika kikao hiki cha Bunge hili la Bajeti, Serikali itoe tamko rasmi kuhusu utekelezaji wa Ripoti ya Hashim Mbita, kuhusu matukio ya Januari 26 na 27, 2001, ikiwa ni pamoja na suala la fidia kwa walioathirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wetu ni lazima wajifunze uungwana na wajue wazi kwamba, vyeo vyao wamekopeshwa na wananchi. Viongozi wanaowadharau wananchi kwa kauli zao, muonekano wao na matendo yao, kwa kweli wanamwaibisha Mheshimiwa Rais wetu. Uongozi wa juu si kukurupuka na kuchemka, ni kutuliza kichwa na kufanya maamuzi kwa busara na kutulia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Kuzuia Rushwa imekuwa ikijitahidi kuongoza mapambano dhidi ya rushwa na hasa hasa kwa mkakati wa kuelimisha umma kuhusu sura mbalimbali za rushwa na namna ya kuzizuia na kupambana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na wenzetu wa *PCB* kuwa na Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji kwa Tanzania tangu mwaka 1999, bado hali ya rushwa inazidi kuwa mbaya kila kukicha. Wananchi wengi wanakerwa na hata kusononeshw na namna *PCB* inavyowavalia njuga Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na viongozi wa Kata na labda Polisi wadogowadogo na Walimu Wakuu wa shule za msingi, kama vile katika Tanzania hakuna rushwa kubwa kubwa. Tume ya Warioba, ilichanganua na kuchimbua vilivyo rushwa za wakubwa na wanazuoni mahiri katika uwanja wa rushwa kama Profesa Fidelis P. Mtatifikolo wa Idara ya Uchumi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wamelichimbua na kulichambua mno tatizo la rushwa katika Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanajiuliza, hivi ni kwamba *PCB* haina uwezo wa kuwajua na kuwashughulikia wala rushwa walio katika ngazi za juu Serikalini na hata katika sekta binafsi au kigugumizi cha kuwashughulikia ni cha makusudi na kina lengo la kuwalinda watu fulani?

Ni kwa nini *PCB* inanyong'onyea na kujikunyata kila ikitajiwa habari ya rushwa kubwa kubwa na nzito nzito? Wapo wenye wasiwasi kwamba *PCB* imetekwa nyara na wanaohofia kufuatiliwa kwa tuhuma nzito za rushwa. Yaelekea *PCB* imewekwa mfukoni na wanaochezeshwa mchezo wa siasa Tanzania na huenda ndiyo maana haifurukuti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri *PCB* nzima ijipange na kupangwa upya na isikilize maoni na hoja mbalimbali za wadau mbalimbali, bila kujali taasisi wanazotoka, itikadi zao na wala historia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na wasomi kama Profesa Joseph R. A. Ayee, wa Chuo Kikuu cha Ghana, kudai kwamba dawa ya rushwa ni pamoja na mageuzi ya kiutamaduni na kimazoea na kuwepo kwa mfumo wa Kitaifa wa kimaadili, bado Tanzania inaweza ikafaidi sana tu kwa kutumia *Open Book Management* au mtindo wa mambo hadharani katika uendeshaji wa mambo ya Serikali, ambapo chochote kisichotishia usalama wa Taifa kiulinzi na kiuchumi, kitachapishwa wazi na kubandikwa kibayana kabisa au kutangazwa magazetini na redioni waziwazi. Jambo hili likisimamiwa vizuri huondoa usiri usio na msingi na kwa hali hiyo kuziba vizuri kabisa mianya ya rushwa. Uwazi na uangavu wa kikweli kweli katika shughuli za Serikali ni adui mkubwa wa rushwa na ni kiboko kikali dhidi ya michezo yote iliyo michafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Usalama wa Taifa ni jukumu muhimu la kila mmoja wetu. Nchi karibu zote duniani huunda taasisi mbalimbali za kuongoza, kuratibu na kusimamia usalama wa Taifa na hasa maslahi muhimu ya kiulinzi na kiuchumi ya Taifa lolote lile. Dunia inazo taasisi kadhaa za kikachero ambazo mara nyingi hufanya kazi zake chini kwa chini na wakati fulani hufanya hata hujuma, kwa lengo la kukuza na kulinda maslahi ya kisiasa, kiuchumi, kiteknolojia na kiulinzi ya Taifa husika. Taasisi kama *CIA*

na *FBI* katika Marekani, *MI 5* na *MI 6* katika Uingereza pamoja na watu wa *Scotland Yard*, pia *The Institute of Mossad* kule Israel na kadhalika ni baadhi tu ya taasisi nyingi za aina hiyo duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kitabu kiichwacho *CIVICS - A Tanzanian Reader*, kilichotolewa na Mradi wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia Tanzania (*REDET*), uliopo katika Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambacho kilichapishwa mwaka 2001, katika sura ya nne ambayo imeandikwa na Augustino Ramadhani, kati ya ukurasa wa 85 hadi 91, kinaitambulisha na kuelezea taasisi inayofahamika kama *The Tanzania Intelligence and Security Service*, ambayo ipo kwa mujibu wa Sheria Na.15 ya mwaka 1996 ya Bunge la Tanzania. Taasisi hii inaongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Idara ya Usalama wa Taifa ni Idara ya kawaida tu ya Serikali, yenye majukumu maalum ya Kiserikali na wanaofanyia kazi ni watumishi wa Serikali na inatakiwa kufanya kazi za kuwanufaisha Watanzania, ni wakati muafaka sasa kwa taasisi hiyo kujifananisha na mazingira mapya ya kisiasa na kiuchumi katika Tanzania, angalau kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kuondokana na mtazamo wa zama za vita baridi duniani ambapo usiri uliokithiri na ukimya wa hali ya juu uliotawaliwa na vishindo vya kimyamya ilikuwa ndiyo sera. (*Makofî*)

(b) Kuwa mstari wa mbele katika kuimarisha demokrasia ya Vyama Vingi na kuwadhibiti wote wanaotamani kuirudisha nchi kwenye udikteta wa Chama kimoja. (*Makofî*)

(c) Kuwadhibiti vilivyo wote wanaocheza rafu na hasa kile kinachoitwa michezo michafu katika uchumi wa soko huria, ambalo halitakiwi kuwa soko holela. Ni jukumu la taasisi hii kuwajua na kuwashughulikia wote wanaoichafua na kuihujumu sera ya ubinafsishaji na uwekezaji, ambayo ikiondolewa michezo michafu ina manufaa makubwa kwa Taifa. (*Makofî*)

(d) Kupambana vikali na wote wanaodaiwa kuliibia Taifa utajiri wake kwa kutorosha raslimali za Taifa na hasa katika sekta ya madini. (*Makofî*)

(e) Kuhakikisha wananchi wanaelewa taasisi hii na majukumu yake. Taasisi hii imejificha mno kiasi kwamba hata Mkurugenzi wake Mkuu ni wananchi wachache mno wanaomjua hata kwa jina tu kama si sura. Mabosi wa *CIA* na *FBI* wanafahamika kwa sura na majina, hivi ni kwa nini Watanzania wasimjue bosi wa *TISS*, ambaye ni mtumishi wao mkuu katika eneo la ukachero bila ya kuhitaji kuwajua watendaji wake na vijana wake? (*Makofî*)

(f) Taasisi hii ni lazima sasa ifanane na demokrasia na itoke huko ilikokuwa imejificha kwenye mielekeo ya taasisi za aina hiyo katika nchi za zamani za kikomunisti duniani. Hata kachero wa zamani wa Shirika la Kijasusi la Umoja wa Kisovieti, Bwana Vladimir Putin, sasa hivi anahubiri demokrasia badala ya mabavu ya Kikomunisti. Dunia bado hajasahau aibu iliyozikumba taasisi za kikachero kama *Securitate* katika Romania ya Kikomunisti, Stasi katika Ujerumania ya Mashariki ya Mkomunisti Honecker na juzi juzi tu taasisi ya Saddam Hussein iliyokuwa ikiitwa Mukhabarat. Taasisi hizo zote zilishindwa kudhibiti usalama wa Mataifa husika na yote yalianguka, kutokana na kutoungwa mkono na wananchi na hasa hasa kutokana na usiri wake, ubabe wake na kupinga demokrasia. *KGB* ya *Soviet Union* pia ilisambaratika baada ya kujiweka mbali mno na watu na kuendekeza utawala wa kimsonge na kirasimu badala ya demokrasia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dunia ya sasa kinachotamba ni taarifa na sote tunaamini kwamba uongozi ni kuwa *informed* na kufanya maamuzi sahihi katika wakati sahihi na mahali sahihi na siyo suala la umri wa mtu. Marehemu Deng Xiao Ping, ndiye muasisi wa mageuzi makubwa ya kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia katika Jamhuri ya Watu wa China, pamoja na kwamba alikuwa na umri mkubwa kabisa. Nelson Mandela pamoja na uzee wake bado ni *intellectual powerhouse* ya Afrika nzima. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwahitaji wazee wetu na busara zao, huwa upo ukomo wa kuwategemea. Mzee Nelson Mandela aliacha uongozi wa kisiasa kule Afrika ya Kusini kwa kuona mbali

na kutambua kwamba changamoto mpya pia huhitaji watu wapya na upo ukomo wa kuwakarabati na kuwakarafati watu. Yapo mambo ambayo ni lazima apatikane mtu mpya na wa kizazi kipyta ili kukabiliana na matatizo ya aina mpya. Si kila mara *recycling* ni jibu la matatizo. Si kila mara kupanga na kupangua safu za watu walewale na wa namna ile ile ndiyo ufumbuzi wa tatizo. Ili kumaliza matatizo na kutoahirisha matatizo, yapo mambo yanayohitaji watu wapya kabisa na wenye fikra mpya kabisa na siyo watu waliokarabatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii habari ya mvinyo wa zamani katika chupa mpya siyo lazima iwe ni yenye manufaa muda wote. Huwa upo msemo wa Waingereza kwamba, *you cannot teach an old dog new tricks*, kwa maana ya kwamba, mbwa mzee huwa hafundishwi mbinu mpya za kukamata sungura. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu linao Watanzania wengi tu amba siyo tu kwamba wametayarishwa vema kielimu na kitaaluma, lakini pia wamekwishaiva kiujuzi na kiuzoefu wa kazi na ni watu wa aina mpya wanaozimudu changamoto mpya za kidunia. Taifa liwaamini vijana wake kama Wamarekani walivyowaamini viongozi vijana kama Bill Clinton na huyu George Bush wa sasa na kama Waingereza walivyomwamini Tony Blair na Warusi walivyomwamini Vladimir Putin. Sote tunaona, kwa viongozi hao mchezo na kulala usingizi hakuna, ni kazi mtindo mmoja, mchana na usiku. Sote hapa Tanzania tunaona namna Mheshimiwa John Pombe Magufuli, anavyochapa kazi, si kutokana na usomi wake tu, ila pia ni pamoja na ujana wake na hata usasa wake, kwamba ni mtu mpya, mwenye fikra mpya na katika dunia yenye changamoto mpya. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 1991 Serikali imekuwa ikitekeleza awamu mbalimbali za Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma. Programu hiyo ilizinduliwa rasmi 1991 japokuwa utekelezaji wake ulianza 1993 na awamu yake ya kwanza ilikwisha mwezi Desemba, 1999. Kuanzia mwaka 2000 imeanza tena programu kubwa ya kuboresha utumishi wa umma (*PSRP*) itakayofikia kikomo mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo zuri kwamba, Serikali inao mpango mkubwa wa kuboresha utumishi wa umma, amba pia unahusisha uboreshaji wa Serikali za Mitaa na inatia moyo kuona kwamba wafadhili kadhaa wa Kimataifa wanaunga mkono mpango huu mkubwa. Lakini pamoja na uzuri wa mageuzi yote hayo katika utumishi wa umma, hasa tangu 1993 na pamoja na kuwepo kwa Sera ya Menejimenti na Utumishi wa Umma tangu Mei, 1998 ilipokubaliwa na Baraza la Mawaziri, bado kipato halisi kinachoingia kwenye mfuko na pochi ya mtumishi wa kawaida au ofisa wa kawaida katika utumishi wa umma, hakiti moyo wala kurandana na ahadi za kuboresha vipato halisi vya watumishi wa umma zilizomo katika sera na awamu mbalimbali katika Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, utumishi wa umma ni ajira yenye heshima na hadhi kubwa sana katika nchi nyingi duniani, ikiwa ni pamoja na nchi zinazoendelea na nyingine zilizo Afrika. Utumishi wa umma ni ajira ya kuonewa wivu na kupigwa mfano katika nchi ya Singapore katika Asia, pia ni ajira inayoonewa wivu katika Botswana na Swaziland na wakati fulani hata katika nchi jirani ya Rwanda. Si rahisi kumhonga Afisa Uhamaaji katika nchi kama Korea ya Kusini kwa sababu hana hata sababu ya kuiwazia au kuitamani hongo yako, lakini katika Tanzania hali ni tofauti sana. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Maadili ya Viongozi ni chombo muhimu katika kusimamia Utawala Bora na Demokrasia. Tume hii siyo tu inao wajibu wa kuorodhesha mali za viongozi, ila pia kujua vyanzo sahihi vya mali hizo. Inapendekezwa Tume ya Maadili ya Viongozi ifuatilie kikamilifu tabia na mienendo ya viongozi kwa lengo la kuiepushia Serikali aibu. Zipo tabia chafu ambazo kiongozi wa umma hatakiwi hata kuhisiwa kwamba anaweza kuhusiana nazo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume hii imsaidie Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhakikisha viongozi wote wa umma ni safi na imsaidie Rais kuwajua viongozi wote wanaokiuka maadili ya msingi ya uongozi, ndani na nje ya ofisi zao, ili wawajibishwe mara moja. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwaenzi viongozi wa Taifa waliotutangulia mbele ya haki na hata walio hai si jambo baya. Kama lipo wazo la kutunga sheria ya kuwaenzi viongozi wakuu, basi sheria

isitungwe ikiwa na wazo la fulani kwenye kichwa. Lengo liwe ni kuwa na sheria makini itakayowapa nafasi wote wanaotakiwa kuenziwa, baada ya kuelewana Kitaifa na kupata orodha ya hao wanaotakiwa kuenziwa, ikiwa ni pamoja na wale wote ambao historia rasmi imewagubika kwa makusudi ili wasionekane. Sheria hiyo isitungwe kabla ya mjadala mzuri na wa kina mionganoni mwa wadau kufanyika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, litengwe eneo maalum la kuwazika viongozi wote wa Kitaifa wanaostahili kwa lengo la kuleta urasmi zaidi wa mambo ya Kitaifa na pia kuweka ukumbusho mzuri zaidi kwa vizazi vijavyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi zilizoanzishwa na watu wenye historia iliyotukuka na waliofanya mambo yanayong'ara Kitaifa na Kimataifa katika wakati wa uongozi wao na wakati wa uhai wao, kwa mfano, Taasisi ya Mwalimu Nyerere, zitafutiwe utaratibu wa kisheria zaidi na wa Kiserikali zaidi wa kuziendeleza na kuziunga mkono. Jambo hili litaepusha uwezekano wa taasisi hizo kutumiwa ovyo na kwa maslahi binafsi na hasa kwa kutumia majina makubwa ya waliozianzisha kama *trade mark*.

Mheshimiwa Naibu Spika, demokrasia ya kisasa ni uwezeshejji, *empowerment* na *enablement* kwa staili ya kutokea chini kuja juu. Serikali za Mitaa ni chombo muhimu cha kuwapa wananchi uwezo wa kuamua mambo yao na kwa hali hiyo kupanua wigo wa demokrasia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kufutwa kwa kifungu cha 6 (6) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kupitia Sheria Na.25 ya mwezi Novemba 2002, kunahujumu demokrasia kwa kuzinyang'anya Halmashauri mamlaka ya kuajiri na kuwamiliki watumishi wake. Suala hili pia linakiuka Katiba ya nchi Ibara ya 6. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iache haraka undumilakuwili (*Double Standards*), mara inahimiza demokrasia kwa maana ya kupeleka madaraka kwa wananchi na muda huo huo inang'ang'anisa sera za kuitawala nchi kimsonge, jambo linalopunguza wigo wa demokrasia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni nyakati za kupeleka madaraka ya kikweli kweli kwa wananchi na siyo yale ya kiinimacho, kama ilivyokuwa wakati wa zoezi la madaraka Mikoani mwaka 1972. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha Utawala Bora katika nchi yetu, inashauriwa viongozi wetu hata walio katika ngazi ya Taifa, wajenge mila na tabia ya kuwajibika pale inapobidi na palipo wazi kabisa, ili kuotesha mizizi ya Utawala Bora na kustawisha demokrasia katika Tanzania. Uzalendo ni pamoja na kukubali ukweli kwa maslahi ya Taifa, hata kama ukweli huo unauma. Tuipende Tanzania yetu kwa kukubali haki na demokrasia ichukue mkondo wake hata kama mkate wetu wa kila siku utapotea. Daima iwe Tanzania kwanza na baadaye kabisa ndiyo sisi na ubinafsi wetu. Maslahi ya Taifa daima yawe imbele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Waziri wetu Mkuu, tunayempenda na kumheshimu sana, atakubali kiungwana kabisa na kiuzalendo kabisa, kukipa nafasi chombo cha Serikali kiitwacho *PCB* au *TAKURU*, kumchunguza yeze kwa uhuru unaokubalika kitaalamu kwa lengo la kuupata ukweli kuhusu mambo anayohisiwa na kudaiwa kuyafanya. Kwa namna ninavyomjua, nina hakika anao ushujaa na anayo busara ya kufanya uamuzi mzito wa kizalendo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nafasi nyeti kama hii ya Waziri Mkuu, kule kuhisiwa tu tayari kunakuwa ni doa katika kioo chetu cha kujitazamia. Baba wa Taifa Marehemu Julius K. Nyerere, aliwahi kusema kwamba, hata ule mnong'ono tu kuhusiana na kiongozi kudaiwa kucheza rafu, unatossa kuwa ni sababu ya kiongozi muungwana na muadilifu kuwajibika.

Taarifa za haraka haraka za wenzetu wa *PCB* katika vyombo vya habari, kwamba hawamtuhumu Waziri wetu Mkuu kwa lolote lile, ila wapo katika uchunguzi wa awali kuhusu madai yaliyotolewa dhidi yake, hazifuti umuhimu na sababu za Waziri wetu Mkuu, kuchukua hatua madhubuti za kuwajibika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi maskini sana ambayo deni lake la nje la jumla ni dola za Kimarekani bilioni 7.648 hadi kufikia Aprili, 2003, kwa mujibu wa *BOT*. Kwa mujibu wa ripoti ya *UNDP* kuhusu Maendeleo ya Watu kwa mwaka 2003, Tanzania ina kiwango duni cha maendeleo ya watu na imepewa thamani ya 0.400 na inashika nafasi ya 160 katika nchi 175. Nchi zenyenye maendeleo duni zinaanza namba 142 inayoshikiliwa na Cameroon na inayoshika mkia katika namba 175 ni Sierra Leone.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inayo nafasi kubwa ya kupiga hatua kimaendeleo kama itahakikisha mfumo wake wa utumishi wa umma umepangwa kiumakini. Dawa ni kuingiza kipendaroho ndani ya watumishi wa umma ili wajitume toka ndani kabisa ya nyoyo zao kulitumikia Taifa lao. Kipendaroho hakizuki tu, ni lazima kijengwe kwa maamuzi ya kimakusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipato vya watumishi wa umma vikiboreshwu vizuri kabisa, vina uwezo wa kuwabdalilisha Watanzania hawa hawa wafanyao kazi Serikalini kwa shingo upande, kuwa walevi wa kazi kuliko hata Wajapani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Waziri atakapokuwa anatoa majibu, aeleze bayana endapo amekubaliana na wito wa Wabunge, kwa kuruhusu *Vote* ya Uhamiaji itolewe kuanzia sasa. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofisi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa hapo tumemaliza wale Wachangiaji wetu Wakuu. Ninao wachangiaji wengi kidogo amba o mmoja apate nafasi. Utaratibu wetu ni ule ule, wale amba o hawajachangia kabisa watapata nafasi ya awali na waliochangia mara moja hivyo hivyo tutakwenda mpaka wale amba o wamechangia mara nne kama itapatikana nafasi basi nitawapa. Sasa kwa kuanzia namwita Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, ambaye alikuwa hajachangia kabisa. Halafu atafuatia Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya na Mheshimiwa Njelu Kasaka, kwa orodha kama ilivyo.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza katika kuchangia hoja hii ambayo imewasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote katika Ofisi ya Rais, Utumishi, pamoja na Utawala Bora. Kwa kweli Bajeti yao ni nzuri ikizingatiwa kama walivyojieleza katika Bajeti yao. Pamoja na hayo nazidi tena kuwapongeza hasa Makatibu Wakuu kuanzia Katibu Mkuu Kiongozi Ikulu na Ndugu Rugumyamheto, amba o wameongoza katika uandaaji wa taarifa hii nzuri. Kwa kweli nawapongeza sana. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nichangie machache katika hotuba hii, kwa kuwa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala, Sheria na Mambo ya Katiba, nimezungumza mengi katika Kamati hiyo lakini napenda nichangie mambo mawili muhimu ambayo ni makubwa. Kwanza, ningependa nichangie suala la utumishi ambalo tumekuwa nalo kwa muda mrefu likiwa na sera na mikakati ya namna ya kuweka sawa watumishi katika nchi yetu. Tulikuwa na mpango wa kupunguza watumishi Serikalini amba o kwa kweli watumishi wengi wamepunguzwa lakini lengo la kupunguza hawa watumishi wabaki wachache lilikuwa ni kuwapa maslahi mazuri na ufansi mzuri wa utumishi Serikalini uwe umezingatiwa. Kwa zoezi hili muhimu mimi kwa maoni yangu limezua matatizo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, tatizo lilikuwa ni wazi kwamba, hawa watumishi amba o wamepunguzwa katika utumishi wao wamekuwa ni wengi na amba o wamegharamiwa na Serikali katika masomo yao na katika utumishi wao. Sasa hivi wapo nje ya utumishi na wengi wao ni vijana. Kwa hiyo, tumeunda kundi kubwa la watumishi amba o hawana ajira, kitu ambacho kwa kweli nacho ni tatizo katika nchi yetu. Ukizingatia suala zima la upunguza jati watumishi tukazua tena matatizo mengine ya kuwa na upungufu wa watumishi katika Wizara ya mbalimbali. Kwa mfano, sasa hivi tuna upungufu wa wafanyakazi katika Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Afya, Wizara ya Ushirika na Masoko na Wizara nyingine. Kwa hiyo, badala ya kuweka utaratibu wa Utumishi Serikalini vizuri, sasa tumezua matatizo mengine amba o hayakuwepo wakati ule wa kwanza. Hivi sasa tunasema Wizara ya Kilimo na Chakula ndiyo uti

wa mgongo wa Uchumi wa Taifa letu, lakini sasa Wizara hiyo haina watumishi. Watumishi wamekuwa wachache mno na ajira zimekuwa adimu. Kuajiri tena ili tuzibe lile pengo inakuwa ni tatizo moja kwa moja la Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda tena katika Wizara ya Afya nayo vilevile kuna upungufu mkubwa tu wa wafanyakazi, mpaka sasa hivi tunaomba na tunadai kwamba tupate Madaktari na tupate watumishi wengine walio chini ya Madaktari ili waweze kuhudumia afya zetu lakini ajira hiyo imekuwa ya kusuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naiomba Serikali kwa kuwa tumefanya zoezi hili kwa umakini kwa lengo la kuboresha utumishi Serikalini, basi Serikali ione umuhimu wa kuweza kuziba mianya ya watumishi au pengo la watumishi katika Wizara mbalimbali ambazo zina upungufu wa watumishi katika utumishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali naiomba kwa sababu labda pengine hatukizingatia uzito wakati tunafanya upunguzaji wa watumishi. Kwa hiyo, ni vyema sasa hivi tukaangalia ile mianya ambayo imeachwa wazi na wale watumishi waliopunguzwa Serikalini ili kuweza kuziba hilo pengo na utumishi wao uweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa njielekeze ni katika suala nzima la rushwa nchini. Suala la rushwa limekuwa tatizo sugu na limeota mizizi kiasi kwamba, namna ya kuliondoa tatizo hili itakuchua muda mrefu. Kwa sababu suala la rushwa kuna mambo mengine, mimi nitapenda niseme machache tu, lakini kuna masuala kama manne ambayo mimi nyaona. Kwanza, wananchi wamekuwa na mazoea kwamba asipotoa chochote haridhiki kama amepewa huduma na mtumishi yule anayehusika. Inaonekana lazima atoe chochote ili aweze kuridhika kwamba, nimemridhisha yule ambaye amenipa huduma na yule mhudumiaji vilevile anataka mpaka apate chochote ili naye aridhike kwamba kweli huyu mtu nimemhudumia vizuri. Kwa hiyo, suala hili limezama kabisa na limekuwa tatizo sugu, namna ya kuliondoa litatuchukua muda mrefu sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa tatizo hili imeonekana Serikali haikuzingatia uzito wa tatizo hili la rushwa, nini ambacho kimesababisha tumeanza na matatizo haya ya rushwa. Inawezekana Tume ambayo ilikuwa imeandaliwa ya Jaji Warioba, ilibaini maeneo fulani fulani na hayo maeneo hawakuzingatia kwamba nini kilichosababisha. Mimi naona ni upande wa maslahi ya watumishi kuwa chini mno kiasi kwamba, wanashindwa namna ya kuishi maisha yao na wanaona kwamba afadhali na bora zaidi waombe chochote kile ambacho kinapatikana kwa mtu ambaye wanamhudumia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo suala hili Serikali ililifanya bila kuangalia na kulichunguza zaidi. Kuna rushwa ya kawaida ambayo tunaita *Classical Corruption* ni ya kawaida tu, salaam, mimi naomba hiki au unampa mtu zawadi na amezoea kupewa zawadi. Pengine ni Daktari lakini anataka apewe zawadi, zawadi hiyo imageuka inakuwa kama rushwa, usipotoa chochote kama zawadi basi inaonekana wewe hustahili kuhudumiwa na yule mtu au na huyo mtumishi. Kwa hiyo, *Classical Corruption* imezagaa kama jambo tu la kawaida na usipotoa chochote kwa kweli mtu anayekuhudumia haridhiki kama amekuhudumia na wewe unayehudumiwa unaonekana kana kwamba pengine mimi sikumfurahisha yule aliyekuwa ananihadumia. Kwa hiyo, suala hili limezagaa sana, tunaita hiyo ni *Classical Corruption*, jambo tu la kawaida au kama salaam au kama ni chakula cha Daktari hilo ni jambo la kawaida lakini ni rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili kuhusu masuala ya ajira yamekuwa na utaratibu mbaya kuna rushwa ya zinaa. Hili hasa ni kwa jinsia ya akinamama mara nydingi lazima wanapoomba ajira, wale wanaohusika huwataka akinamama hao mapenzi. Nayo mapenzi lazima ayatimize, asipoyatimiza kweli hawezu kupata ajira. Kwa hiyo, hilo naamini Serikali hajjaliangalia kwa makini kuona kwamba ni tatizo limo ndani ya jamii, rushwa ya zinaa. Hili lazima Serikali iliangularie kwa makini na kuangalia namna ya kulifanya utatuza ili lisiwepo ndani ya jamii yetu.

Tatizo la tatu au aina nydinge ya rushwa ni *Political Corruption*, nasema kwa sababu hapa ndiyo wasimamizi wa Ikulu. Suala la *Political Corruption* kuna watumishi wapo ambao wanawekwa tu kwa sababu ya rushwa ya kisiasa. Wanafanya kazi kwa kumbembelezwa, kwa kufadhiliwa tu kwamba, huyu

anastahili ni mwenzetu, ni sisi katika sura nyingine yaani ni ndugu yetu wa karibu sana, lakini ukiangalia utumishi wake haupo katika utaratibu wa utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wako watumishi wa aina hiyo. Utumishi wetu tunajua kwamba mwisho ni miaka 60, lakini wapo watumishi wengine mpaka sasa wana miaka 70, 72, 73, wengine wana vipindi viwili au vitatu vya Mkataba wa miaka miwili miwili, wakati wengine tumeshawatoa kwa kupunguza watumishi walio chini ya umri huo kwa kustaafu kazi. Sasa kitu ambacho kwa kweli hata kama ni sera, hata kama ni mipango mizuri na mikakati mizuri hapo inaharibika yote. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi ambao wameshafikia umri wa kustaafu lazima waondoke. Wale watumishi ambao bado wanastahili na miaka yao ingali katika hali ya utumishi, basi wabaki katika utumishi. Lakini tunapofanya hivyo, kwa kweli mimi siwaelewii kama ni sera na kama ni uwazi haupo kwa hawa watumishi ambao wamezidi umri wanawekwa kwa sababu ya *Political Corruption* ili wawalinde au wafanye nini katika mtu yule aliyemweka. Kwa kweli hili mimi naomba lingezingatiwa kwa wale wote ambao wamezidi umri hata kama ni mwenzetu na kama ni ndugu yetu basi wakati umefika aache kazi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la nne ni *Commercial Corruption*. Ni masuala ya kibashara biashara, ambayo sasa yanazagaa katika nchi yetu na suala hili la biashara unaliona kama mtu anafanya Mikataba, lakini mikataba ile ina maslahi na yule ambaye anaweka Mkataba mle hasa anayewakilisha nchi yetu. Kwa hiyo, utakuta kwamba mtu yule anafanya Uwakala, lakini kwa namna ya kuweka maslahi kwake na yakikubalika hayo maslahi yake ndipo anaweka saini. Kwa hiyo, hiyo ni *Commercial Corruption* ambayo ni mbaya inaua nchi yetu. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi ningeomba kwamba Utawala Bora kwa masuala haya na Kitengo hiki ambacho kinashughulikia masuala kwa kweli wangeyazingatia na kuyaona wasiangalie kwa mtazamo mmoja tu wa kuona mtu mpaka atoe fedha kwa mtu fulani ndiyo ionekeane kwamba hiyo ni rushwa. Lakini kwa vyovyyote vile yapo hayo maeneo makubwa na mazito na mabaya sana, ambayo yanasaababisha rushwa izidi kushamiri. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali na kuishauri kabisa kwamba, iliangularie upya na ikiwezekana ifanye tathmini juu ya suala hili la rushwa nchini kwanza chanzo ni nini? Kikieleweka chanzo basi tunaweza kulitatu tatizo hili. Bila kujua chanzo tutaendelea na rushwa hii mpaka mwisho wa dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali naiomba ipange mpango mpya wa kupambana na tatizo hili la rushwa. Kwa sababu tatizo hili limekuwa kama ni donda ndugu ambalo haliponi na watu wanaofanya hayo mambo wanajulikana, lakini hawakamatwi wala hawafungwi. Sasa hapa tunasomewa taarifa hizo nyingi kweli majalada yamefungwa, majalada yapo mezani tu hayashughulikiwi. Kwa hiyo, naomba suala hili Serikali iliangularie upya na ipange mkakati mpya wa mapambano katika suala la rushwa. Vinginevyo tutaendelea hivi hivi na bahati nzuri na mbaya Utawala Bora uko chini ya Ofisi ya Rais, sasa likionekana bado na ndiyo Jemadari Mkuu, anayepambana na suala hilo la rushwa wakati sasa umeshamiri inaingia ndani na mizizi imekolea kwenda kwa wananchi na kuumiza Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofsi*)

**MHE. CHRISTANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kuhusu hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, mimi naunga mkono hoja hii na nampongeza vilevile Mheshimiwa Waziri, kwa kuiwasilisha vizuri. Pia ningependa kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais mwenyewe, maana ndiyo mwenye jukumu, kwa kazi nzuri anayoifanya kwa nchi hii. Vilevile napongeza Vyombo vya Dola vinavyomsaidia Mheshimiwa Rais kuongoza Serikali vizuri. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la *TASAF* na mimi ningependa niseme kidogo kwa sababu kwa bahati nzuri Wilaya yangu mimi na Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, tuna Mradi wa *TASAF* katika Wilaya yetu. Kwanza, napenda nishukuru namna Mradi huu unavyotekelvezwa katika Wilaya yetu, watendaji ni waaminifu na wanafanya kazi vizuri sana. Pia na mimi na mwenzangu Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, tumeshirikiana vizuri sana kwa sababu kila miradi inayoanza inawashirikisha wananchi na sisi Waheshimiwa Wabunge tunajua kila mahali ambako mradi unatekelezwa. Kwa hiyo, napenda niseme kwamba, Mpango wa *TASAF* ungepaswa kuigwa hata kwa kazi zingine kwa namna unavyoshirikisha wananchi na mafanikio haya yametokana na kuwashirikisha wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, juzi nilipokuwa kwenye Jimbo langu, kwa sababu ya ari na moyo wa watu katika moja ya Kata za Jimbo langu, wananchi wa kawaida tu viongozi wao bila raia, viongozi tu waliweza kuchanga shilingi milioni 16/= kwa ajili ya miradi inayotekelvezwa na *TASAF* kwa sababu wameelewa faida yake. Kwa hiyo, napenda kupongeza Mpango huu wa *TASAF*. Vilevile ningependa kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa *TASAF*, Ndugu Kamba na wenzake. Kitu ambacho sisi tumeshuhudia kwenye Wilaya yetu ni kwamba, kila miradi inapolekwa majibu hutoka kwa wakati wake hawacheleweshi majibu na hakuna *bureaucracy* katika chombo hiki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya hayo ningependa niseme kiasi kuhusu suala la Utawala Bora na rushwa. Mimi nitayaunganisha yote kwa pamoja. Kabla sijasema naomba kwa ruhusa yako niseme kuwa Sera ya Kupambana na vita dhidi ya rushwa ni Sera ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha Mapinduzi kiliweka sera yake na kutaja jambo hili kwa uzito kabisa kwa sababu Chama hiki hakipendi rushwa, kingependa kupambana na wala rushwa na nitasoma katika Ibara ya 100 mpaka 103 ya Kitabu cha mwelekeo wa CCM kwa mwaka 2000 - 2010, inasema hivi nanukuu: "Juhudi za kupambana na uozo wa rushwa nchini zimeanza kutoa matunda. Kazi ya kupambana na vitendo vya rushwa ni kazi ya kudumu na inahitaji uongozi uliojitlea mhanga kupambana na vitendo hivyo. Ibara ya 103, inasema kwa kuzingatia uzito wa tatizo lenyewe CCM, itahakikisha kuwa Serikali inaendelea na mapambano hayo kwa kasi kubwa na kwa kushirikisha wananchi." (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu gani? Naomba waniwie radhi wenzangu, mimi hapa sijawahi kusimama nikapiga kelele ya jumla kwamba kuna rushwa. Mimi huja na hoja ninayohisi ndani yake kuna rushwa. Wasiwasi wangu ni pale viongozi kila anayesimama anasema rushwa, lakini hawezo kutoa ushahidi kuhusu vitendo vya rushwa. Mimi napata woga kidogo. Kwa sababu gani? Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wa CCM na Wapinzani, kwa kuwa tunachukia rushwa kama kila Mheshimiwa Mbunge angepamba moto kwenye Jimbo lake hii rushwa ingekwisha katika nchi. Sasa tunamwachia nani wa kudhibiti rushwa? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nawaomba Waheshimiwa Wabunge, niwaalike kwangu, mje msikie wananchi wa Jimbo langu wanasema nini kuhusu rushwa. Kazi yangu mimi nilipokwenda kuomba kura niliwaambia wananchi mkinichagua kazi yangu ya kwanza ni kupambana na rushwa na maonezi. Mimi nimefanikiwa nilishahamisha watumishi waajiriwa, kama nikikuta Kamati ya Siasa ya Kata yangu ina ushahidi wa kumwita mtu anayekula rushwa au anashukiwa, mimi kazi yangu ni kumrudishia waliomleta Serikalini na nimefanya hivyo.

Juzijuzi Mkuu wangu wa Wilaya alikwenda kumbeba Daktari wa Zahanati kwa sababu watu walishalalamika na ushahidi upo. Nikamwambia DC nenda ushahidi huu na upelelezi umefanyika nenda kachukue yule mtu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yapo mambo ambayo mimi siwezi kuyasema hapa Bungeni. Kwa sababu kule Mkoani kwangu maonezi ni makubwa sana katika Halmashauri zetu. Sasa lazima Waheshimiwa Wabunge, tuanzie pale kwenye Halmashauri kule ndiko kuna Miungu watu wanaowatesa wananchi. Sasa tukilia wote hapa Bungeni, Waheshimiwa Wabunge wanalia, Waheshimiwa Mawaziri wanalia na kila mtu analia kuhusu rushwa, sasa nani atashughulikia rushwa! Mheshimiwa Waziri, ambaye ana madaraka anaweza akakemea wafanyakazi wa Wizara yangu, naomba msithibutu kula rushwa, lakini akisema kuna rushwa katika Wizara yake lazima akubali kuwajibika, maana yake yeze ndiye anayetakiwa kusafisha rushwa katika Wizara yake. Hapa naomba tutofautishe wananchi hawawezi

kunung' unika kuhusu rushwa, Waheshimiwa Wabunge wanunung' unika kuhusu rushwa na Waheshimiwa Mawaziri wanunung' unika kuhusu rushwa, nani ataondoa rushwa katika nchi hii. Kwa hiyo, mimi natoa *challenge* kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Upinzani na wa CCM twendeni tukapambane na rushwa katika Majimbo yetu na tuwaseme wanaokula rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitawapa mfano mmoja, nimeanza kazi mpya sasa kila ninachojua namwandikia Mheshimiwa Waziri anayehusika na nakala kwa mkubwa asipoifanyia kazi nitaileta Bungeni. Eeeh nawapasha bwana kwako kunanuka rushwa. Ndiyo mimi nasema kwa Waheshimiwa Wabunge wa CCM, naomba tusiwafanyie kazi Wapinzani. Tusiwafanyie Wapinzani kazi ya bure wako humu kwa nini hawaleti ushahidi? Kwa mfano, wamesimama hapa wanasema kuna rushwa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nasema kazi moja ya Vyama vya Upinzani ni kuibua Serikali zenye udhalimu, ufisadi na rushwa ndani ya chombo kama hiki. Sasa mimi natoa *challenge*, kama kweli Serikali hii inanuka rushwa kama inavyoolezwa na rushwa imekithiri, Wapinzani wanafanya kazi gani hapa Bungeni, wamekuja kutembea au wamekuja kufichua makosa, walete hoja hapa na ushahidi wa kuonyesha jinsi Serikali inavyonuka rushwa. Sasa sisi wenyewe tunaumana meno. Watu wa nje wanatusifu. Mimi nitawapa ushahidi hapa, mimi sipendi kusema vitu kienyeji, nitawapa ushahidi hapa. Watu wanaotujua wanatusifu kwa mfano, mimi nimetembea na naomba Ofisi ya Spika, muongeze juhudui ya Waheshimiwa Wabunge, kwenda nchi za nje kuona mambo. Mimi natembea sana mwenyewe sijawahi kupata kupelekwa nje ya nchi na Ofisi ya Spika, nakwenda mwenyewe kwa uwezo wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa Australia na nilikuwa London, sifa ya Tanzania nje ni kubwa sana. Wananiambia Bwana Christant Mzindakaya, nchi yenu mmefanya nini sifa nzuri duniani? Kwa mfano, kwa mambo ya uwekezaji sisi sasa tunalinganishwa na Bolivia kwa sifa. Serikali yote ovyo inayonuka kwa rushwa, haiwezi kupata wawekezaji itawapataje? Sasa ninyi mnajitukana wenyewe, mambo yenu ni mazuri na sifa ni kubwa, mnajitukana wenyewe na mnajivua nguo wenyewe. Mimi nashangaa kweli! Rushwa inayofanyika Tanzania ni ndogo ndogo hata kubwa naomba tuzilete hapa. Mimi naomba Mbunge yejote, kama anaogopa anipe watu anaowajua kwamba ni wala rushwa mimi nitawashughulikia. Anipe mimi nitawashughulikia si mnaogopa kusema kweli, ni unafiki vilevile kusema uongo, watu wazima mtasemaje hapa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape takwimu hapa kuna *Organisation* moja inaitwa *AFRO Peromita*, wametengeneza *paper* Namba 11. Wamefanya utafiti katika Tanzania. Wamefanya kazi mbili. Moja, kuhusu Utawala Bora na rushwa katika nchi hii. Kazi hii waliifanya mwezi Septemba, 2001. Hawa ni wenzetu wanatupima walifanya *sampling* kwa nchi zaidi ya 12 za Afrika. Sasa katika utafiti huo, nchi zilizohusishwa ni hizo 12, nazo ni Botswana, Ghana, Lesotho, Malawi, Mali, Namibia, Nigeria, *South Africa*, Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe. Sasa wanasema kwamba, Watanzania walielezwa kama ndiyo pekee wanaoamini Taasisi zao kwa wastani wa asilimia 81 wakifuatiwa na Namibia asilimia 71, wananchi wanatusema vizuri pamoja na Bunge hili na nitawaambia wanasema nini juu ya Bunge hili, hivi ndivyo wanavyotusema. Hilo la Kwanza.

La pili, kuhusu utendaji wa viongozi wa kuchaguliwa ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, Rais, utafiti huo unaonyesha kwamba, Marais wa Afrika wanapewa asilimia 55 kwa jumla ya Marais. Lakini Marais wa Tanzania kwa mfano, Rais wa Tanzania amepewa asilimia 90 anafuatiwa na Rais Museveni. Mimi nasoma taarifa yao, sitoi moyoni juu ya Museveni, natoa maoni haya hapa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani tumepewa asilimia 68 mpaka 70, sifa yetu kwa wananchi na hata kwenye rushwa wamewatetea viongozi wa kuchaguliwa *percent* ndogo sana inafika kama 40 hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niseme hili jambo kwa sababu sisi wenyewe tunajiumiza bila kujua kama tunajiumiza na tunawafanyia kazi watu ambao hawafanyi kazi yao pale pembeni. Kwa mfano, bila kutia chumvi wote ni mashahidi, taarifa hizi zinathibitishwa na Mkutano Mkuu wa CCM. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM walimpigia kura Mwenyekiti wao wa Chama cha Mapinduzi kwa asilimia 100 kuthibitisha haya. Leo kama ungekuwa unawapanga Marais 10 bora wa Tanzania, hawezikukosa humo Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, atakuwemo tu katika 10 bora. 10 bora ni pamoja na

wasaidizi wake, maana yake haning'inii peke yake, anafanya kazi na watu. Kwa hiyo, mimi nasema tuanze kushughulikia watu mmoja mmoja hapana kujumlisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ningependa kulisema na hili mimi naona ndiyo kero. Ndani ya Serikali yetu baadhi ya Waheshimiwa Waziri, wameachia Watendaji wa Serikali kuendesha Wizara. *Wame-surrender wisdom* yao, wataalam ndiyo wanaamua kila kitu. Ukienda kwa Mheshimiwa Waziri ukimwambia jambo, anasema ooh ngoja niulize wataalam, ukirudi kesho anasema wataalam hawajasema. Mimi nimeshuhudia miaka ya 80, Rais, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alimfkuza Mheshimiwa Waziri, kwa ajili ya majibu ya wataalam kusema anasubiri, akasema wewe unaabudu wataalam achana na Wizara yangu. Hii ya kuabudu wataalam, wataalam ni washauri. Kwa nini nyie Waheshimiwa Mawaziri, mnawaachia wataalam ndiyo waamue mambo, acheni hii! Wanajijua wengine nilishawaambia nawahurumia kwa leo. Kwa hiyo, nasema hili jambo *seriously*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho wenzetu wanatusema na nyie wote mnakiona, *bureaucracy* imezidi katika Serikali, maamuzi hayatoki kwa wakati wake. Hii ni kasoro ambayo ndiyo mimi naomba muirekebishe Waheshimiwa Mawaziri wetu. Kasoro ya *bureaucracy* chukueni madaraka amueni, kuamua ni kuamua, wakati hata kama umekosea bora uamue. Wengine wanaogopa nikiamua sasa nitaonekana nakula rushwa. Sasa si bora uamue, kuamua ni kuamua tu acheni woga wa bure. Serikali mmepewa muiendeshe. Mimi pia nilishawahidi kuwa Waziri na nilishakuwa Mkuu wa Mkoa, mimi nilikuwa naamua siwezi kuacha kuamua nani ataniamulia kazi yangu, si niamue tu hata kwa makosa. Haiwezekani kutembea na mafaili kila siku kwenda kwa Rais, amueni mambo mkosee, bila Mheshimiwa Rais wanashindwa kufanya kazi kila kitu wewe. Sasa Mheshimiwa Rais ndiyo anakuwa anawasimamia Mawaziri mgongoni watekeleze wajibu wao, hii si sawa. Amueni mambo mmepewa madaraka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja hii. Naomba wote tupambane kwa vitendo kuondoa rushwa. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nina mafua kidogo lakini nitajitahidi. Kwanza na mimi napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, anayeshughulikia utumishi kwa kuwasilisha hoja yake vizuri na amejitahidi kuchambua mambo kwa undani zaidi. Nitaongelea labda mambo matatu.

La kwanza, ni hili la maboresho ya Utumishi Serikalini. Mheshimiwa Waziri, ameeleza mambo mengi kuhusu maboresho na matumaini yake ya baadaye kwamba, italeta utumishi bora Serikalini. Lakini mimi nataka niongeze tu kwamba, maboresho peke yake bila kuwa na usimamizi imara, hayawezi kuleta mabadiliko yoyote. Lazima viongozi walimo Serikalini wawe tayari kusimamia kazi zilizo chini yao na wawe tayari kuwasimamia watumishi walio chini ya ngazi zao. Mkitegemea tu kwamba maboresho tumeyaona tangu yalipoanza mpaka leo katika baadhi ya ofisi mabadiliko yaliyotokea ni kidogo mno kama yapo. Baadhi ya maeneo utakuta utendaji bado ni ule ule kama uliviyokuwa kabla, bila nidhamu maboresho peke yake hayatafanya kazi. Kunahitajika nidhamu ya hali ya juu na hili nataka niunganishe kwamba, katika Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, suala la nidhamu ni muhimu likawepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la watu kutokuwa na nidhamu na hawatekelezi yale wanayoambiwa wayafanye pamoja na maelezo mazuri yaliyotolewa na Serikali. Nitatoa mfano mmoja, wakati tunabadilisha mfumo kwamba, watumishi wa Serikali wa ngazi za juu wakopeshwe magari wawe na magari yao, ilikuwa ni kukinga magari ya Serikali yasitumike oyoo nje ya wakati wa kazi. Lakini kinachotokea leo ni kwamba, watu wamekopeshwa magari wameyafungia nyumbani bado wanatembelea magari ya Serikali. Mimi sitazamii kumwona Mheshimiwa Waziri au Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, ambaye amekopeshwa gari anakwenda kusali kanisani au msikitini na gari la Serikali wakati anatakiwa awe na gari lake mwenyewe. Wanakwenda mpaka sokoni na wanakwenda kubeba pumba na magari ya Serikali badala ya kutumia magari yao na Serikali mko hapa mnatureleza kwamba, mabadiliko yanakuja kuboresha. Tunataka mabadiliko hayo yazingatie pia suala la nidhamu na kusimamia kazi ambazo mmezitoa. (*Makofî*)

Halafu pia katika magari ya Serikali, kuna suala la kuzuia mtu asiyeruhusiwa kuendesha gari la Serikali. Kwa mfano, labda sheria imebadilika hivi karibuni, lakini zamani ilikuwa kwamba Viongozi wa Serikali hawawezi kujijendesa wenyewe kwenye magari ya Serikali, lazima waendeshwe na madreva walioajiriwa na Serikali baada ya kuthibitishwa kwamba, ni madreva wazuri. Lakini bado leo hii unakuta kiongozi wa Serikali anaendesha gari la Serikali yeze mwenyewe amemuacha dreva na mfumo wa Serikali upo mnamtazama tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwajibikaji na kufutilia yale mnayoyaamua ni baadhi ya mambo ambayo katika maboresho yatakuwa ni muhimu ili maboresho hayo yaweze kuzaa matunda, bila kufutilia haina maana, hata hii ya kusema kwamba mimi ni Waziri au mimi ni Mkuu wa Mkoa au mimi ni Kiongozi nipo Dar es Salaam nitajua yanayotokea Kasulu au yanayotokea kule Serengeti, hiyo siyo kweli. Mgawanyo wa Serikali ulivyoundwa unakuwezesha wewe kufutilia mambo mpaka chini kabisa, vinginevyo kama huwezi kufutilia mpaka kule ambako unatakiwa kufika, basi hiyo kazi imekushinda. Mfumo uliowekwa unakuruhusu ufuutilie mambo mpaka ngazi za chini. Kwa hiyo, nilitaka kusemea hilo.

Vilevile katika suala la nidhamu, ninashangaa kuona kwamba katika nchi yetu imefika mahali ambapo viongozi wa siasa wanaanza kubishana hadharani na watu waliomo katika *uniform*. Katika taratibu za nchi nyingi zilizopo ni kwamba, watu waliopo katika *uniform* yaani katika Majeshi mbalimbali, hawawezi kubishana na wanasiwa hadharani, wao matatizo yao wanayapitishia kwa viongozi wao wa kisiasa. Lakini katika Tanzania inafika mahali unaona watendaji katika vyombo vyta *uniform* nao wanasiwama hadharani kubishana na wanasiwa ambao ndio viongozi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Jenerali wa Zimbabwe aliwahi kusema kwamba, wao hawatamkubali Rais kutawala Zimbabwe ambaye hakupitia mapambano ya kutafuta uhuru. Huyo Jenerali alionya na Viongozi wa nchi za SADC, wakasema si kazi yake kusimama hadharani na kutamka maneno ya kisiasa. Mambo ya wanasiwa awaachie wanasiwa.

Sisi katika Tanzania imefika mahali watu waliomo katika *uniform* nao wanasiwama hadharani kubishana na wanasiwa. Hili ni kosa na tena mlikomeshe kabisa lisiwepo watu katika *uniform* wawattii viongozi wao na kama wana tatizo walipeleke kwa Waziri wao, aliyeusika ndiye aje azungumze na wanasiwa wenzake. Sio mtu katika *uniform* na yeze anasimama anaanza kubishana na wanasiwa. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda niyaseme haya katika kuanzia, lakini la pili ambalo nataka nilizungumze linahusu Utawala Bora. Katika Utawala Bora, misingi yake mikubwa ni kuzingatia sheria, haki na demokrasia, kulinda usalama wa raia pamoja na mali zao, nimezungumzia pia kuwepo kwa nidhamu ndani ya mfumo mzima wa uendeshaji na kuheshimu haki za binadamu na pia sheria kutobagua mukubwa au mdogo ndio mahali ambapo kunakuwepo na Utawala Bora. Baadhi ya mambo ambayo yaliyokuwemo katika suala hilo ni pamoja na kuhakikisha kwamba, Watendaji wake wote wanatekeleza majukumu yao, hawatumii madaraka waliyonayo kuwanyanya au kuwaonea watu wa ngazi za chini. Ndiyo maana kuna kipindi fulani Mheshimiwa Rais, aliwahi kusema kuna baadhi ya watu ngazi za Kata kule wanajifanya Miungu watu. Mheshimiwa Mbunge, mmoja wetu sasa hapa amezungumzia kwamba, ngazi za Halmashauri ya Wilaya kuna watu wanajifanya Miungu watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nitoe mfano mmoja. Kule Wilayani kwangu Chunya kulitokea jambo fulani. Kuna mtu mmoja anaitwa Bwana Kadu alikuwa na mbao zake. Yeye alikuwa anajenga nyumba ya kulala wageni akanunua mbao nyingi, nyingine akapasua yeze mwenyewe porini akazihifadhi nyumbani mwake ili zije zimsaidie kuezeka, kupaua kutengeneza madirisha, milango na samani za ndani. Ikatoka kwamba Mkuu wa Wilaya yeze akaenda alipopata habari kwamba yule bwana ana mbao akaamrisha mbao zile zikamatwe. Baada ya kuzikamata akamwamrisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (*DED*), azichukue zile mbao na kuzipeleka pale Makao Makuu ya Wilaya. Kweli akazipeleka na baadaye akamwamrisha *OCD* apeleke kesi Mahakamani. Kesi ikapelekwa Mahakamani. Baada ya kufika Mahakamani Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikachukua jalada hilo kulipitia

kuona kesi ikoje. Alipolipitia hilo jalada *DPP*, Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali, akaona kwamba yule bwana mbao zile zilikuwa ni halali, ni mbao zake na zilikuwa zimegongwa na watumishi wa Idara ya Maliasili, kwa hiyo zilikuwa ni mbao halali za kwake.

Kwa hiyo, akarudisha taarifa kwamba hiyo kesi haiwezi kufikishwa Mahakamani na akaagiza mbao zile arudishiwe mwenye mbao. Baada ya kufanya hivyo, Mwanasheria wa Serikali aliyepo pale Mbeya, naye akamwandikia *OCD* kwamba kesi ile haipo na mbao zile arudishiwe mhusika. *OCD* akamwandikia Mkurugenzi kwamba, arudishe mbao kwa mwenye mbao. Lakini baada ya hayo yote, Mkuu wa Wilaya, akazuia zile mbao yule mtu asirudishiwe. Hivi huo ni Utawala Bora au ni mtu anatumia madaraka aliyonayo. (*Makofi*)

Kama tunaheshimu Utawala Bora ni pamoja na kuzingatia mgawanyo huu wa madaraka na kuzingatia sheria za nchi. Sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali huyu Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali, ameona hakuna kesi na ameagiza kwamba, mbao zirudishwe kwa mhusika, bado Mkuu wa Wilaya ameng'ang'ania kwamba, hizo mbao hawezi kurudishiwa, wana malengo gani, wanataka kugawana hizo mbao au ni kutumia tu nguvu au ubabe wa madaraka?

Mimi nilikuwa naomba kwa Waziri Mhusika na Utawala Bora, unipe jibu leo kwamba kwa nini huyu mtu hajarudishiwa mbao zake mpaka sasa baada ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusema mbao zile arudishiwe na *OCD* kuandika barua kwamba mbao zile arudishiwe, kwa nini bado wanashikilia mpaka sasa? (*Makofi*)

Mimi naomba jibu hilo nilipate leo leo kwamba hizo mbao yule mtu atarudishiwa au hapana basi tujue la kufanya baada ya hapo. Kwa sababu katika nchi hii tusianze kuchukua madaraka makubwa ambayo hatunayo au ni kumwezesha mtu ambaye hana madaraka. Mtu amesharuhusiwa kuchukua mbao zake na imethibitika kwamba alikuwa anajenga na kweli anajenga mpaka sasa. Mimi mwenyewe nimefika kwenye jengo lake alilokuwa amelijenga, nimeliona. Leo anaambiwa mbao zake hawezi kurudishiwa kwa nini? Hatuwezi kuendesha kwa hisia, kama ana ushahidi angeutoa basi. Watakapokuwa wanarudisha wahakikishe wanazirudisha mbao zote alizokuwa nazo kama zimepungua itabidi walipe. (*Makofi*)

### **MBUNGE FULANI: Ndiyo!**

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema Mkuu wa Wilaya labda nifafanue hapa pia kwamba aliyejikuwa amefanya vile amefutwa kazi na Rais juzi juzi hapa. Kwa hiyo, nayo aliyejuka hahusiki kwa sababu yeze ni mgeni, lakini kwa sababu cheo ni kile kile ameyakuta hayo mimi ningombaa maelezo maelezo kwamba mbao zile amerudishiwa mhusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spia, la tatu linahusiana nizungumzie jambo la rushwa. Pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Mzindakaya, aliyojata hapa hayafuti kwamba rushwa ipo ndani ya Tanzania. Mwezi Mei, 2002 Mheshimiwa Rais alikuja kuongea na Wabunge katika mukutano wao wa kutathmini mambo ya rushwa hapa Bungeni na alitoa hotuba hii tarehe 27 Mei, 2002. Katika *paragraph* ya kwanza anasema na nanukuu: "Ni wazi kuwa pamoja na jitihada zote za kuzuia rushwa, hakuna uhakika wa kufuta kabisa rushwa". Kwa lugha nyingine ni kwamba, kwa maelezo haya alikubali kwamba, rushwa ipo ndani ya Tanzania. Mimi nasema rushwa ipo na lazima tuijadili na lazima tuelekezane mambo ya kufanya ili tuweze kufuta. Kutusifu watatusifu kutokana na hatua tunazozichukua, lakini marehemu Mwalimu Nyerere, alisema kama unataka kuangusha ukuta ukipasuka usiache kuutwanga endelea kutwanga mpaka uanguke. Uktionyesha mwanya umepasuka ukiacha hautaanguka na rushwa lazima tuendelee kuipiga vita mpaka itakapotokomea.

Sisi tumesema hapa, Rais anasema katika hotuba ile ya tarehe 27 Mei, 2002 ukurasa wa 9. Nanukuu: "Sera yetu ni kutovumilia rushwa hata kidogo kwa kwa Kiingereza (*0 tolerance*) ni kwamba, rushwa isiwepo kabisa". Lakini leo rushwa tunaiona ipo na wananchi wanaumia na rushwa na wanaotuhumiwa na rushwa kinachofanya rushwa iondolewe katika Tanzania ni pale ambapo wanaotuhumiwa na rushwa hawachukuliwi hatua yoyote. Kutokana na hilo watu wamezoea kwamba hata akifanya nini hataondolewa au hatachukuliwa hatua yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna mambo ya Mahakama, Serikali inaposema kwamba watu walete ushahidi hiyo sio njia ya kupambana na rushwa. Hutapambana na rushwa kwa njia za ushahidi wa Kimahakama. Lazima kuwe na *Political Responsibility* na *Political Accountability*. *Political Accountability* inakutaka wewe uliyemuweka mtu katika madaraka anapokuwa na matatizo umchukulie hatua za kisiasa, za kiutowala na wala usingoje hatua za Kimahakama. Hatua za Kimahakama ni ngumu sana. Rais katika hotuba alisema sitowenza kuwafikisha Mahakamani lakini yatakayotoka kule sisi hatuma madaraka nayo na ni kweli. Serikali haina madaraka mbele ya Mahakama. Mtu huwezi kumfikisha Mahakamani kuthibitisha matukio kama haya ya rushwa ni ngumu sana na mtu anaweza akaachiliwa pamoja na kwamba hajapokea rushwa bado anaweza akaachiliwa *on technical grounds*. *Technicalities* anaweza akatoka.

Lakini tunachotaka sisi ni kwamba, wale *appointing authority* ya wanaohusika wawajibishwe kisiasa, wawajibishwe kiutowala ndipo mtakapopambana na rushwa. Ni katika mfumo huu wetu sasa hivi ambapo unaona kwamba hakuna anayewajibishwa kisiasa. Hata wakatiwa Mwalimu Nyerere, watu walikuwa wanawaambia kisiasa wakionekana kwamba wana matatizo walikuwa wanawajibishwa. Lakini leo imetuwa kwamba mtu anayetuhumiwa au anayefikiriwa kwamba amepokea rushwa anabaki vile vile bila kuguswa badala yake Serikali inasema tunataka mtuletee ushahidi wa Kimahakama. Nani mwananchi wa kawaida atakayekaa anampeleza kiongozi fulani mpaka apate ushahidi wote utakaomuwezesha kwenda Mahakamani, ni mwananchi wa namna gani huyo na muda wenyewe ataupata wapi? (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ule ule mnapotaka kwamba mwananchi ndiyo alete ushahidi Serikali ina Polisi na *CID*, Idara ya Usalama na vyombo vyote vya dola ambavyo vinaweza vikatolewa mambo haya viko mikononi mwa Serikali na wanalipwa mshahara na kodi ya wananchi wetu. Bado mnataka wananchi ndio waje watoe ushahidi kwenye Mahakama. Hili ni jambo ambalo haliwezekani. Kama nia ya kupambana na rushwa ipo lazima mtazamo pia ubadilike. Kama ipo nia lazima mtazamo ubadilike na hatua za kuchukua zibadilike. Wakati hii awamu ya tatu ilipoingia kwenye madaraka, kwa kweli kwa kupambana na rushwa iliingia kwa kishindo na kila mtu alipata matumaini kwamba sasa mapambano yameanza. Lakini kadri muda ulivyokwenda, ndivyo ambavyo mambo yalizidi kuzorota na mpaka sasa suala lenyewe kwa Kiingereza linasema limeshakuwa *watered down*, halina nguvu tena. Tungependa tuendelee mpaka mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasubiri majibu ya Waziri ahsante sana. (*Makofsi*)

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, mimi naunga mkono moja kwa moja mia kwa mia. Mimi nitazungumzia kwenye Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yangu mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wanachama wote wa *African Parliamentary Network Against Corruption Tanzania Branch*, tunaomba kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imetuwa chachu kwa kutusaidia sisi Wabunge na hasa Wabunge wa hii *Association* ya Kupambana na Rushwa kujua wajibu wetu, *The Role of Parliamentarian in Fight Corruption*. Naomba nimshukuru sana kwa dhati, ninamwomba kabisa aendelee kutusaidia tukiwa tunaelewa tutatekeleza majukumu yetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili naomba pia niishukuru *PCB* chini ya Mstaafu Meja Jerenali Kamanzima, kwa kutusaidia sisi maana *PCB* imesaidia Bunge kujua rushwa ni nini na sisi wajibu wetu ni nini. Naomba kwa kuititia hapa Bungeni, nimshukuru Mheshimiwa Ndugu yetu Hossea, amefanya kazi ya ziada kutufanya kazi sisi Wabunge ili tuweze kujua majukumu yetu.

Pia naomba niishukuru *UNDP* semina zote za Wabunge mlikuwa mnazipata ni *UNDP*, kwa kuititia Wizara tumeweza kupewa fedha za kufanya semina. Wanasema hivi sasa wanajiandaa kwa sababu katika *recommendations* zetu tulitaka kufanya *standing order review*, tuliweka *recommendation* wanasema watatusaidia. Kwa hiyo, naomba nitoe shukrani hiyo. (*Makofsi*)

Lakini pia naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri, *APNAC Tanzania* imekuwa mfano katika dunia. Kwa sababu gani? Wamesema wanashangaa kwa nini *Tanzania APNAC* inapata msaada mkubwa na Serikali inawapa msaada kuliko nchi zingine. Wanashangaa wanasema wanataka waje wajifunze. Lakini moja tuliloliona *APNAC* sehemu nyingi za dunia imeanzishwa na *Opposition* na *Opposition* sio kwa nia ya kupambana na rushwa ni kwa nia ya kutaka kuchukua nchi. Lakini *Tanzania APNAC* imeanzishwa na *Opposition* na *Ruling Party* tumekaa pamoja kwa kusaidiana na Serikali yetu ili tupambane na rushwa. Kwa hiyo, wanashangaa tunapewa msaada na wanataka kuja kujifunza kwetu. Kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Waziri endelea kutusaidia na sisi tuwe mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nakuomba Mheshimiwa Waziri ulisaidie Bunge. Katika mikakati ya kupambana na rushwa, nguzo mbili zimeshaandaa *Action Plan*. Serikali katika Idara zake mbalimbali, Mahakama imeandaa lakini Bunge haina. Sasa mimi nakuomba Waziri ulisaidie Bunge, kwa sababu katika ile mikakati ya kupambana na rushwa tulitaja mpaka Bunge liwe na *Action Plan* na iwe produced ili ioneckané katika kitabu chako cha Idara mbalimbali jinsi ya kupambana na rushwa. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba kwa kweli ni jambo la kusikitisha Bunge halina *Action Plan* ya kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ninaomba Waziri asilifumbie macho kilio cha wananchi kwamba sehemu kubwa ya Mahakama haiwatendei haki. Ingawa linasemwa halipo lakini nakwambia lipo. Mficha ficha ugonjwa kilio kitamfichua. Wananchi sasa hivi wamechukua madaraka mikononi mwao kupiga wezi, kuua wezi ni kwa sababu ya kutokuridhika na Mahakama. Kwa hiyo, mimi ninachokiomba tutafute utaratibu na mimi narudia na kila popote nitakaposimama nitarudia Bunge lina chombo cha kuwadhibiti ndani ya Bunge, wananchi wanawadhibiti na Serikali inawadhibiti na chama kinawadhibiti kilichomleta madarakani Mbunge. Serikali inadhibitiwa ndani ya Bunge, ndani ya Serikali yenye, inadhibitiwa ndani ya wananchi kwamba wasiporidhika wananchi hawaiapi kura.

Lakini Mahakama imekuwa Mungu mtu. Ina chombo chao tu cha ndani hakuna chombo nje ya Mahakama cha kuwadhibiti. Ndiyo maana Mahakama sasa hivi ni matatizo. Mimi naishi Serikali na nguzo zote hizi, tukae tutafute utaratibu wa chombo nje ya Mahakama na mimi naomba nishauri chombo ambacho naona kinafaa ni Tume ya Haki za Binadamu, wakati mtu anapothibitika amenyanyaswa na Mahakama, katika hii Sheria ya Tume ya Haki imeondolewa jambo lolote lililotolewa hukumu na Mahakama haliwezi kuzungumzwa katika Tume ile. Sasa mimi naomba ipewe haki hiyo na ndani yake wawepo pia Majaji na Mahakimu (wanasheria). Kuna kesi ambayo unaona kabisa watu wamenyanyaswa na mimi niko tayari kutoa ushahidi wa kesi ambayo hukumu inaonyesha kabisa hata mtu mwendawazimu atajua hapa haki haikutendeka. Niko tayari kutoa ushahidi, hilo naomba liendelee. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Wizara itusaidie sana *APNAC Tanzania Branch*, kufuatilia zile *recommendations* zilizotolewa katika semina mbalimbali za *APNAC*. Kuna baadhi ya *recommendations* hazijatekeleza. Sasa kwa sababu ziko nyingi, naomba nisizitoe lakini najua unazo Mheshimiwa Waziri. Lingine, tuwafundishe wananchi wetu suala zima la rushwa. Najua sasa hivi tumeanza mikakati lakini naomba wananchi wajue rushwa ni nini, ina ubaya gani.. Sasa hivi watu wanafikiru nisipotoa rushwa haki sipati. Sasa rushwa siku hizi imekuwa ndiyo haki. Kwa hiyo, mimi naomba tufuatilie. Naomba kabisa Waziri utusaidie kwa sababu katika *Action Plan* ya *APNAC* tumesema hivi Wabunge tunataka tugawane twende katika Mikoa tutazame mikakati inayofanywa ndani ya Wilaya, Halmashauri na Mkoa, wana mikakati gani ya kupambana na rushwa. Au wanasema tu, kisha tuje hapa tukupe *feedback*. Kwa hiyo, tunaomba sisi utusaidie na mimi nakushukuru nimeshaanza kuona *PCB* Mkoani inatoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Madiwani waelimishwe suala zima la rushwa na liwaingie. Mtakuja kuwalamu Madiwani kumbe hawajui. Haya yote matatizo yanayozungumzwa utendaji bora nini Madiwani inafikia wakati na natoa mfano kabisa inapofikia kuitisha kwenye tenda inatisha. Anapewa mtu tenda unamwona kabisa huyu *cripple*. Hapa naomba nichukue nafasi. Mawaziri sisi *backbenchers* tunapokuja kusema kuna tatizo mahali hatuna nia ya kuwanyanya. Tuna nia ya kusaidia Serikali yetu. Imefikia hatua Mawaziri wanainuka bila utaratibu kuona *backbenchers* wanawanyanya. Mimi naona si sahihi. Tunawasaidia nyinyi kama lina matatizo nje yawe nje sio ndani ya Bunge. Bunge tunajua sheria

inasema ukiinuka kuzungumza unatakiwa uwe na ushahidi. Kwa hiyo, ukiinuka mtu kuzungumza unao ushahidi. Mimi nilikuwa naliomba hilo tena nalizungumza kwa uchungu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize suala lingine, mimi naomba nisaidiwe watu wanazungumza kila siku suala la *IPTL* na bilioni 3 kila mwezi. Serikali haina pesa lakini tunatakiwa tulipe bilioni 3 kuilipia hiyo *IPTL*. Sasa mimi naomba ebu tulizungumze watu wanazungumza mwisho linazungumzwa vibaya, si kazi ni zuri, kwa hiyo mimi ndilo ninaomba Waziri wa Utawala Bora ulizungumze suala la *IPTL* unapotoa majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba katika *recommendations* zetu tumesema hivi suala zima la ajira katika *position* za watu wakubwa lipitishwe Bungeni. Angalau likipitishwa Bungeni tunasema fulani anafaa natoa mfano tu naomba nitoe mfano *IGP*, huyu kwa sababu ni mtu ambaye naweza kumtania. Labda mnataka kumuajiri *IGP*. Basi apitie Bungeni tu, apate kama Waziri Mkuu, anapata kura kutoka Bungeni akishachaguliwa tunakuja kumwambia unafaa, viongozi wengine wakubwa kwa nini tusiwapitishe Bungeni. Mimi nilikuwa naomba hilo. Hata mikataba, ile mikataba mikubwa mikubwa ipite ipitishwe Bungeni. Inaweza kuishia kwenye Kamati husika ya Bunge na Kamati ikatoa ushauri.

Mwisho, *PCB* wanafanya kazi nzuri sana wanapekua wanaona matatizo. Wanapotaka kwenda kupeleka Mahakamani wanaambiwa aah!! *DPP* ndiyo atakayeamu. Mnawavunja nguvu. Ninaomba wawe na right ya kupeleka Mahakamani pale wanapoona kuna ushahidi kamili, wasingoje *DPP* ndiyo atoe maamuzi. Lakini lingine mimi ningeomba pia taarifa ya *PCB* iletwe kwenye Kamati Maalum. Tulishapendekeza Bunge liwe na Kamati ya kuzungumzia masuala ya rushwa. Tulishapendekeza katika *recommendations*, iletwe katika ripoti ya Rushwa. Kamati na iwe *confidential* hatuna haja ipigive kelele ndani ya Bunge, lakini ndani ya Kamati ile izungumzwe waone utaratibu gani utaendelea. Hili mimi nilikuwa naomba nishauri.

Nilikuwa nataka kutoa mchango wangu kwenye masuala ya *Good Governance* na kwa sababu kama Mwenyekiti wa *African Parliamentary Network Against Corruption Tanzania Branch*, nimepata sifa kubwa nje kwa sababu ya Serikali ya Tanzania kuisaidia *APNAC*. Ninaomba Wabunge tuendelee pamoa na Serikali yetu, Wabunge wa pande zote mbili, upande huu na upande wa Upinzani wa twende tusaidiane tuhakikishe suala la rushwa linaondoka na anayesema rushwa haipo si kweli. Kwa sababu ingekuwa rushwa haipo Rais asingeunda Tume ya Warioba (*Warioba Commission*). Amejua kuna tatizo hilo kwa hiyo amelitafutia mikakati. Ukitataa kuna tatizo matokeo uthalitafutia mkakati. Kwa hiyo, Serikali imefanya mikakati kuhakikisha inapambana na rushwa. Isipokuwa nashauri tuiseme rushwa ni kansa hapana. Kansa maana yake matibabu yake haifiki *hardly ten years* ina *re-occur*. Tuseme rushwa ni donda ndugu. Kwa *Medical* inaitwa *Tropical Ulcer*. Ni shida kulitibu lakini ukikazana linapona.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja .

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi kuchangia kidogo hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora.

Kabla suaanza kuchangi, napenda kuchukua nafasi hii kusema kwanza, naiunga mkono hoja, sina matatizo nayo. Aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote wawili katika Ofisi hiyo, kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya mpaka hivi sasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mchango wangu utajielekeza zaidi kwenye jambo moja tu nalo ni Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Lakini kabla ya hapo nichukue nafasi hii na mimi kutoa pongezi nydingi sana kwa uongozi wa *TASAF*, kwa kazi nzuri ambayo walikuwa wanaifanya mpaka hivi sasa. Kwa kweli *TASAF* imekuwa ni kama kioo cha kujitazama jinsi gani tumeweza kuleta mambo yetu ya maendeleo hapa nchini. *Organization* nzuri, ufuutiliaji mzuri na ndiyo maana hata *World Bank* walipofanya *evaluation* majuzi hapa, walimwaga sifa nydingi sana kwa uongozi wa *TASAF* kwa jinsi ilivyofanya kazi nzuri. (*Makofî*)

Ombi langu kwa *TASAF* sasa ni kwamba kama walivyosema wenye katika hotuba kwamba zile Wilaya ambazo ziliikuwa zimebekwa wenye awamu ya kwanza ziko mbioni kumaliza ile awamu ya kwanza na sasa hivi Serikali kwa maana ya *TASAF*, inaandaa mpango kamambe kwa ajili ya kueneza

shughuli za *TASAF* katika Wilaya zingine ambazo zimebaki, Ruangwa ikiwa mojawapo. Tunatazamia sana kwamba hili halitachelewa na haitasubiri kumaliza au kuhitimisha miradi ambayo ilikuwa imebaki kiporo katika Wilaya zile ambazo zilikuwa katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingie kwenye *topic* ambayo imenileta hapa nayo ni *Management* ya Utumishi wa Umma. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi, ameanza utaratibu mzuri sana katika kutoa *Management* ya kisasa kwa wahudumu wa umma. Nakumbuka mwaka jana tuli-lodge programu hapa ya kusaini mikataba kati ya watendaji hao na wananchi ambao wanawahudumia. Kwa kweli hiki ni kitendo cha maendeleo. Kusimama kwangu hapa nataka kusema tu kwamba, ni jinsi gani baadhi ya viongozi hawaheshimu mikataba hiyo ambayo tulitia saini mwaka jana na mpaka sasa hata wino haujakukana tumeshaanza kukiuka yale maadili ambayo tulikuwa tunesema tutayatekeleza.

Wilaya ya Ruangwa inategemea sana kilimo. Hatuna viwanda, kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Wilaya ya Ruangwa. Bila kilimo pale hamna maendeleo. Katika mwaka uliopita tulipokuwa tunatayarisha mradi wa kilimo kwa utaratibu wa sasa wa kilimo shirikishi, tulikaa na wenzangu viongozi wa Wilaya, tumeandaa mradi wa kuendeleza kilimo ili upelekwe mbele ya safari kuombewa fedha.

Kwa kweli lazima tuwe sawa sawa na yule Bwana Shamba aliyekuwepo pale kwa bidii zake alizofanya. Sasa baada ya kufanya kazi hiyo vizuri hatua iliyofuata ni kupeleka mradi huu au maombi hayo Mkoani ili yapelekwe mbele ya safari na mwisho yapite hapa Bungeni na yapangiwe fedha ili utekelezwe ule mradi. Kilichotokea ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotokea kinastusha sana katika maombi ambayo yalipelekwa kutoka Mkoani kupeleka Makao Makuu ya Serikali Kuu, Wilaya ya Ruangwa, haikuombewa hata senti moja. Hapa ninalo jedwali ambalo nimeletewa na Ofisi yangu ya Bunge ya Ruangwa, ambayo inaonyesha maombi ya fedha zilizopelekwa Serikalini kwa ajili ya sekta ya kilimo. Kila Wilaya hapa wamepata *allocation* yao. Tunachukua kilimo kama mfano, wengine wamepata allocation yao kufika Ruangwa sifuri, no allocation. Mifugo Ruangwa no *allocation*. Ushirika tumepesta shilingi milioni mbili kwa umwagiliaji maji sifuri. Katika hali hii tutafika wapi?

Wilaya ya Ruangwa ni moja ya Wilaya katika Mkoa wa Lindi ambayo inazalisha mahindi mengi. Watu wa Mtwara wanajua hili kwa sababu sasa hivi wako pale wanununa mahindi yale kidogo tuliyonayo, katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Wilaya ya Ruangwa ndio mzalishaji mkuu wa mazao ya mboga mboga, nyanya, vitunguu na kadhalika. Mazao haya yanazalishwa chini ya kilimo cha umwagiliaji, siyo *irrigation* ya mifereji, lakini ni *irrigation* ile ya kunywesha kwa ndoo ambayo inataka kuwe na mtandao wa *shallows*.

Sasa, nashangaa hapa hakuna hata senti moja iliyoombwa kwa ajili ya Wilaya hii! Hii Wilaya itaendelea vipi? Ni nani tunatakiwa tumshike mkono ambaye hakupeleka haya maombi? Ninaomba Serikali imtafute huyo mtu ambaye hakupeleka maombi ya Wilaya ya Ruangwa huko kunakotakikana na kwa maana hiyo kuikosesha Wilaya ya Ruangwa *share* yake ya maendeleo katika mwaka wa 2003/2004. *It is a very serious thing*, kwa sababu bila msaada huu, Wilaya itazidi kuditidimia chini kimaendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa uchungu sana, ninaomba wahusika watafutwe na wachukuliwe hatua, lakini wakati kazi hiyo inafanywa, naomba Serikali itoe *allocation* ambayo haistahiki kwa Wilaya ya Ruangwa katika Sekta ya Kilimo.

Hizo *figures* ziko mahali fulani, wazitafute huko wazipate ili tupate fedha na sisi tuweze kutekeleza mipango yetu ya kilimo, ambapo msimu wa kilimo kwetu unaanza mwezi wa tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, sikuwa na mengi ya kuzungumzia ila ni tatizo hilo tu. Pia, nitapenda kufahamishwa na Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, lakini najua wahusika ni zaidi ya Wizara moja, ndani yake kuna Wizara ya Kilimo na Chakula na TAMISEMI, wote hao wamehusika katika kuhujumu maendeleo ya Wilaya ya Ruangwa kwa kutokuipa *allocation* ya fedha kwa ajili ya kuendeleza kilimo ambacho ndicho uti wa mgongo wa maendeleo ya Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, naunga mkono hoja hii na sina haja ya kuipinga, lakini nataka haya yafanywe ili na sisi tunapokwenda nyumbani, tukafanye kazi ya kujenga nchi yetu kama inavyotakikana na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika Wizara hii ya Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kwanza katika nchi hii ni udogo wa mishahara kwani mishahara hiyo haikidhi haja za Watumishi Serikalini. Mtumishi anashindwa kuwa hata na uwezo wa chumba cha kupanga, wengine inabidi wapange wawili wawili, kitu ambacho kwa kweli kwa mtu ambaye ana kazi yake halafu anashindwa kuhudumiwa na ule mshahara wa kawaida siyo kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano katika Jiji la Dar es Salaam, ukifanya hesabu ya nauli ya basi inakuwa ni kubwa kuliko hata huo mshahara wenyewe. Kwa kumpa mtumishi mshahara mdogo, unamtamanisha kufanya jambo lingine la *shortcut* ili aweze kupata fedha nyingine za matumizi. Kwa hiyo, Serikali ijithadi kuwapa mshahara mizuri ili wasiwe na *shortcut* ambazo si nzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo napenda kuzungumzia hapa ni kutoa sifa kwa Wanawake. Wanawake wana uwezo sana, kwani tukiangalia Wanawake amba wanashikilia Wizara, mfano hii Wizara ya Utumishi na Wizara ya Afya, utakuta kwamba zinaendeshwa vizuri kwa sababu zinaongozwa na Wanawake. (*Kicheko/Makofî*)

**MBUNGE FULANI:** Anasifia tena Wanawake!

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Uwezo wa Wanawake siyo kwa Tanzania tu, kwani hata Uingereza wamegundua kwamba mwanamke ukimpa nafasi anakuwa na uwezo zaidi kuliko hata mwanaume! (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, kuhusu ajira katika sehemu mbalimbali kuanzia humu Bungeni, ma-DC na Watumishi wote Viongozi kama amekwishafikia lengo hilo la 30% kwa Wanawake. Tunatamani hata iwe 40% kwa sababu ni Watumishi bora. Kwa hiyo, wakati wa majumuisho ningeomba nijue hilo kama hiyo 30% imekwishafikiwa. (*Makofî/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Mwambie bado anayo.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisemi mambo ya mzaha kama watu wanavyofikiria hapa! Tunao ushahidi, Betty Mkwaswa wa *ITV* ameshindanishwa katika Afrika nzima na ameshinda, amepata zawadi. Hapa siyo kwamba natania, kuna watu amba wamepata sifa na wameweza kumudu kazi zao. Tatizo ni kwamba hatuwapi hawa akinamama nafasi. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya pili ni kwamba, kati ya Wabunge 13 Wanawake walioshindanishwa, ni mmoja tu ameshindwa. Kwa hiyo, tuwape nafasi hata hizi za kushindanishwa, watashinda. Kwa hiyo, tuwape nafasi hawa akinamama watafanya vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuzungumzia kuhusu ajira. Ajira inaleta matatizo sana na inakosesha matumaini. Kwa mfano, wanafunzi wanaomaliza Chuo Kikuu halafu wanarudi nyumbani, eti hakuna kazi, lakini utaona kwamba walipata elimu ndani ya Tanzania na wametumia gharama kubwa sana katika masomo!

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwuliza Waziri wa Utumishi, hawa watu tumewafundisha mpaka wakafikia viwango hivyo kwa sababu gani, ili waende nyumbani wakalime au wakafanye kazi nyingine za ujambazi? Hao si watu wetu amba tunategemea wafanye kazi za umma! Tuache haya mambo ya kuwapa watu kazi za mikataba, ili vijana wetu wapate nafasi. Kuna wakati mwingine niliambiwa kwamba: "Aah, huyu ni kijana sana, hawezি kushika madaraka." Lakini hebu tukumbuke, Mheshimiwa Salim Ahmed Salim alichukua madaraka akiwa na miaka mingapi?

**MBUNGE FULANI:** Ishirini na mbili.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Alichukua madaraka akiwa na miaka ishirini na mbili! Kijana kabisa, amechukua madaraka ya Ubalozi, Uwaziri na kadhalika. Sasa, leo hii ni kwa nini hawa vijana wetu tunaona hawawezi, eti kwa sababu ni wadogo! Suala hili naona ni la kutilia mkazo. Napenda Mheshimiwa Waziri anifahamishe vizuri, hawa vijana wetu tunaowasomesha wanafika *form six*, wanamaliza shule na tena wanasona vizuri na wanafaulu, wanapataje ajira ndani ya nchi hii ili damu changa ijenge nchi hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, hao wa *University* ambao kwa kweli nilishuhudia mwenyewe wakilia, unakuta mtu ana *masters* yake na *degree* yake anayo mfukoni, anakwenda Kijijini kukaa bila kazi. Wengine tumeomba wanajaribu kupita pita kwenye Shule hizi za *Primary* au za *Secondary* wasaidie saidie labda *partly job*. Lakini sasa watapata wapi yale matumaini walijokuwa wanategemea, kwamba sasa nimesoma, ili niweze kufanya kazi vizuri! Naomba Wizara hii, ifanye kazi yake kama Wizara, wanafunzi wa Chuo Kikuu wanapomaliza masomo yao wote wapate kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, wengine niliwaona kwenye utafiti, nilikuwa naongea nao katika utafiti kwa upande wa kilimo, wamekwsenda huko Kusini kufanya kazi. Watanzania wengi wenye uwezo wanafanya kazi nje ya Tanzania na sisi tunawaacha tu, tunabaki na wale wakongwe wakifanya kazi na wengine tunawapa mikataba, badala ya kuajiri hawa vijana damu mpya waweze kutufanya kazi! Naomba kabisa asitoke kijana Chuo Kikuu akaenda nyumbani eti hana kazi!

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu upendeleo katika Utawala Bora. Katika suala hili kuna vyeo ambavyo siyo vya kisiasa, mfano kuwa Mjumbe wa Bodii, kuna watu wenye uwezo na wapo Upinzani. Sasa tusiingize Siasa humo, tuwape na watu wengine kazi wafanye kama wana uwezo bila kujali Itikadi. Pia, hili jambo la kusema eti Watumishi wasiwe na Chama chochote cha Siasa siyo zuri. Sasa kama wafanyakazi wote nchi nzima hawatakuwa na Chama chochote cha Siasa, ni watu gani mnapenda wawe na Vyama? Ukienda maofisini unaambiwa: “Bwana, hapa tunakatazwa kuwa na Chama.” Mtu akionwa na kadi ya CCM haulizwi, lakini akiwa na kadi ya Upinzani matatizo. Naomba suala hili liwe na usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Siasa maana yake ni shughuli na utendaji wa kila siku. Nasikia watu wanaambiwa: “Nyie mashulenii msifanye siasa,” hapana, Siasa kwanza tuijue, halafu ndiyo tuseme: “Msifanye Siasa.” Kwa hiyo, Siasa ifundishwe mashulenii na vile vile, kwenye maofisi waruhusiwe kuijunga kwenye Vyama wanavyotaka ili mradi wasiharibu utaratibu au muundo wa kazi.

Yaani wasiende nje na nia ya kazi zao, wasifanye vitu vingine ambavyo labda kazi yao hajjawatuma. Watumie tu utaratibu wa kazi na wafanye kazi yao vizuri. Ninaomba pia hii Elimu ya Uraia, ifundishwe nchi nzima ili Wananchi wajue haki zao, nayo ni katika Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maana kwamba Siasa ifundishwe kuanzia *Primary School* mpaka *University* na wajue Siasa maana yake ni nini. Isiwe ni wimbo, iwe ni kama somo mojawapo kwa sababu ni changamoto, *otherwise* tutaishia hivi hivi tu. Sasa hivi watu wa miaka 40 wanaambiwa: “Nyie bado ni vijana, hamuwezi kuchukua madaraka” eti kwa sababu hawakufundishwa Siasa wakiwa shulenii! Sasa huyu Salim Ahmed Salim, ambaye alichukua madaraka akiwa na miaka 22 ye ye ali soma wapi au labda alizaliwa tofauti? Hakuzaliwa tofauti, kwa hiyo, tuwape watu uwezo wa kufanya hivyo vitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tulikuwa tunazungumza katika ubishani wa ucheshi hapa Bungeni kuhusu masuala ya akinamama na kadhalika, kuna wengine waliona nimewaudhi, naomba radhi kwa wale ambao wanaona kwamba niliwaudhi. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kumpongeza Waziri wa Utumishi kwa sababu amekuwa kwenye Wizara hiyo kwa muda mrefu. Napenda kumwambia kwamba, hayo niliyoyasema ni ya msingi sana na nitafuatilia utendaji wake na ninaomba katika majumuisho anijibu. Pia, Waziri wa Utawala Bora yupo pale na ananisikia, ninaamini kwamba haya niliyosema atayatilia maanani na nitaendelea kumpa ushauri zaidi. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Dr. Nagu na Mheshimiwa Masilingi, Mawaziri wa Nchi katika hii Ofisi, pamoja na watendaji wao wote kwa hotuba nzuri na Bajeti nzuri ambayo wameitayarisha na malengo yake yamekuwa dhahiri na yanaeleweka katika hotuba hiyo. Nawapongeza sana. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba, ninaunga mkono Bajeti ya Wizara hii kwa asilimia mia moja. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba, pamoja na kuwa inawezekana kweli huwezi kumfundisha mbwa mzee njia mpya za kukamata sungura, lakini na sisi Waafrika tuna usemi wetu wa kusema kwamba, uzee ni dawa na huenda ikawa ndiyo sababu Chama cha Mapinduzi, kwa uzee wake kimeweza kuongoza vizuri nchi hii kwa miaka 40. Huwezi kumkabidhi mbwa mtoto majukumu ya kulinda wakati hajui ukali wa simba, atamfuata na simba atamuua! (*Makofsi*)

**MBUNGE FULANI:** Mapigo hayo! (*Kicheko*)

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea kidogo kuhusu rushwa. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameleeza kwamba, katika kuendeleza vita dhidi ya rushwa, utafiti utaendelea kufanywa katika kubaini mianya ya rushwa ili waweze kupata mapendekezo namna ya kuiziba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba CCM na Serikali yake, imeshinda kwa *platform* ya kupigana vita dhidi ya rushwa. CCM na Serikali yake inatambua kwamba rushwa ni tatizo katika nchi hii na ni wazi kwamba, hiyo mianya na sababu ya rushwa vinafahamika. Kusema kwamba leo hii tutakaa tufanye utafiti juu ya mianya na vyanzo vya rushwa, kwa kweli tutakuwa tunajidanganya, tutakuwa tunapiga siasa, hatufanyi kazi katika nchi hii. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mtu ambaye hajui kwamba kipato cha mtumishi wa Serikali hapa Tanzania ni duni kiasi kwamba ukweli tunafanyia kazi uzalendo na siyo kipato. Ni ukweli kwamba, ukimkabidhi mtu jukumu la kusimamia mradi wa mamilioni ya pesa, huku unampa mshahara ambao hautoshi kwa wiki moja, ni lazima atapata kishawishi cha *ku-supplement* kipato chake, hasa ukizingatia kwamba sisi hatuko kama wenzetu wa huko Ulaya, amba ni yeche, mke wake na mtoto mmoja. Sisi tunabeba ukoo na katika kubeba ukoo majukumu yetu ni makubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka mingi sana ile *habit* ambayo tulikuwa tunangojea *May Day* tutangaziwe hata nyongeza ya mshahara ya Sh.100/= kwenye mishahara yetu haipo! Kweli nakubali tunalo tatizo la pesa, lakini kuna matumizi mengine ikiwa yatapunguzwa, mfanyakazi wa Serikali anaweza akaongezewa mshahara. Tujaribu kufikiria namna ya kupunguza yale matumizi ambayo siyo muhimu, tuwakwamue hawa Watumishi wa Serikali kutoka hiyo sehemu. Huenda ikawa tunawalaumu, lakini tumewalazimisha wawe hivyo! (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nani ambaye hajui kwamba kuna hali duni sana katika Utumishi wa Umma? Twende tukaangalie katika maofisi yao huko waliko, twende tukaangalie vitu wanavyopewa maofisini, havitoshi ni lazima kuwe na vishawishi. Naomba hiyo pesa itakayotumika katika kufanya utafiti wa mianya ya rushwa, Mheshimiwa Warioba, alikwishatuambia hizo rushwa zinapatikana wapi, tufuatilie ile ripoti ya Mheshimiwa Warioba na tutekeleze yaliyosemwa. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubali kwamba rushwa ni kama usherati, ni jambo linalofanyika kwa siri na ni vigumu kugundua, lakini njia ya kuizuia ni kuanza kuwawezesha hawa ambao wanashawishika kupokea rushwa, mfano mtu anasema: “Mzee sijanywa chai.” Mtu huyu aweze kunywa chai kwanza kwa kujitegemea yeche mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuna jambo kubwa sana ambalo nafikiri ni lazima tulielewe, hii *Regulatory System* yetu, kila kukicha kunatolewa tamko: "Tangu leo iwe hivi." Ni kweli kulikuwa na Sheria ya saa za kufungua na kufunga baa na hajafutwa, lakini kwa kutambua kwamba ilikuwa imepitwa na wakati, Serikali ikafumba macho kidogo, lakini tamko lilitolewa juzi tayari limeshafungua mwanya mwingine wa rushwa. (*Makofsi*)

Pale Dar es salaam ikifika saa tano kamili, sasa Polisi anapita, siyo kulinda majambazi, bali ni kuvizia mtu anayemalizia bia yake moja baa, ili achukue rushwa! Sasa, matamko mengine ambayo tunatoa yanatupa zaidi mianya ya rushwa. Tu-*address* haya matatizo kwenye *traffic*, kwenye hizi Sheria ndogo ndogo ambazo kwa kweli zimepitwa na wakati na kwenye maslahi ya wafanyakazi wetu. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo jingine ambalo linapigwa kelele nalo ni juu ya kuwajibika, mtu anatajwa kwamba ni mla rushwa anaambiwa wajibika. Nilifikiri sisi kama Wabunge tumeshaelewa wazi kwamba, nchi yetu ikiongozwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inaongozwa kwa Utawala wa Sheria na Utawala wa Sheria inatakiwa mtu ahakishwe kwamba anayo tuhuma nzito ndiyo awajibishwe. Maneno ya kwenye majukwaa kwa sababu za kisiasa au maneno ya mahali popote kwa sababu tu mtu anamchukia, yakifanya mtu awajibishwe matokeo yake ni kwamba, tunaweza tukawa katika kusawazisha migogoro yetu ndani au nje tunakosa utumishi wa watu amba ni muhimu kwa kupiga kelele za kisiasa kwamba watu wawajibishwe. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono ule msimamo kwamba, ikiwa kuna tuhuma halali ya rushwa huyo mtu awajibishwe, lakini ikiwa ni tuhuma ambayo inatoka kwenye jukwaa la Siasa tu bila ushahidi, mfano wakinitangaza leo hii kwamba nina nyumba tuseme Mwanza, hakuna ushahidi wa ile nyumba na anajitokeza mtu anasema hapana, hiyo nyumba siyo ya Lamwai, ni nyumba yangu, sasa niwijibike kwa nini! Wabunge tuisitumiwe katika kuleta migogoro ya kisiasa ndani ya nchi yetu. Huyo anayesimama kwenye jukwaa la Siasa huko nje anajiteeta kwamba ni Mwanasiasia anaendesha Siasa dhidi ya Chama cha Mapinduzi na kutuhumu Viongozi, atoe ushahidi na athibitishe, *PCB* ifanye kazi. Lakini hatuwezi kupoteza pesa na wala hatuwezi kupoteza Viongozi wetu kwa ajili ya tuhuma tu na ni tuhuma za kisiasa. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, amefanya kazi nzuri sana, Serikali yake ya Maaskari wa Miavuli wamefanya kazi kubwa, japo kuna kasoro hatuzikatai, ni Serikali ya binadamu, siyo Serikali ya Miungu, hayo matatizo huenda ikawa siyo ya rushwa, lakini hao wanaotaka kuingia ndani ya Serikali kwa kuongea juu ya rushwa zilizopo, angalia kibanzi kilicho kwenye jicho lako kabla hujaangalia kibanzi kwa mwenzako! (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala lingine kuhusu Watumishi. Hakuna mtu hapa ndani ya Bunge ambaye hajapitia mikononi mwa Walimu. Wote hapa tumepitia mikononi mwa Walimu, lakini siyo Tanzania tu, hii kada ya Walimu katika Watumishi wa umma ni kada inayoonewa mahali popote duniani. Kazi yetu ni kuwasaidia Walimu ili wawewe kuwa na hali nzuri kidogo. Wapo Walimu, kwa mfano, kwa rafiki yangu kule Rufiji, ambao ukiwaona wanavuka zile *delta* utasikitika kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sasa hivi pale Dar es Salaam, kwa sababu ya wingi wa wanafunzi kuna *shift* mbili. Wanafanya kazi asubuhi na mchana. Mwalimu anafanya kazi kwa zaidi ya saa 10, yet tunaambiwa kwamba ualimu ni saa 24, kwa hiyo asipate kipato cha ziada. Kama hamna *overtime*, basi ichukuliwe kuwa ni *special cadre*, wapewe mshahara amba ni tofauti na watu wengine, lakini tukitegemea uzalendo wao, baada ya miaka 20 tutakuwa hatuna Viongozi katika nchi hii. Walimu watakuwa wanafanya kazi shingo upande kiasi kwamba watasikika wanapiga makelele darasani kwa saa 10, lakini hawatakuwa wanafundisha, *output* itakuwa *nil*. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa ujumla waifikirie sana kada hiyo, kama hamuipi *overtime*, ipeni mshahara wa kutosha. Pia kuna *complaints*, Walimu hawapati pesa zao za likizo na hawapati mafao yao mengine. Yanakwenda wapi wakati Serikali Kuu inatoa? Vile vile, hawapati fedha zao za uhamisho, ni kwa nini Walimu wawe wanaonewa muda wote huu? Naomba hayo yafikiriwe. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, hivi ile kada ya *trainees* katika Serikali imekwenda wapi na je, Serikali haioni kwamba hiyo ndiyo ilikuwa njia ya *ku-absorb* hawa watu wanaomaliza Shule tayari kurithi wale watu wanao-retire? Lakini sasa ukitangaza kwamba eti unataka *experience* ya miaka mitano ili umuajiri mtu, hiyo *experience* ataipata wapi kama hajakaa kama *trainee*? Ni kwa nini hiyo kada ya *trainee* isiwepo, ili yule mtu miaka mitano itakapofika awe ameshapata *experience*? Sasa hivi tuna jeshi kubwa sana la watu ambao hawana kazi na hawatapata *experience*, kwa maana hiyo, hawataajiriwa kabisa. Naomba hiyo kada irudi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo, machache narudia tena kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha asubuhi. Kama tulivyofanya jana, wachangiaji wanne watapata nafasi mchana, halafu tutawapa nafasi watoa hoja ili waweze kuendelea. Tutakapofika ataanza Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga.

Baada ya hayo, sasa nasitisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipatia fursa hii na mimi niweze kuchangia katika hoja ya Ofisi ya Rais, Utumishi pamoja na Utawala Bora. Kwanza kabisa napenda kusema kwamba ninaunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli dhana ya Utumishi na Utawala Bora ni dhana ambayo tunajifunza na ni dhana ambayo ni *dynamic* kwa hiyo sina budi kuwapongeza Mawaziri wote Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Waziri wa Nchi, Utawala Bora, Mheshimiwa Wilson Masilingi, kwamba kwa pamoja wameiandaa hotuba hii kwa kuzingatia wakati uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wengi tunapata kigugumizi sana na hasa ukitaka kuelewa *concept* ya Utumishi na Utawala Bora. Utumishi kama ulivyo ni kuona maslahi ya Watumishi wa Serikali, maslahi ya watumishi wa umma na watumishi wote kwa ujumla yanaboreshwa kulingana na matakwa ya sera ya nchi. Kwa kweli napenda nipongeze jitihada za Wizara hii na hasa kwa kuanza na mikakati ya nguvu pamoja na mikataba ya utumishi. Kwa kweli *the hard way* nakumbuka ni kwamba tumetoka katika uchumi hodhi sasa hivi tuko kwenye uchumi huria ambao tunahitaji mambo mengi yabadilike kulingana na mahitaji yenye ya soko yanakwendaje.

Lakini si vibaya na mimi nijaribu kugusia kidogo pamoja na mikakati hii ni nini kizingatiwe zaidi kwa sababu unaposema kwamba tuko katika *Civil Service Reform* nategemea kwamba Watumishi wa Serikali hawatalalamika kutokupandishwa vyeo vyao, hawatalalamika kwa kuwa na mishahara midogo, hawatalalamika wasataafu kutolipwa pensheni kwa muda unaostahili, hawatalalamika watumishi wa umma watajivuna kwamba utumishi wa umma ni ajira yenye heshima na kwamba ina hadhi kubwa sana. Hivyo mtumishi anapaswa kujiona kwamba anapaswa kuridhika na kazi yake. Kwa maana hiyo ni kwamba kipato anachokipata kinaoana na ajira na kinaoana na maisha ya kawaida ya mtumishi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutokana na matatizo ndiyo hapo sasa dhana ya utawala bora inapoingia. Tunaposema rushwa ni mdudu mbaya sana, kuna mikakati ya kumwangamiza mdudu huyu? Lakini hawezi kuondolewa kwa sababu ya mikakati isiyokuwa na utekezaji wake. Hivi kweli tukianza kuangalia watumishi katika nchi hii, kipato ambacho wanachokipata kwa kweli hakioani na maisha yao ya kila siku. Hawa watumishi watajikimu vipi ili waweze kukidhi mahitaji ya msingi katika jamii zao na katika kuendesha maisha yao ya kila siku? Nadhani hapa msingi unaopaswa kuangalia hapa ni kwa namma

gani huyu mtumishi sasa anajengewa mazingira yatakayomsaidia aweze kuboresha maisha yake yeze pamoja na familia yake. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kiwango cha mishahara hiki kinapaswa kitathiminiwe vizuri kiendane vile vile na mfumo wa soko. Hivi inakuwaje leo hii Watumishi wa Idara za Serikali au mamlaka za Serikali kwa mfano kama walianza na Benki Kuu wakaanza kulipa mishahara mizuri kwa sababu wanazalisha, tuna wafanyakazi wa *TRA* wanalipwa vizuri kwa sababu wanazalisha. Lakini Mtumishi wa Serikali yeze anabaki kwenye *range* ya 50 na mshahara ambao kwa kweli ukizingatia haumtimizii mahitaji yake ya kila siku, madhara yake ni kwamba aidha hatafanya kazi vizuri ya Serikali ili akafanye kazi nyingine ya kumwongezea kipato kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake ya kila siku na hii ni kuibidia Serikali muda wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda niwasifu sana Mawaziri hawa. Sasa hivi tunakuwa tunawamulika wote. Utasema kuna *corruption*, kuna utumishi mambo hayaendi vizuri lakini tukubali kwamba zile *processes* zimeanza, hawa watu wameanza hawana muda mrefu lakini tunaona mikakati yao inakwenda vizuri.

Mwaka 2002 wakati wanasoma hotuba yao hapa walihidi vitu vingi sana ambavyo vinapaswa kufanyiwa utekelezaji badala ya kuwa katika muundo au katika sura ya mikakati. Mimi nadhani ni vema zaidi sasa hili suala la kusema tunajaribu kuangalia limepitwa na wakati. Ukianzia na upande wa rushwa Tume ya Jaji, Francis Nyalali, ilainisha mambo mengi sana mazuri sana. Lakini ni watu wangapi leo hii wamekamatwa na rushwa? Kama siyo wachache ambao tumewasikia tu na baadaye kesi zinaishia Mahakamani na kesi zinafutwa. Unakuta kama ni rushwa wengi wanaoangamizwa ni wale Mahakimu wanapokeea shilingi 2,000, 3,000/= lakini kweli *are we serious* kwamba tuna-fight against corruption? Mimi nadhani ingekuwa ni msingi mzuri sana tupate movement ambayo ni kweli iko faithfully na ambayo itasaidia kujua kwamba kama mtu anahusika katika rushwa basi aadhibiwe kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa *PCB* mimi naona kuna haja uangalie upya kwa sababu ni chombo cha Serikali. Serikali ndiyo watumishi ambao wanatuhumiwa wanakula rushwa. Sasa ni nani atamshitaki mwenzake? Kwa sababu wakati mwininge inakuwa ni vigumu sana kama pengine kuna Mtumishi wa Serikali wa ngazi fulani ambaye anatuhumiwa katika rushwa na chombo hiki hakiwezi kumchunguza inabakia ni hadithi za kubadilisha *statement* mara ohoo, tulisema hivi hapana, hii ndiyo sahihi. Mimi nadhani hiki chombo kingefanywa zaidi kuwa na makucha ya kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuangalia Wizara hizo mimi narudi kwenye mradi wa *TASAF*. Kama Serikali hii imefanya mambo mazuri ni katika kukopa pesa kwa ajili ya miradi ya *TASAF*. Tumekuwa sasa hivi tunabebeshwa deni kubwa sana ambalo limekopwa huko nyuma bila wananchi kushirikishwa, lakini sasa tunalilipa kwa kushirikishwa na kwa kweli mradi wa *TASAF* mkopo kutoka Benki ya Dunia, ni dhahiri kabisa kwamba sasa wananchi wanajua ni nini wanakitaka na nini wanachoweza kukipata ndani ya mradi wa *TASAF*. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na miradi miwili ambayo tumeikopa, kuna mradi wa MMEM na mradi wa *TASAF*. Ukienda vijijini *the difference is very clear* kwa sababu moja umeshirikisha wananchi moja kwa moja na mwininge ulifanywa kwa msukumo kutoka Wilayani. Sasa hii imeleta utofauti wa miradi hii katika kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani dhana hii ya kufanya *Participatory Rural Appraisal (PRA)* imesaidia sana kuweza ku-sensitize wananchi wao wenyeve kuweza kuibua miradi yao na kulingana na vigezo vyao vya kuweza kupewa priorities zao. Hii imesaidia sana na ndiyo ilikuwa mbinu shirikishi na kupata support ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwamba Waheshimiwa Wabunge, ambao hawana miradi ya *TASAF* wanaona kama ni nadharia tu, lakini mimi naomba ni-declare interest niseme kwamba mimi ni beneficiary wa mradi wa *TASAF*. Wale wote ambao miradi ya *TASAF* kwa kweli iko katika Wilaya zao ni mashahidi wa uhakika kabisa. (*Makofit*)

Juzi hapa tulikuwa na *mid term review* ya *World Bank* kwa kweli wale watu wa *World Bank* wanasema hatujawahi kuona mradi unafanikiwa namna hii. Kulikuwa na watu kutoka Masafu - Malawi ambao wao wameshakwenda *stage* kubwa zaidi ya mradi wa *TASAF* walikiri kwamba Tanzania mmeweza *ku-implement at a very high degree stage* kuliko wao Malawi. Hii sasa mimi napenda niupongeze uongozi wa *TASAF* kwa kweli umefanya kazi nzuri sana, lazima tuwapongeze jamani tuwapigie makofi walau. (*Makofi*)

Mtu akifanya kazi nzuri lazima apongezwe. Maana hata Pemba nimefika nimekuta *TASAF* inafanya kazi. Sasa hebu niambie kweli katika maslahi ya nchi iwapo pesa zinakopwa na halafu zinapelekwa kwa wananchi wao wenyewe hata wangesema tulipe kwa namna gani tutalipa bila tatizo. Lakini hii ya kukopa wananchi bila kushirikishwa hamuoni pesa zinakwenda wapi, zinapotea huko ndiyo mambo ya *corruption* yanaingia ndiyo *PCB* wanafanya kazi lakini kazi hatuioni wakati mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naipongeza kwa dhati sana *TASAF*. *TASAF* katika Wilaya yangu ya Magu wamefanya mambo mengi sana. Tuna miradi ya jamii, tuna miradi ya ujenzi na ninaomba iendeleee. Kingine kwa Waheshimiwa Wabunge, nataka niwaombe kwamba tuombee *TASAF TWO* iweze *ku-take place immediately*. Huyu ndiyo mkombozi wetu sisi wananchi na sisi kama Waheshimiwa Wabunge. Ninaamini kwamba hata katika Jimbo lako la uchaguzi kama kuna kigugumizi gugumizi cha sura ya hili na lile, ukiwa na *TASAF* umesafisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda niupongeze sana hiyo. Lakini vile vile napenda nizungumzie kuhusu suala la ubinafsishaji. Watanzania wengi walitegemea sana kwamba katika kubinafsishaji mashirika yetu tungeweza kupata kazi nydingi kwa vijana.

Vile vile katika *Reform Sector* tunasema kwamba Serikali inabakiza wafanyakazi wachache ambao ingeweza kuwashudumia kwa karibu zaidi kwa kuweza kuwalipa mishahara mizuri na kuwapatia malipo ambayo tunaweza kuwasaidia kinyume na kuwa na wafanyakazi wengi. Sasa hivi Serikali ina wafanyakazi zaidi ya 250,000 ni namba ambayo siyo kubwa sana. Lakini kwa nini sasa Wizara isifanye mkakati wa makusudi kuwashudumia hawa?

Mimi nategemea kwamba mfanyakazi angalau kila mwaka anajua kwamba kima cha mshahara kinaongezeka kadri maisha yanavyozidi kupanda. Lakini wafanyakazi wa Serikali wamekaa kwa miaka mingi sana kwa mishahara kidogo. Mimi naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, nina imani kwamba mwaka ujao utakapoleta Bajeti yako ningependa kusikia kwamba wafanyakazi sasa wanalipa mishahara kulingana na uwezo wa kuishi kwa muda wa mwezi mmoja. Kwa sababu haina maana kuwa tunawadanganya watumishi kwamba Serikali inawalipa inawajali, inawajali viyi kama mtu hakujali tumboni nani anayekujali zaidi jamani?

Mimi nadhani anayekujali zaidi ni yule ambaye anahakikisha kwamba angalau zile *welfare* zako na maisha yako ya kila siku yamekuwa *taken care*. Hili tutaelwa zaidi tunaposema kwamba kuna *clients service charter*, tutakuelewa zaidi Mheshimiwa Waziri. Lakini kwa watumishi inakuwa ni vigumu sana kuelewa kwa sababu toka tumeanza mkakati huu hawawezi kupata *a tangible benefit* kutokana na mikakati hiyo. Kwa hiyo, naona sana hili tuweze kulifanya. (*Makofi*)

Mwisho napenda kumpongeza Mheshimiwa Wilson Masilingi, kwa Utawala Bora kuititia kitengo chake cha *PCB* kwa sababu ni mmoja kati ya Mawaziri ambao wanapata kazi kubwa sana hata humu Bungeni kwa sababu Wizara yako ni nyeti. Unaposema kwamba suala la rushwa ni kama ngono, sasa ngono nani anaweza kuithibitisha? Ni tatizo. (*Makofi*)

Sasa Mheshimiwa Wilson Masilingi, nakupa pongezi kubwa sana, endelea na uzi huo huo kuimarisha majeshi yako na kwa kweli *PCB* imekwenda mpaka Wilayani mpaka Magu siku hizi kuna *PCB*. Juzi juzi hapa nimesikia kuna watu wamekamatwa. Lakini hii angalau wananchi wanaona kwamba kweli *PCB* inashuka chini. Sasa cha maana muwe na uwezo wa kuweza kufuutilia rushwa, ifuatiliwe na wananchi waonee kwamba kuna matokeo ya namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi kama wananchi hawataona matokeo wataanza kusema ahaa, Mheshimiwa Wilson Masilingi, hapa anachemsha. Sisi hatutaki uchemshe Mheshimiwa Waziri, tunataka ufanye kazi hasa na wataona mafanikio. Tena una *Major General* anaitwa Kamazima. Sasa watu kama hawa tunataka tuone kazi yao nzuri. Una vijana wazuri kama akina Hosea wana historia nzuri sana. Lakini tusione uzuri wa watu tu tunataka tuone uchapaji kazi amba unaboresha na kusaidia nchi yetu. Tumsaidie Mheshimiwa Rais, kama Serikali tunaomba msaidieni sana kwa sababu yeze ana imani kwamba hii vita tutapigana sisi Watanzania kwa pamoja na hakuna jinsi yoyote ile. Sidhani kwamba kuna mtu peke yake anawenza kupigana vita namna hii isipokuwa ni sisi *collectively*. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiseme sana. Kwa vile ni dakika kama tano nimezungumza zinatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. (*Makofsi*)

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwenye hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma. Suala langu lingekwenda kwenye Wizara ya Afya lakini sikupata nafasi ya kuchangia. Lakini kwa kuwa linahusu ajira naona hapa itakuwa sehemu muafaka pa kuleta kero hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero yangu inahusu hospitali teuli ya Jimboni kwangu Ifakara. Nadhani itahusu pia hospitali zingine Teule hapa nchini. Serikali iliingia mikataba na Mashirika ya Kikanisa ili kuteua hospitali zingine ziwe hospitali teule. Lakini kwenye taratibu ya ajira nadhani kulikuwa na matabaka mawili ya ulipaji mishahara. Mishahara ya wale watu amba wamekuwa *seconded* na Wizara mara nyingi mishahara yao ilikuwa bora zaidi kuliko wale amba walirithiwa kwenye hizo hospitali za Mashirika hayo kama Jimboni kwangu Dayosisi ya Mahenge, amba mwajiri wao alikuwa Mhashamu Askofu. Sasa tofauti yenye ni kuwa watu wenye ujuzi sawa, stashahada sawa, lakini mishahara wanatofautiana ingawaje wote wanafanya kazi kwenye mazingira ambayo yanafanana.

Sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri kwa wadhifa wake kuwashughulikia watumishi ungeliangalia hilo ili usawa wa mishahara na marupurupu yafanane. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba kuchangia kwenye upande huo huo ni juu ya wadhifa wa hiyo hospitali kuwa hospitali teuli. Kwa sababu imetuwa ni teule inahudumia majimbo mengi ya jirani. Hospitali ya Ifakara ilianza mwaka 1927 ikiwa na vitanda 27 tu. Sasa hivi ina vitanda 371 lakini Hospitali ya Ifakara ina daktari *consultant* mmoja tu.

Kwa hiyo, namwombwa Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano kwa mujibu wa hotuba yake Ibara ya 28 na 34 atafute kuwapa kibali hawa ili waweze kuajiri wafanyakazi. Siyo upungufu kwenye *consultant* peke yake bali hata madaktari na wauguzi. Naomba hilo aliangalie ili kero ipungue Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linahusu kulipa kufuatana na taaluma. Hospitali ya *St. Francis* pia ina chuo cha kufundisha *Medical Assistants* katika kufundisha pale watu wengine wenye daraja la ualimu tofauti kabisa na walimu kwenye idara ya kawaida ya Elimu na Utamaduni wengi hawa walimu wa taaluma mishahara yao bado ni midogo kabisa na hali ya chini. Kwa hiyo, naomba waangaliwe pia kuboreshwa kwa hiyo mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya haya nadhani sina zaidi la kuchangia ila tu naomba pindi itakapowezekana Serikali iweze kuangalia upya mkataba ule wa awali ulioingia na mashirika hayo ili usawa utolewe kwa wafanyakazi wote kwa sababu wote ni wananchi, mahitaji yao ni sawa na kwa kuwa wana taaluma sawa hakuna sababu ya malipo kutofautiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante. (*Makofsi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, kwanza niwapongeze Mawaziri wote wawili kwa pamoja kuweza kuandaa hotuba hii na wakawenza kutuwasilishia asubuhi ya leo. Ni Wizara muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu.

Naomba Waheshimiwa Mawaziri wote wawili wakumbuke kwamba mwaka 2001 tuliingia kwenye muafaka baina ya Chama cha CUF na CCM. Katika muafaka huo tulikubaliana kwamba iundwe Tume ya Mheshimiwa Hashim Mbita, kuchunguza mauaji ya tarehe 26 na tarehe 27 yaliyotokea Pemba na Unguja na hata Bara. Tume hiyo ilifanya kazi nzuri sana na taarifa yake imetoka imekabidhiwa Serikali. Lakini kwa bahati mbaya mpaka sasa Serikali haijasema chochote juu ya taarifa hiyo. Lakini pili, hata wale waathirika ambao tuliahidiwa katika kamati ya muafaka kwamba wangeweza kupatiwa angalau kifuta machozi mapema iwezekanavyo mpaka leo Serikali haijachukua hatua yoyote.

Sasa kwa sababu Wizara hizi mbili ndizo zinazohusika, tungeomba kupata kauli mbili kutoka Serikalini, ya kwanza, juu ya hatua ya taarifa ya Mheshimiwa Hashim Mbita, lakini ya pili, juu ya kifuta machozi walichoahidiwa waathirika kwamba watapewa. Ni mategemeo yangu kwamba Mawaziri watakapofanya *winding up* watakuwa wametueleza mambo hayo mawili ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la ajira ya walimu wa sekondari na msingi. Juzi tulipokuwa tunazungumzia Wizara ya Elimu, tulizungumza sana suala zima la ajira ya walimu na kiwango cha elimu ambacho kinateremka. Hivi sasa kuna wastani wa walimu wawili wanakufa kila siku. Sijui kama takwimu hizo Waziri anazo lakini kwa mwaka 2001 walimu 1,020 walikuwa wamekufa kwa matatizo mbalimbali. Halafu katika walimu 1374, 400 hawakuweza kuripoti kazi, 323 waliacha kazi. Sasa sina hakika kama *replacement* inafanywa kutoka na matatizo haya yanayotokea, yanaziba mapengo katika ajira zinazofanywa kwa kila mwaka hatuna hakika hilo.

Tatu, pengine Wizara ya Utumishi haijaka kwa kina ikaangalia hasa matatizo ya walimu na namna ambavyo wanaweza walimu wakabaki kazini. Tunaona orodha kubwa ya walimu wanaoajiriwa lakini pia walimu ambao hawaripoti kwenye kazi zao taarifa hiyo bahati mbaya katika taarifa katika Waziri wa Elimu alipoleta Bajeti yake halikuwemo.

Mimi nina wasiwasi kwamba tatizo moja ambalo linakabiliwa na walimu ni viwango vidogo vyamishahara yao, marupurupu yao na maslahi yao kwa jumla. Sasa nafikiri ni vizuri kwa sababu imo katika ukurasa wa 10 hata wa taarifa kamati ya huduma za jamii, ningombwa Mheshimiwa Waziri atupatie maelezo ya kina kuhusu hili.

Nne, vile vile katika muafaka tulizungumzia suala la vyombo vyombo dola kujingiza mambo ya siasa. Bado *trained* kwa kiasi fulani hasa kwa idara zilizoko chini ya Rais, Idara ya Usalama wa Taifa, bado kwa kiwango kikubwa inajihuisha katika mambo ya chaguzi. Hili litaweza kutuletea matatizo mbele ya safari. Tulipitisha sheria na tukasema katika sheria ile kwamba wale amba wameamua kuingia kwenye siasa waje kwenye siasa. Vinginevyo wabaki kwenye vyombo na wawatendee wananchi haki kama inavyotakiwa. Kwa hiyo, bado katika idara ya usalama wa Taifa hili halijawezekana. (*Makofî*)

Nne, kama tulivyosema katika hotuba yetu kwamba wakati umefika kwa vyombo hivi sasa kuwa wazi kwa umma kwa sababu mfumo tuliotoka nao na mfumo wa sasa ni vitu viwili tofauti. Vyombo hivi sasa vinatakiwa viwe wazi angalau kwa kiasi fulani hata angalau wakuu wake wa kazi wajulikane na washirikiane na wananchi kwa sababu njia moja ya kupata taarifa ni kushirikiana na wananchi. Kila mnopojificha basi kupata taarifa nako ni kugumu sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana kazi nzuri wameifanya sijasema hawakufanya kazi nzuri, wamefanya kazi nzuri, nchi yetu imebaki kwenye amani kwa muda mrefu, tuna-*appreciate* hiyo kazi na waendelee na kufanya kazi ya kuhakikisha kwamba amani na utilivu katika nchi ipo, lakini vile vile twende na mabadiliko yanayotokea katika dunia ili tuhakikishe kwamba vyombo vyetu vinafanya kazi kutokana na mabadiliko haya yanayotokea hivi sasa. Tunalo tatizo la raslimali zetu nyingi zinachukuliwa, tunayo matatizo ya wizi unatokea mkubwa sasa hivi wa aina yake, lakini tunayo matatizo ambayo tunaambukizwa kutokana mahusiano na nchi tulizonazo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko kwenye *East African Community*, tuko kwenye SADC, keshokutwa tunaingia kwenye AU. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo yatakuwa yanatuambikiza kwa kiasi fulani kwa sababu tumewaruhusu watu kuingia kwenye mipaka yetu kinyume cha utaratibu wa zamani.

Kwa hiyo, vyombo vyetu vinatakiwa vibadilike vile vile, katika namna ya kufuatilia mambo kama haya. Kwa hiyo, mimi ningeishauri Idara ifanye mabadiliko ya kuja hata mbele ya Bunge wakazungumza

na Wabunge, vyombo vingine vinakuja, hatujapata kumwona Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa akija kuzungumza hata na Wabunge akatueleza hali ya nchi, wenzetu wanazungumza na vyombo vyao, wanakwenda wanazungumza na vyombo vikubwa kama hiki, wanaelewana, kwa hiyo, mimi nafikiri chombo kibadilike kidogo kiwe na utaratibu ambao kitakuwa karibu na viongozi na kadhalika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala zima la maadili. Nashukuru Serikali inajitahidi kupiga kelele katika suala la maadili, lakini nasema kupiga kelele ni jambo moja na kutekeleza ni jambo jingine. Tunahitaji kuwa *serious* katika utekelezaji. Maadili ya kazi zetu nyangi yameanguka, yameathirika na kila tukienda mbele ya safari maadili haya yatazidi kuanguka kwa sababu watu wanajifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikuambie *experience* moja niliyoikuta, tulikutana na vijana ambao walikamatwa kwa ajili ya kufanya ujambazi wa kutumia silaha, ni wadogo sana, miaka 14, 15, mmoja alikuwa 18 tukawauliza ninyi ni vijana wadogo sana kwa nini mnafanya ujambazi? Wakasema sasa ninyi wakubwa mnakula sisi tule wapi? Hatuna kazi, walijibu hivyo hivyo. Siku ya kwanza waliokaa gerezani nilikaa na hao vijana kama 8 walikuwa wamekamatwa Zanzibar na sihala. Wakaniambia ninyi wakubwa mnakula ,sisi wadogo tule wapi, basi tunatumia na sisi hekima zetu za kula.

Sasa hiyo ndiyo hali tuliyo nayo ni kwamba maadili yakiteremka na watoto nao wanatazama ninyi wakubwa mnafanya nini. Kwa hiyo, nasema ni vizuri tukaanza kutazama maadili vizuri ili tuwe mfano kwa vizazi vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nkipata maelezo baada ya hoja hizi basi nitaamua huko mbele ya safari. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Utumishi pamoja na Utawala Bora na Ofisi ya Rais kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake, napongeza taarifa ya Kamati ambapo mimi mwenyewe pia ni Mjumbe katika Kamati hii na pia kwa kiasi kikubwa nampongeza Waziri Kivuli wangu, Mheshimiwa Grace Kiwelu, kwa hotuba yake nzuri ambayo mimi naamini kama upande wa Serikali umeipokea na kama utaifanyia kazi vizuri kwa maslahi ya Taifa letu, itaweza kuusaidia umma wa kizazi hiki na kizazi kijacho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango mbalimbali ambayo tumekuwa tunaendelea kuipata na majibu mbalimbali ambayo tumekuwa tunaendelea kuyapata kutoka upande wa Serikali na hasa wakati wa *winding-up* za Mawaziri, inaonekana tunakwepa mojawapo ya dhana kubwa ya Utawala Bora ambayo huwa ni utamaduni wa kukubali kukosolewa. Mtu unapokuwa umekubali kukosolewa naamini inaboresha utendaji wako kwa kitu kile kile katika utendaji wako wa siku zinazokuja. Ninajua kwamba Watanzania kwa kweli ni wajuzi wa maneno. Yuko mfadhili mmoja aliwahi kuniambia kwamba nyie Watanzania leo asubuhi ukimpa mtu *imprest* ya shilingi milioni mbili kwamba aende safari Mwanza safari ikachelewa na inabidi ifanyike kesho yake asubuhi, ukimwambia arejeshe hiyo milioni moja au milioni moja nusu atatoa maelezo yanayokidhi ufafanuzi wake kwamba hela zile amezitumia na atarejesha. (*Makofî/Kicheko*)

Sasa Watanzania kwa maneno na kwa lugha na kwa kuchambua ni wazuri mno. Hakuna hoja ambayo Mtanzania anaweza akashindwa kuijibu hata iwe namna gani na anaweza kuandika ile *thesis* ya kujieleza akapata U-Profesa, akapata U-Daktari kwa mantiki ya kujieleza. Lakini ile *concept* ya utekelezaji au kutekelezeka kwa hayo yote anayoeleza inakuwa ni suala jingine. Sasa haya maneno ambayo ufanuzi ambao tumekuwa tunaupata, mwagine ni wa lugha kali kali, mwagine ni wa kujaribu ni kama wa vijembe, sisi tunasema yazungumzwe lakini iwe sehemu ya kuweza kukubali kukosolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati haya mambo yakiwa yanaendelea nilikuja kukumbuka utani wa watani wawili wakati tuko katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Profesa Jumanne Maghembe, alimwambia Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, kwamba siku moja Kimaro alipata kibarua cha kuwa kondakta na upiga debe kwenye daladala kule Dar es Salaam.

Sasa alipopelekwa na yule mjomba wake kwenye kazi hiyo Dar es Salaam, akamwandikia mwenzake Elibariki aliyebacki kule Moshi kwamba kule Dar es Salaam kuna *KNCU* nyingi. Sasa yeze ile ghorofa ya *KNCU* kuona ina ghorofa tano, kuja Dar es Salaam anaona *Kilimanjaro Hotel*, anaona nini anasema ni *KNCU* nyingi. Sasa kumbe yule mtu mwininge anaweza akamwita mshamba, lakini huyu mtu naamini ni kwa sababu alikuwa hajatembea. Wanasesma tembea uone na Wafaransa wanasesma *atagenda atimae chumba*. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwa watu ambaa ni wepesi wa kutaka kukosolewa, mara nyingi si vizuri kukimbilia lugha ya kujikinga *as a defensive mechanism*, ni kukubali kukosolewa. Mimi wakati mwininge huwa napenda kuamini kwamba mtu kile anachokifanya, kitu mtu anachokitekeleza ndio upeo wake wa hali ya juu wa kutekeleza hicho kitu na ndivyo anaamini kwamba amefanya sana.

Kama umepewa Shirika la *Air Tanzania* kuliendesha ambalo limekufa sasa hivi tukauza, ukaona linazalisha hela ya kuwalipa wafanyakazi wako tu na nyingine inabaki deni kila mwezi, ukiambiwa utoe ufanuzi wa Shirika hilo wewe kama Mkurugenzi unasesma tumejitahidi na tuna mikakati mikubwa na nini kila kitu na mishahara tumelipa yote na deni tunadaiwa kidogo tu. Sifa zote anazojipa Mkurugenzi ni kutokana na uelewa wake kwa wakati huo. Lakini akiambiwa kwamba kuna Shirika lingine ambalo labda ni *Alliance, British Air Ways* kwamba hilo Shirika raslimali zake ni kubwa mno linatengeneza faida nyingi mno, huyu mtu atasema bwana mimi nafanya kazi kubwa sana. Lakini kwa sababu ya kutopenda kujifunza kwamba *British Air Ways* wanafanya nini, kwa nini wanaboresha Shirika lao mwaka hadi mwaka na wanatengeneza faida kubwa sana.

Sasa Mheshimiwa Waziri mmoja alipokuwa anatoa ufanuzi hapa anasema katika Jimbo la Mheshimiwa fulani tumejenga hospitali, tumejenga visima, tumefanya nini, nasema ni kazi nzuri na tunampongeza, lakini isiwe kipimo cha kujipima kwa hicho kidogo, tujipime na vile vikubwa ambayo ni vikubwa zaidi ili tuweze kuboresha zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike wakati tukubali kuanza kujadili mambo magumu ambayo kwetu sisi tunawenza tuisipende kuyasikia lakini ndio *fact* zipo. Tuyajadili kuliko kungojea wakati unapokuwa umeshakuwa mgumu, wakati ambapo mitafaruku inaweza kuwa imeshaanza, matokeo yake tukashindwa hata kui-control hiyo mitafaruku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila baada ya miaka mitano huwa tunafanya chaguzi na sasa hivi tunafanya chaguzi zinazoshirikisha Vyama vingi ambayo vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria. Sasa ndani ya chaguzi hizi kuna kushinda na kushindwa. Utawala Bora ni pamoja na kukubali kuandaa mazingira mazuri ya kukabidhiana madaraka. Tukubali tuenze kutengeneza mazingira mazuri yanayoweza kuwaepushia Watanzania mitafaruku pale ambapo mtu anakuwa ameshindwa na ameshindwa kabisa kwa kura ili akabidhi madaraka kwa yule aliyemshinda badala ya kubaki tu kungojea kwamba kitu kitakachotusaidia dakika za mwisho ni ujanja ujanja wa kufanya hivi, kufanya hivi. Tunajitengenezea kaburi huko mbele ya safari! Kuna mahali ambapo watanzania watafika mahali hata hizo njia za ujanja ujanja zitashindikana na matokeo yake solution iwe kuondoka na shingo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Watanzania tusingependa tufike huko. Nchi yetu tunapenda, amani na utulivu ambaa umeasiwi na waasisi wa nchi hii...

#### **MBUNGE FULANI:** Wa CCM.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** CCM na baba yangu na babu yangu na babu wa babu walikuwepo na wajukuu wangu wa Kigoma wakiwemo, ni kwamba tunataka tuzienzi na ziwepo. Lakini bila kutengeneza mazingira ya kuwezesha hiyo na kuwa na mipango endelevu na mipango inayoweza kutekelezeka katika mazingira tunayokwenda nayo, kwa kweli tunaweza kuhatarisha usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nafikiri ndani ya Utawala Bora ambapo na Ofisi ya Rais iko humu humu kwenye Bajeti hii, ifike mahali Chama Tawala (CCM) na Serikali yake ambao sasa ndio nyie, mna ridhaa ya kuongeza jahazi; ndio ma-architecture, ndio ma-contractor wa kutengeneza mambo. Tengenezeni mazingira yatakayoweza kuruhusu pale mtakapoona sanduku la kura limewakataa

mkubali yule atakayekuwa amewashinda mumkabidhi madaraka na tuige mifano ya nchi nyingine. Tumeona Kenya japo yule bwana, Mkurugenzi wa Uchaguzi alichelewa kutangaza akapokea kofi kwanza akatangaza kisawasawa. Sasa sisi tukubali tusifike huko, tusingoje makofi. Tukubali katika taratibu ambazo tumejipangia sisi wenyewe, tuweke utaratibu wa kukabidhiana madaraka. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema hivi, tunakubaliana kabisa na dhana ya *globalization* na Mheshimiwa Rais mara nyingi amekuwa anasema hatuna jinsi ya kulikwepa suala la utandawazi na yeze ni Mwenyekiti mwenza tunampongeza. Lakini tuwe waangalifu na utandawazi. Tukienda kichwa kichwa tutaliwa. Tutaliwa kabisa! Kwa sababu tunapozungumzia utawala bora, *corruption*, hata suala la *corruption* ni *globalized* sasa hivi. *It is a global issue.* Anakuja mwekezaji na lugha nzuri na pesa nyingi kwa kujua kiwango chenu cha kutotambua masuala yaliyomo kwenye *package* ya *globalization*. Hata ile *bargaining system* yake inakuwa ya kiujanja ujanja na kwa kukujua kwamba weye uwezo wako ni mdogo, ni mshamba katika masuala haya anakuacha solemba unaingia kichwa kichwa kwenye mkataba ndio unashitukia umeuza nchi kwa njia ya kalamu na sahihi yako moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba tunapozungumzia suala la *globalization* hata suala la *corruption* na Mheshimiwa Waziri mhusika wa suala hili nasikia ataleta mkataba hapa wa kuridhia, itabidi ajiandae na mimi nitachangia kwa nguvu zote kwamba tunaporidhia mikataba mingine tujiangalie sisi *base* yetu kwanza ya kuhimili hata hicho kitu chenyewe sisi wenyewe katika mazingira yetu. *Level* yetu ikoje, uwezo wetu ukoje kabla hatujaingia hata kwa mambo mengine makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nisingetaka nigongewe kengele ya pili. Mheshimiwa Waziri tunangoja majibu yako. Kambi ya Upinzani na Baraza langu kwa ujumla tumekubaliana baada ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, suala la Waziri Mkuu na mambo yake tumelifunga rasmi, wala hatutaki kulijadili tena kwa sababu na Bwana Yesu wakati anawahubiria wanafunzi wake alisema mwenye masikio na asikie, mwenye macho aone. Sasa umma na raia ndio wataweza kuona mwelekeo na mambo tunayoyazungumza sisi hapa Bungeni. Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. (*Makofi*)

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Mchangiaji wetu wa mwisho ambaye amechangia mara mbili ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, ndio wa mwisho kwa leo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nianze kwa kuchukua nafasi ya kukushukuru kwa kunipa ruksa maalum katika ukumbi huu wa Bunge ili niweze kuchangia hoja iliyoletwa mbele yetu na Wizara hiyo ambayo ina Mawaziri wawili wanaofanya kazi ndani ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo usemi unaosema kwamba mara zote yule anayelipia ngoma ndiye anayechagua wimbo. Unapolipia ngoma ya aina yoyote ile iwe ya kienyeji, iwe ni muziki, iwe ni taarabu, kwa hiyo, wewe ndio utatakiwa pia useme na nyimbo zitakazoimbwa kwenye hiyo ngoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema hivyo nina maana nzito sio kama ile inayofikiriwa kwa wepesi. Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndio iko madarakani kwa sasa hivi na ndio Serikali inayoongoza na kusimamia mipango yote ya maendeleo katika nchi ya Tanzania ikiongozwa na Ofisi hii ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi mimi naomba niwapongeze sana Mawaziri hawa wawili kwa sababu kwa usemi wa kulipia ngoma, basi nyimbo walizozichagua zinafanya kazi inayotakiwa katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni uungwana na jambo la busara sana kila linapofanyika jambo ambalo ni la manufaa katika jamii ya Watanzania hatuna budi kulizungumza na kulisifia. Ninawashukuru hata ndugu zetu wa upinzani sasa wamegundua kwamba yapo mambo ambayo yanafanywa na Serikali hii chini ya Ofisi ya Rais ambayo kweli yanaonyesha kwamba kuna mwelekeo wa maendeleo katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo ambayo yanaashiria pongezi za moja kwa moja katika utendaji mzuri wa majukumu ya kila siku ya Ofisi ya Rais, basi naomba tu nizungumze mawili matatu kama ushauri wa kuboresha zaidi nyimbo hizo zilizochaguliwa baada ya kulipiwa ili kazi

inayofanywa na Mawaziri hao wawili na inayobeba kioo cha nchi ya Tanzania iweze kueleweka vizuri na kwenda katika utaratibu mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kushukuru Wizara kwa kugundua kwamba upo umuhimu wa kuwa na ile Tume ya pamoja ya Utumishi wa Umma. Tume ya Utumishi wa Umma kwa mawazo yangu ninaamini kabisa kwamba inatakiwa ianze kufanya kazi haraka sana. Watumishi wengi katika nchi ya Tanzania bado wako katika matatizo makubwa na ninaamini kabisa kama Mheshimiwa Rais atamaliza haraka kuteua hao Makamishna watakaoiongoza Tume hiyo, basi matatizo mengi ya watumishi wa umma katika nchi yetu ya Tanzania yataanza kushughulikiwa kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kucheleta kuteuliwa kwa Makamishna hao kunaendelea kuchelewesha utendaji kazi wa Tume katika kutatua matatizo na migogoro ya watumishi katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe na amwombe Mheshimiwa Rais hilo lifanyike mapema ili masuala ya utumishi wa umma yaanze kushughulikiwa kwa kadiri ya utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba mionganoni mwa matatizo makubwa ambayo ni sugu, nadhani ni hilo linalohusu upandishwaji wa vyeo wa watumishi na upandaji wa mishahara yao katika ngazi mbalimbali. Mimi kama Mjumbe wa Kamati hiyo ya Katiba, Sheria na Utawala Bora, tulizungumza kwa kirefu sana tatizo linaloikabili nchi yetu katika zoezi zima la kupandishwa vyeo kwa wafanyakazi wa kada mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wengi wamekuwa wakifanya kazi kwa muda mrefu, lakini kada na ngazi mbalimbali zinazoshughulikia suala zima la upandishwaji wa vyeo vyao, imeonekana kuwa na upungufu mkubwa na hivyo mtumishi wa umma anaweza akakaa miaka kumi bila kupandishwa cheo na anapokuja kupandishwa cheo haileweki haki zake zilizopotea katika miaka yote hiyo iliyopita zitalipwa na nani na zitafanyiwa nini.

Kwa hiyo, pamoja na mambo mengine ambayo yanatakiwa yashughulikiwe, mimi nilikuwa naomba hilo nalo lingepewa kipaumbe na kama tunavyokumbuka kwamba tayari siku za karibuni tulishasaini Mkataba wa Huduma Bora kwa Wateja na nafikiri wateja wakubwa wa Ofisi hizo ni pamoja na hao watumishi wa umma ambao wamekuwa mara nyingi wakipata matatizo ya upandishwaji wa vyeo, kupandishiwa mishahara yao na maslahi mengine ambayo yanawakabili kila siku.

Pamoja na hayo nilikuwa naomba pia kutoa ushauri wangu kuhusiana na ajira za watumishi wa kigeni katika nchi yetu ya Tanzania. Suala la ajira za watumishi wa kigeni katika nchi yetu ya Tanzania mimi nilikuwa nashauri kabisa Ofisi ya Rais ianze kuliangalia vizuri. Ninashukuru kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amelizungumzia, lakini kwa kweli kila mwaka limekuwa likizungumziwa na mimi nafikiri sasa Ofisi hiyo ingeanza kutusaidia kutupa *data* kamili zinazohusu suala zima la ajira za watumishi wa kigeni ndani ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wengi wa kigeni wamekuwa wakichukua nafasi za Watanzania katika kufanya kazi ndani ya nchi zetu, wamekuwa wakilipwa mishahara mikubwa lakini kazi hizo zingeweza kufanya na vijana wetu wengi ambao wana elimu nzuri na zinazoweza kufanya kazi kwa nafasi hizo hizo zinazofanywa na hao watumishi wa kigeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Ofisi ya Rais iangalie sana suala hilo na ikiwezekana kwa kweli pamoja na *report* tuliyopewa na Mheshimiwa Waziri, lakini basi tuone kwamba linatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa naendelea kuomba kwamba Tume ya Maadili kwa siku hizi za karibuni suala la maadili ya watumishi wa umma, viongozi na kadhalika limekuwa likipata upeo na sura kubwa sana ndani ya nchi ya Tanzania. Lakini nafikiri nipongeze Tume hiyo kwa sababu kwa kweli imeanza kufanya shughuli zake kwa kiasi na kiwango kikubwa. Lakini hivi kweli mpaka sasa hivi ni watumishi wangapi ambao wanaingia katika utumishi ama kada mbalimbali za uongozi, wanajua msingi mkubwa wa maadili wanayotakiwa kuyafuata wanapokuwa katika utumishi wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niendelee kusisitiza kwamba mafunzo kwa umma, mafunzo kwa watumishi na hasa kuhusiana na maadili yao katika ngazi wanazofanyia kazi ni suala lingine la msingi ambalo litawasaidia sana kuelewa na hivyo kurahisisha hata zile kazi zitakazokuwa zinafanywa na Tume hiyo ili kuboresha utumishi huo bora wa umma, lakini pia kuendelea kuleta sura nzuri ya hali ya watumishi wa umma na maadili yao katika kazi zao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtumishi wa umma, kila kiongozi anatakiwa kuwa na maadili bora kulingana na kada ya nafasi yake anayoifanyia kazi. Tunaomba tu pia ili kuendelea kuboresha utawala bora, suala la haki za binadamu na elimu kuhusu haki za binadamu iendelee kusisitizwa na ikiwezekana tuendelee kuona utaratibu mzuri wa kuwa na mtandao wa kuhakikisha jamii inapata haki kutoka katika ngazi za Vijiji mpaka Taifani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi katika nchi yetu ya Tanzania na hasa wale wanaoishi katika maeneo ya Vijiji na hasa wale wanaoishi mbali na maeneo ambayo yanaweza yakatoa haki katika mambo yao ya kila siku wamekuwa wakishindwa kufikiwa. Nadhani pia tatizo lingine kubwa ni ufnyu wa bajeti katika nchi yetu. Lakini katika masuala ya haki za binadamu mimi nilikuwa nafikiri kwamba ni bora kabisa tuweke mkakati wa moja kwa moja ili kuona ni namna gani tunaweza kabisa kuwashirikisha wananchi wote wa Tanzania wakaelewa ni mahali gani wanaweza kupata haki zao na mahali gani wanaweza wakafika na wakauliza jinsi ya kuweza kupata haki zao kwa urahisi bila ya kuwa na urasimu wa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia upo utaratibu ulioandaliwa wa kupokea na kushughulikia malalamiko yanayotolewa na wananchi kuhusu watumishi wa umma. Kwa kweli katika kipengele hiki na utaratibu huu bado hali ni mbaya. Bado wananchi hawana uhuru wa kutosha na bado wanapambana na vikwazo vikubwa pale wanapojaribu kutoa taarifa mbalimbali zinazohusiana na suala zima la huduma zinazotolewa na watumishi wa umma katika maeneo mbalimbali ya kazi huko walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana suala hili pia katika Bajeti ya mwaka huu lizingatiwe kwa karibu ili kuweza kuboresha huduma hizo ziweze kufika kwa wakati na mahali zinapotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nisimalize hotuba yangu au maelezo yangu bila kuishukuru Ofisi ya Rais katika mpango mzima wa ushirikishwaji wa jamii katika miradi ya maendeleo kupertia mfuko wa *TASAF*. Ni kweli kabisa mfuko huu haujafika katika maeneo mengi ya nchi ya Tanzania, lakini katika maeneo yale machache ambapo mfuko huu umefanya kazi, kwa kweli tunaomba kwamba tupongeze kabisa uongozi mzima wa mfuko huu wa *TASAF* na utaratibu ultiwekwa na jinsi mfuko huu ulivyoweza kufanya kazi za kuleta maendeleo na zinazoonekana kabisa mionganoni mwa jamii ndani ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoendelea kupongeza, ninaomba tu uongozi mzima na muundo mzima wa mfuko huu basi kwa maana katika awamu ya kwanza umeweza kufanya kazi za kutosha, lakini uendelee kuongeza juhudu zaidi na ikiwezekana kuangalia miradi ya akina mama pia katika kiwango cha karibu ili kuweza kusaidia kuleta maendeleo ya pamoja ya kiutendaji ndani ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda mwisho niombe pia kwamba kumekuwa na utungaji wa sheria ndogo ambazo zinatakiwa zifanye kazi katika suala zima la utumishi wa umma, utawala bora na kadhalika. Mimi nilikuwa naendelea tu kusisitiza sheria hizi ndogo zinapoandaliwa, basi zihakikishwe kwamba hazigongani na Katiba yetu ya nchi ili kuweza kuzifanya zitekelezeke vizuri. Ninashukuru sana Ofisi ya Rais, yapo matatizo madogo madogo yaliyokwishakuonekana lakini wameahidi kwamba wataona ni namna gani tunaweza kushughulikia. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana masuala haya yaendelee kuangaliwa kwa karibu zaidi ili yasilet matatizo katika utekelezaji wa mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, mimi naendelea kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Mawaziri hawa wawili lakini pia ninaomba pia kumpongeza Mheshimiwa Rais mwenyewe wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi alivyokuwa mhimili wa nguvu katika kuhakikisha

kwamba miaka hii mitano nchi yetu ya Tanzania inapiga hatua kubwa katika maendeleo ya namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Sera za Chama cha Mapinduzi zitaendelea kudumu na ninaendelea kusisitiza kwamba Chama hiki bado kitaendelea kutawala na bado kina nguvu na tunaendelea kuwaomba wenzetu ambao wanatusaidia kutushauri wachukue nafasi kubwa ya ushauri na sio kulumbana na pia wachukue nafasi kubwa ya kupongeza haya mambo yanayofanyika na Chama cha Mapinduzi ambayo yanaonekana na kimsingi ni kwamba haya yote yanayoonekana yanatufaidisha sisi wote Watanzania bila kujali itikadi zetu wala bila kujali ukabila wala dini wala kitu chochote.

Kwa hiyo, barabara zote zinazotengenezwa tunatembea wote, *dispensary* zote tunaingia wote na kutiwiwa na kila kitu kinachopiga hatua kwa kweli kinatusaidia sisi wote kwa pamoja. (*Makofii*)

Kwa hiyo, nawashukuru ndugu zetu wa upinzani wanatusaidia kutushauri lakini kwa kweli waongeze bidii ya kutushauri na sio kupiga kelele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofsi*)

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kuna Mheshimiwa Waziri mmoja alileta karatasi yake hapa, ndio nimekumbushwa sasa hivi kwamba alitakiwa kuchangia. Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir. Huyo ndio mchangiaji wetu wa mwisho. (*Makofsi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi, hoja ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiongozi wa Upinzani kabla hajakaa ndugu yangu Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, alisema yuko Naibu Waziri mmoja hapa alisimama akatoa mfano wa mambo madogo madogo katika jimbo moja kule Pemba, alikuwa ananikusudia mimi na kwa sababu mimi ni muungwana ningependa kumkumbusha ye ye kwamba ukisalimiwa basi uungwana ni kujibu kwa bashasha, siyo habari nzuri, basi hapana! Nzuri, nyumbani hawajambo, watoto je?

Sasa unapojibu hivyo wanasema tuna kiburi na jeuri. Kumbe ndiyo uungwana wenyewe na unapodharau mambo madogo huwezi kupata mambo makubwa. Upo msemu wa Waingereza usemao: “*Take care of the cents and the shilling will take care of itself.*” Sasa wewe ulimwona yule Mchaga aliyeona ghorofa tatu, akafikiri zote ni KNCU kuwa ni mshamba, wewe unataka kuona ghorofa tatu kuanzia juu kabla ya chini, kumbe ushamba hauna kwao. (*Kicheko/Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kuchangia hoja hii katika sehemu ya kwanza, Utawala Bora. Asubuhi wakati Msemaji wa Upinzani anachangia hoja hii katika ukurasa wa pili ibara ya tano, alizungumza maneno yafuatayo, naomba kunukuu: "Pamoja na kuwepo kwa Taasisi nyingi zinazoshughulikia suala zima la Utawala Bora, bado Tanzania iko mbali sana tu katika kuwa na jamii inayofanana na Utawala Bora."

Nafikiri kauli hii ameitamka kwa sababu ya mtazamo wenyewe upungufu. Nchi hii ina Utawala Bora na ni vizuri Watanzania tukawa tunajivunia mambo yetu ambayo yanakuwa ni mazuri. (*Makofsi*)

Baada ya hili kubwa la Utawala Bora katika jamii yoyote ile ya wanadamu, ni uhuru na amani. Ukiona hata mtaani kwako, jirani yako wanandoa wamekaa miaka nenda miaka rudi hujasikia ugomvi wala kufungishana mizigo, humo ndani kuna uhuru na amani na amani tunayoiona ndani ya nchi yetu ni matokeo ya Utawala Bora. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachilia mbali mfano wa Taifa zima, chukua chama katika siasa, ukiona watu wameshindwa kuelewana katika mkuwashindwa ambao wana dhamira moja, lakini hawaruhusu

kila mtu kutoa maoni yake kwa njia yake ili wafikie dhamira hiyo, hapo ndipo panapokosekana Utawala Bora. (*Makofi*)

Chama kikubwa kama Chama Cha Mapinduzi chenye watu wengi, bado wanakaa na kubishana na kushauriana lakini baadaye wakatoka kwa salama na amani. Huo ndio mfano mzuri wa Utawala Bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ulioifanya nchi hii inayoongozwa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kuweza kuhimili na kukabili misukosuko ya mabadiliko mbalimbali. Nchi ambayo haina Utawala Bora, haina viongozi makini na chama madhubuti, haiwezi kukabili misukosuko ya mabadiliko hata kwa dakika mbili. Ndiyo maana mnaona Perestroika imegawa Urusi vipande vipande. Hayakuwa mambo ya bahati mbaya. Lakini Tanzania pamoja na ulimbukeni, maana hatukuwa tumeandalishi juu ya kupokea vyama vingi, lakini bado Chama hiki cha Mapinduzi kiliweza kuishika Serikali vizuri na kuhimili ulimbukeni ule wa vyama vingi wa matusi, kejeli, wakati mwengine watu kujitia na rangi nyekundu usoni, dalili kwamba tutamwaga damu, lakini bado chama kilisimama imara kuhakikisha kwamba Utawala Bora unaleta amani ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Upinzani amesema kwamba Utawala Bora ni kusahau na kusamehe, sadakta, barabara kabisa. Kusamehe na kusahau ndiyo Utawala Bora. Mimi nakubaliana naye. Lakini unapotamka hili kwa CCM ni kumfundisha samaki kuogelea. Maana hiyo ndiyo sera yetu. (*Makofi*)

Ndiyo sera yetu na ndiyo maana CCM ilihakikisha kwamba siyo tu kwamba tunaanzisha mazungumzo ya Muafaka kama alivyosema kaka yangu Hamad Rashid Mohamed. Lakini tuliusimamia Muafaka ule kuhakikisha kwamba baadaye watu tunakuwa kitu kimoja, tunasahau yaliyopita, tunasameheana, tunaanza upya. (*Makofi*)

Kama wasemavyo Waswahili: "Ya nini kuyadhukuru na yakinipa huwa hayadhuru?" Lakini nawashangaa sana anaposimama mtu yule yule anaitetea dhana ya kusahau na kusamehe, akataka iundwe Tume kama ya Afrika ya Kusini eti ije ifufue uchungu na madonda ya tarehe 26 na 27 Januari, 2001. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ambayo anajua haikuundwa na Bunge hili. Kuna ilikoundwa na majibu yamepelekwa huko na watu wa Muafaka wapo wa pande zote mbili, tunawaona humu ndani. Unataka kuyatoa kule uyaleti mahali ambapo si pake. Huyu ndiye anaetetea kusahau na kusamehe. Ndiye huyo huyo anayetetea kusahau na kusamehe, anataka tuunde Tume ya kufufua habari za akina marehemu Kassim Hanga, Kasanga Tumbo, Joseph Kasela-Bantu, Abdulrahman Mohamed Babu, Oscar Kambona na Othman Shariff Mussa na wengineo wengi, ili iweje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana mwanadamu mwenye akili zilizo kamilika anapotaka kutengeneza jambo ana sababu. Sababu ya hii ni nini kusahau na kusamehe au kutonesha yaliyokauka ili yaibuke upya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wanaoyaangalia matokeo wapate kusimulia na wengine kuyageuza kuwa mtaji. Lakini tupo tuliozoea kuangalia chanzo cha matokeo ili kurekebisha jambo hilo lisitokee tena, mara nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo yaliyokuwemo ndani ya Muafaka kuangalia, hivyo kulikuwa na kitu gani? Kulikuwa na lazima kufikia hapa? Kama ilikuwa hamna lazima tufanyeje tuondoche hapa tulipo twende huko. Tumeondoka na watu tumerejea tuko Bungeni, anataka turudi kule kule. Huku ni kufanana na mtu kwenye giza kubwa unampa tochi halafu unamwambia mulika nyuma, yeze anakwenda mbele. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kitu tuunde Tume. Kuiga tu, tuunde hiki tuunde hiki, tunaiga tu, tunaiga tu. Wengine wanataka *NARC*, wala hawataki kuangalia mazingira ya *South Africa* yaliyopelekea kuunda Tume ile, wala mazingira ya Kenya yaliyopelekea kuundwa na *NARC*. Haya undeni mnachotaka kiundwe. Mtatukuta tuko imara tunakusubirini kwa hamu kweli kweli. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatisha unapomwona kiongozi anabeza hata Operesheni Vijiji ndani ya nchi hii, hajui Hospitali, Vituo vya Afya, Shule, Visima vya maji, anavyoviona leo ni matokeo ya watu kukusanywa pamoja katika vijiji vya ujamaa. (*Makofî*)

Haya yasingewezekana kwa mtindo ule wa kila mtu kukaa mahali pake alipo. Sasa sijui amezungumza kwa sababu ya umri, hakuyaona au kayasahau kwa sababu tunaandikiwa tupewe tusome bila kuyaona, ni matatizo haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msemaji amefikia mahali kusema uongozi ni utumishi na wala sio ufalme. Wakatumia na neno la Kizungu, *bureaucratic pomposity* eti sisi viongozi wa Serikali wa Chama Cha Mapinduzi tunawaonyesha wananchi jeuri, kibri, mikogo na minjonjo ya kukamata vyeo. (*Makofî*)

Sasa mkisema, tukikaa kimya, sisi tunakuwa wajeuri kweli kweli. Lakini tunapowajibu huo ndio uungwana wenyewe. Sasa tukiwajibu ninyi mnaona hiyo ni minjonjo. (*Kicheko/Makofî*)

Sasa huko ndiyo kukurupuka na kuchemka, siyo sisi na binadamu wa kawaida, kama hawesi kustahamili joto haingii jikoni. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mengine tunapoyasikia sisi tunashangaa tuyajibu au tufanye maana yake wananchi wanasikia, inabidi tujibu tu. Tunatafuna jongoo kwa meno. Mtu anasimama anasema: "Mimi ninavyomjua Mheshimiwa Waziri Mkuu Frederick Sumaye, ninavyomjua mimi, ana uwezo wa kubeba ushujaa wa kuwajibika na kuachia ngazi." Huyu unamjua wapi? (*Kicheko/Makofî*)

Haya ameyatamka kwenye ukurasa wa 13. Kwa nini aachie ngazi? Kwa sababu mwaniasiama mmoja huko amesema Mheshimiwa Frederick Sumaye ni mla rushwa. Katika mazingira ya sasa ikiwa tutachukulia kila linalosemwa na kiongozi wa kisiasa kutoka kambi ya upinzani juu ya kutuhumiana basi hakuna atakayebakia ndani ya Ukumbi huu. (*Makofî*)

Maana maneno yao mara nyingi yanakuwa hayana mbele. Kwa mfano mkubwa, msemaji huyu amesema katika ukurasa wa nne fasili ya tano mstari wa nane, eti sisi tunawatolea ufedhuli wananchi. Amesema leo humu asubuhi. Sisi tunawatolea ufedhuli wananchi. Ingekuwa ndiyo kila lisemwalo na lenyewe tulichukue tuwajibike, nani angebakia humu ndani? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungkuwa mafedhuli tungechaguliwaje mara zote hizi kurudi humu ndani. Lakini hawa wenyewe kwa wenyewe wiki iliyopita yuko kiongozi mmoja yuko hapa namwona wa Chama Cha Upinzani, kamsingizia kiongozi mwenzake wa chama cha upinzani kwamba amenunuliwa na CCM na alipewa zawadi ya kukodisha watalii kwenye *Mount Kilimanjaro Marathon*, tukasoma kwenye magazeti. Sasa na hilo ukilichukulia lilitivo, yule mzee naye astaafu. Sasa watabakia wangapi? (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno haya mimi namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Frederick Sumaye, afanye kazi zake, usiku alale usingizi buheri wa afya. (*Makofî*)

Vyombo vinavyohusika vikiona ana hatia vitachukua hatua na kwa Chama Cha Mapinduzi hayo si mambo ya ajabu kwetu. Hivi hizi nongwa za nini? Mbona kama ni urais bado haujafikia? (*Makofî*)

Halafu wengine wanatuambia kwamba eti wazee hawa mnawateua teua, hawawezi hata kukamata sungura. Ninyi hawa wazee wa kwenu wanaweza kukamata sungura, si mnao? (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kiwango hiki cha mzee ni kipi? Sijui kiwango cha uzee ni umri au kukaa madarakani muda mrefu. Maana nikiangalia vyama ambavyo vinawakilishwa hapa Bungeni, Chama kimoja kimekuwa na viongozi Serikalini, mmoja amekuwa Mkuu wa Idara ya Uchumi ya Chama Tawala, mwingine amekuwa mshauri wa Rais wa Serikali hii hii. Chama kingine amekuwa Naibu Gavana wa Benki Kuu. Hivyo kama ni kuupotosha uthumi wa nchi hii wao wanajitowaje kwenye jahazi hili? Sasa

ukiwa CCM uwe mzee huwezi kukamata sungura. Ukitoka ukienda kwenye Kambi yao wewe ni mzee kijana!! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, ndani ya Kikao hiki cha Bajeti kazi yetu kubwa WaheshimiwaWabunge, ni kuangalia mafanikio na matatizo ya Bajeti ya mwaka uliopita kwa Wizara husika ili tuweze kutumia akili yetu sasa ya kuangalia namna gani Bajeti inayokuja tutachangia iweze kufanya kazi yake inayotarajiwa na wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuja kugeuza kikao chako kuwa ni kilele cha mkutano wa siasa kama wanavyofanya huko nje. Habari ya siasa tusubiriane nje na sisi tuna uwezo wa kusema maana tunayasema tunayoyatenda na yapo ya kuyaonesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mmwenyekiti, wenzetu wataonyesha yale ambayo tumekosea yanayoonekana kuwa sahihi hawayaonyeshi, wananchi wanayaona. Jamani tuachieni wazee wetu, kama mnataka kula nyama kuleni wazee wa kwenu, wa kwetu tutakuwa nao bado. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani hata siku moja kuwa na jamii isiyokuwa na wazee. Hata kwenye mfugo wa mbuzi, yupo yule beberu ambaye akipita unaskia harufu yake. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini hawazungumzii uzee wa umri, kwa sababu wana wazee wakubwa kuliko wazee ninaowajua mimi ndani ya CCM. Hawazungumzii kutawala muda mrefu, kwa sababu nina uhakika wana wazee waliotawala muda mrefu kuliko wa kwetu. Uzee wanaouzungumza ni hekima, wanaogopa tukibakia na hekima zile ndani ya chama hiki, basi wataharibikiwa. Hawa hatuwatoi hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, kwa kutumia muda wako vizuri.

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi kwa hotuba yake nzuri ya leo.

Hata hivyo kwa niaba ya *ALAT* Taifa napenda nikushauri uchukue hatua za haraka ya kurekebisha sheria ambayo bila kujali kupeleka madaraka kwa umma na bila kujali muafaka uliofikiwa kati ya Wizara yako na Kamati ya utendaji ya *ALAT*. Mheshimiwa Waziri ni muhimu afahamu ya kwamba hata iweje bila kuafikiana na *ALAT* hakutakuwa mvutano wa muda mrefu amba badala ya kuleta maendeleo kwa wananchi tutazidi kuwarudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike ya kwamba unapotoa madaraka ya kuajiri, kuwajibika na kadhalika kwa watendaji unakuwa umeshawabagua na kuvunja nguvu ya Madiwani na ni wazi ya kwamba kutakuwa na migongano mikali ya kutisha. Mheshimiwa Waziri kwa kufuta Kifungu 6 (b) cha sheria ya utumishi wa umma Na. 8 ya 2002 ni kitendo kibovu na kinakiuka Katiba ya nchi. Elewa ya kwamba Wizara yako ndiyo inatakiwa ihakikishe haki na sheria za utumishi zinatuwa. Sasa umma wa Tanzania utakuelewaje wewe unapofanya mambo bila ya kuangalia athari zinazoweza kutokea Mhele?

Napenda Wizara yako ifahamu ya kwamba sasa hivi kupeleka madaraka kwa umma ni jambo lililo wazi na hakuna atakayetumika. Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya *ALAT* ninayo imani kubwa kwamba utarekebisha mapungufu yote ambayo yanaletwa na wataalam wako kwenye sheria ya utumishi kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe tu ya kwamba mimi na mwenzangu tumepewaa jukumu na *ALAT* Taifa kufuatilia mabadiliko haya. Nashauri ili kupunguza malumbano uiandikie *ALAT* Taifa marekebisho ambayo unategemea kufanya isishe kwenye maneno ya mdomo wa kwa simu. Natumaini

wewe utakuwa *number one* kuhakikisha malengo ya kupeleka madaraka yanatekelezwa kufuatana na sheria kabla hajavurugwa kwa marekebisho ya ajabu ajabu na pia kufuata Katiba ya nchi Ibara ya 6.

**MHE. DR. AISHA OMAR KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Mary Nagu, Mbunge na Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mbunge kwa hotuba yao nzuri waliyoitoa.

Pili, nawapongeza watendaji wote chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi Ndugu M. Y. C. Lumbanga, akishirikiana na Makatibu Joseph A. Rugumnyamheto wa Utumishi na Abel Mwaisumo wa Ikulu. Tatu naunga mkono hoja asilimia zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Serikali kwa juhudu kubwa za kuona kuwa sera na misingi ya *management* inatimizwa. Vile vile napongeza Serikali kwa jinsi inavyosimamia utekelezaji wa dhana ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tatizo la Utawala Bora katika sehemu nyingi za kutolea huduma kwa wananchi vikiwemo vitendo vya rushwa vinaendelea. Tunaipongeza Serikali kwa kupeleka Maofisa wa *PCB* hadi Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaomba Serikali ifuutilie utendaji wa watumishi hawa kwani baadhi yao huwa wanashahau majukumu na maadili ya kazi zao na kushiriki katika vitendo vya rushwa au vinavyoashiria rushwa. Ni vema kwa kushirikiana sote tuwe tunapokea taarifa za utendaji wao, wenye mashaka na kufanya kazi kama inawezekana kupertia mipango shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Idara ya Utumishi inajitahidi kuweka sawa utaratibu wa utoaji bora kwa mwananchi kupertia sera za huduma kwa mteja, ni vema Serikali iweze kuongeza kasi ya kuwapatia wananchi kupertia Halmashauri zao watendaji wenye kutosheleza na wenye taaluma ili kukidhi nia na tafsiri ya huduma bora kwa mteja, badala ya utumishi kuonekana kuwa kikwazo na matokeo yake kuleta malalamiko yasiyo na msingi.

Kuhusu Watumishi wa Idara nyingi hususan afya, watalaam na ugavi bado kwa muda mrefu hawapandi vyeo wala mishahara kutokana na kasi ndogo ya watendaji husika kutoshughulikia ile hali watumishi wanahamasika kwenda kusoma kuongeza ujuzi. Pamoja na maeleo mazuri ya Mheshimiwa Waziri kuhusu suala hili ni vema sasa Serikali isimamie ili wale wanaokwamisha dhana hii washughulikiwe badala ya kuwaacha na hivyo kuipaka matope Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuweza kuandaa utaratibu wa kufaidika na kupandisha mishahara ya watumishi kwa asilimia 6 hadi 10. Nawapongeza tena na ninawatakiwa kila la kheri katika kutekeleza sera na utekelezaji wa miongozo ya utumishi na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. TEDDY L. KASELLA BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja ilio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala Bora ni pamoja na kuangalia matumizi ya fedha mazuri ya vyombo/mali ya Serikali. Hapa ninataka kusema kwamba kwa kuwa sasa tuko kwenye mfumo wa vyama vingi na kwa kuwa sasa pia vyama vya siasa vinapata ruzuku japo mgao wake una tofauti kubwa sana wengine wanapata *Alhamdulillah*, vyama vingine ndiyo hivyo tena ili mradi ruzuku na kwa sababu hii, vyama vingine vinaonekana havifanyi kazi sababu ya nyenzo hiyo iitwayo ruzuku. Lakini sisemi utofauti huu la hasha, nataka kuzungumzia matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si jambo geni kuona viongozi wa Chama kinachotuongozwa wakitembelea wananchi, wakienda Mikoani, Wilayani, Vijijini, wakitumia magari ya Serikali na gharama zote za misafara hii ya Serikali, lakini wakifika huko wanafanya kazi za chama husika. Ingefaa shughuli hizi zitofautishwe ili utawala bora hapo uonekane. Kwani kama Waziri huyu ni mgeni wa wote bila itikadi na ni haki yake kutumia magari hayo.

Lakini akiwa ni Mwenyekiti wa Chama fulani basi ni mgeni wa Chama husika. Fedha za ruzuku za vyama ndiyo hapo zitumike, kama wenyeviti wa vyama vingine wanavyofanya, huu ndiyo usawa na ndiyo haki bila ubaguzi.

Kuna ubaguzi mwengine katika sehemu au nyanja mbalimbali ambazo hazitakiwi hivyo. Hivyo ajira wapate sawa bila itikadi. Katika chaguzi, wanawake wachaguliwe bila kujali itikadi zao. Wajumbe wa Bodi, wachaguliwe bila kujali itikadi. Ni jambo la kushangaza sana, kutochaguliwa Wajumbe wa Bodi eti kwa sababu ya itikadi hasa Wapinzani. Hivyo wachaguliwe tu kufuatana na hekima, busara na ujuzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamalizia kwamba watu waenziwe kufuatana na kazi walizofanya katika Taifa hili. Naungana na hotuba ya Waziri anayesubiri wa Wizara hii Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge kwa hili alivyoliwakilisha. Sioni sababu ya kuongeza zaidi ila nitashukuru sana iwapo litatekelezwa ipasavyo kwani nahuksika kwa Historia ya Mzee Joseph Kasella-Bantu (M.A) ambaye ni baba yangu mzazi.

Kwa hiyo, ili Watanzania wote wajue ilivyokuwa ni vizuri wote waliofichwa wafichuliwe katika historia kwani historia ipo pale pale, inachelewesha tu, lakini haifutiki. Kwa hili siyo huyo hapo juu tu bali ni wote ambaeo wanajulikana kama Kasanga Tumbo, Oscar Kambona, Kassim Hanga na kadhalika na wale ambaeo hatujwaji lakini walifanya kitu katika Taifa hili. Aidha, ni katika kudai Uhuru wa nchi ya Tanganyika na Zanzibar, kudai haki za wafanyakazi, Demokrasia ya kweli, haki za binadamu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ajira na ujira ni muhimu, lazima mshahara uende sambamba na kazi, ujuzi na utalaam. Hapo tutazuia rushwa zisizo za lazima. Pia suala la rushwa tusilifumbie macho, Serikali ipo na ina vyombo vyake, itimize wajibu wake maana kuna mgawanyo wa kazi, hivyo tujitahidi tusiingiliane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walioajiriwa kwa kazi hiyo basi watimize wajibu wao ipasavyo. Nasi Wabunge hasa walio kwenye Chama cha kupambana na rushwa tusaidie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Mary Nagu, kwa ushirikiano wake. Ni mtu ambaye anashirikisha Waziri anayesubiri. Mimi nimekuwa Waziri subira kwa miaka 6 hivi, alinishirikisha bila kunibagua. Naomba Mawaziri wengine wafuate mfano wake kwani wote tunafanyakazi kwa manufaa ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenyewe mwelekeo mzuri. Mheshimiwa Waziri kwa sababu wewe upo karibu na Mheshimiwa Rais, ningependa kuboresha hotuba yako kwa mambo yafuatayo:-

Kwanza, ajira, Mheshimiwa Waziri ni kitu ambacho kina mianya ya rushwa haajiriwi mtu yeoyote kama hajatoa zawadi. Zawadi ni rushwa hata kama ina thamani ya shilingi moja, kuna aina nydingine ya rushwa, rushwa ya ngono ambayo hii huwakumba watumishi wanawake, akikataa kutoa ngono basi haajiriwi.

Kuna rushwa ya uwenzetu rushwa hii ni adui zaidi maana huajiriwa mtu kwa sababu ni ndugu wa karibu na mwajiri akaachwa mtu ambaye ana sifa ya kazi hiyo. Mheshimiwa Waziri rushwa ni jambo la siri siri sana, si rahisi mtu kuweza kugundua ushahidi wa rushwa, hauwezi kupatikana kwa kupigwa picha baina ya mtoaji na mpokeaji, haiwezekani pia kuweza kupata video ya mtoa rushwa na mpokeaji. Kwa sababu hiyo Tume ya kuzuia rushwa ikisikia harufi tu ya rushwa basi isisubiri ushahidi ukamilike au kupata ruhusa kwa mtu yoyote hata Raisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Utawala Bora ni pamoja na viongozi bora, viongozi bora ni kazi ya Rais, wakati wa kuchagua Viongozi wa Serikali yake, asichague Waziri kwa sababu ni rafiki yake au amekuwa ni mwasisi wa chama chake japo kwamba hana uwezo wa kuongoza Wizara au Mkoa au

Wilaya akichagua safu nzuri ya viongozi safi katika ngazi ya Taifa basi na wao watachagua viongozi wa chini yao kwa mfumo huo huo wa viongozi safi na utawala bora unaanzia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais awe tayari kumfukuza kazi mtu yoyote bila kuona taabu na amuwajibishe mtu yelete mara atakapokwenda kinyume na kuutia doa Utawala Bora.

Katika nchi zinazoendelea Mheshimiwa Waziri huweka sehemu maalum ambayo raiwanaruhusiwa kutoa maelezo yao yoyote wapendayo yanayohusu utawala wa Serikali, askari wa siri hupeleka mahali hapo kusikiliza wananchi wanaisema vipi Serikali yao kwa mema na mabaya. Maelezo hayo hupelekewa Rais na akachambue lipi lina maana akalifuatilie na yasiyo na maana akayaache. Je, Mheshimiwa Waziri Wizara yako inamsaidiaje Rais katika kujuu utawala wake ni bora au si bora, ni wa uwazi au usiri?

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii. Tumefurahi sana sisi wanawake wa CCM kuona kwamba takwimu za ajira ya wanawake zimepanda Serikalini kwa mfano 34% ngazi za chini na 39% ngazi ya kat. Tunaomba ajira hii ifikie 50% kwa nchi yetu na hasa ngazi ya chini na uongozi 30%.

Pili, kuhusu *TASAF*, katika Jimbo la Mlandege mradi wa soko bado hatujapewa fedha, wataalamu wa *TASAF* wanazo *documents* zote na *Steering Committee* ilishapitisha. Naomba Mheshimiwa Kamba, afuatinile suala hili baada ya makubaliana.

Tatu, kuhusu Wakala wa *TTB*. *TTB* ililetwa utumishi ili iwe wakala na wafanye idara ya kujitegemea na kuwa sekte itakayojiendesha yenye bila kutegemea Wizara ya Utalii. Je, imefikia wapi? Kama kuna matatizo ni yapi?

Nne, mfuko wa kuendeleza watumishi wanawake, tunaomba mfuko udhamini wanawake wengi viongozi Tanzania hasa kwenye mafunzo ya stashahada na *Ph.D*. Mimi binafsi naomba nidhaminiwe mafunzo ya *Ph.D* kama kiongozi wa wanawake.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Mary Nagu, kwa hotuba nzuri, yenye mwelekeo wa kuweka haki sawa za watumishi wa nchi yetu. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii sina eneo la kusahihisha au kuboresha isipokuwa nina ombi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kusimamia na kufuutilia watumishi wanaonyanyasika kazini na wanaokosesha haki zao wanapostaafu na wakiugua. Ninaomba kuwepo utaratibu wa makusudi kabisa wa kutetea watumishi wanaonyanyaswa kwa kusikiliza malalamiko ya watumishi wa chini nyakati za ziara za viongozi wa Wizara husika (Utumishi) lakini wasikilizwe wakiwa peke yao bila kuwa pamoja na wakubwa wao kwa sababu hawawezi kusema wazi mbele ya wakubwa wao wa kazi wanaogopa kufukuzwa kazi.

Pili, naomba sheria ya haki ya matibabu kwa watumishi wa chini iongezeke, upande wa posho zao ziwe sawa ila daraja za hospitalini zinaweza zikawa kama ilivyo sasa kwa sababu kula kunafanana kwa kila binadamu.

Tatu, watumishi wa taasisi binafsi wapewe mwongozo wa kutenda haki kwa watumishi wao katika kulipwa mafao yao ya kustaafu kama inavyostahili na siyo wapendavyo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hongereni kwa maandalizi ya hotuba nzuri.mchango wangu ni katika maeneo machache tu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uhaba mkubwa sana wa watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa. Vikao vimeshafanyika na uchambuzi wa mahitaji halisi umefanywa na tayari maombi yetu yameletwa Wizarani. Tunaomba myaangalie mkizingatia kuwa Wilaya hii ni changa, imeanza rasmi mwaka 2000 na ina idadi ya watu laki mbili na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki ijayo nitawatumieni *fax* ya kopi ya maombi yetu kwenu. Vinginevyo tutakuwa tumeanza Wilaya katika misingi legelega ambayo itakuwa vigumu kurekebisha baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kongwa, wanaomba sana kuingizwa katika mradi wa *TASAF* katika awamu ijayo kwa vile wananchi wako tayari kushirikiana na kuchangia miradi hasa ya zahanati na vituo nya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *circular* ya Katibu Mkuu Kiongozi kuhusu masharti ya ajira ya Wabunge, iangaliwe upya hasa kuhusu kuruhusu Wabunge wa Viti Maalum na wa kuteuliwa na Rais kupewa fursa ya kurudi makazini mwao baada ya kupindi cha Ubunge kuisha na wakati huo huo kutowataja Wabunge wa majimbo pia kufaidika na *exemption* hiyo. Wakati umepita sasa wa kuwa na *regulations* zinazobagua kundi lile lile linalolengwa. Wabunge wengi ni *experts* katika *areas* zao za *specializations* si vema huko mbele kuwaacha tu, baada ya gharama kubwa ambazo Taifa limegharimika kuwasomesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kumaliza *Ph.D* yake na kwenye hotuba yake nimeona juhudzi za Serikali kusomesha watumishi wake ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza, kwa nini Wabunge huwa hawana programu yoyote ile ya mafunzo na kwa nini inawalazimu kujigharamia wenyewe masomo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wakati umefika sasa wa kutoa fursa ya Wabunge wanaotaka kuijendeleza angalau wakalipiwa sehemu fulani ya gharama maana elimu ya juu ni ghali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumaini kuhusu marekebisho yaliyofanywa kwenye sheria ya utumishi wa umma Na. 8 (kupitia sheia Na. 25 ya Novemba, 2002) yatafanyiwa marekebisho tena. Mheshimiwa Waziri utakumbuka namna ambavyo ilikuwa ngumu kwenye Kamati kuhusiana na suala hili, tunaomba kipengele cha kuipa mamlaka Halmashauri kirudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Ofisi, Utumishi pamoja na Makatibu Wakuu na Wenyeviti wote katika asasi mbalimbali zilizoko katika Ofisi ya Rais. Naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa limeota mizizi katika nchi yetu hususan kwa kulindana. Kuna viongozi amba ni wabovu lakini wamebakia kuhamishwa kutoka kituo kimoja hadi kingine.

Kila kituo wananchi na Chama Tawala kinawalamikia lakini Ikulu inawakumbatia na huku tunapanga vikali masuala ya rushwa. Wananchi wa Kongwa wamemalamikia *DC* akahamishwa kwenda Rombo. Wananchi wa Rombo pamoja na Chama Tawala wakalamika akahamishwa Musoma. Wananchi wa Musoma Vijijini na Mjini na Chama Tawala walilalamika akahamishwa Kiteto. Tunaambiwa na sisi wananchi na Chama Tawala tulalamike ili aweze kuhamishwa. Huu ndiyo mfano wa utawala bora wa Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi ya kushukuru *TASAF* ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa maendeleo kwa Wilaya ya Kiteto. Uibuaji wa miradi ya *TASAF* hutokana na wananchi wenyewe. Katika Kijiji cha Ndendo waliamua kuanzisha shule ya sekondari na Kamati ya *TASAF* Wilaya inakublaiana na Mwenyekiti wa *DC* aliweka sahihi kwenye muhtasari wake na kupelekwa Makao Makuu ya *TASAF*. Wananchi wameshachanga madume zaidi ya 200, wameshakusanya mawe *trip* 65 na mchang'a

zaidi ya *trip* 25 na wameshachukua matofali mifuko 200 na wanaendelea na shughuli ya kujenga hiyo sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, kwa vile wananchi wa Kijiji cha Ndido kwa niaba ya Tarafa yote Makani walifuata misingi yote ya kupitisha miradi bila kukosea na kwa vile *DC* ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya *TASAF* kupitisha miradi anakataa kusaini barua ya kuombea fedha kwani hataki sekondari hiyo kujengwa kwa sababu zake mwenyewe. Naomba tatizo hili litatuliwe kwa maslahi ya wananchi na Kiteto. Nachukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wote na wataalam wa Mfuko wa *TASAF* kwa kazi yao nzuri katika Wilaya ya Kiteto.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa hotuba yake nzuri sana ambayo imeweka wazi masuala muhimu ya uongozi na utawala bora na kuainisha mantiki ya mabadiliko katika menejimenti ya utumishi wa Umma. Nampongeza sana kwa kusoma hotuba yake kwa ufupi, lakini bila kuacha masuala ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwapongeza wale wote ambao wametoa mchango katika kuimarisha maudhui ya hotuba hii wakiwemo Mheshimiwa Wilson Masilingi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Bwana Lumbanga Katibu Mkuu Kiongozi, Bwana J. Rugumyamheto, Katibu Mkuu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na viongozi na watendaji wakuu wa vyombo vyote chini ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, mafunzo maalum yatolewe kwa Maafisa Tawala wa Wilaya (*DAS*). Kuna baadhi hawajaiona Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivyo hawajui wajibu wa Wabunge na hadhi yao.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza kuunga mkono hotuba hii. Napenda kuwapongeza Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kutoa kibali cha kuajiri watumishi wa Idara mbalimbali ambayo ilikuwa kero sana nchini. Naomba muendeelekuokoa jahazi pindi watakapohitajika.

Napenda kushukuru kwa marekebisho ya mishahara ya walimu na watumishi wengine ambao wanastahili. Ombi langu marekebisho ya mishahara yafanyike kwa watumishi walioko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa ni adui mkubwa wa maendeleo. Kazi hii ni kubwa sana ambayo inahitaji ushirikiano wa Tume, wananchi na watendaji wanaohusika. Rushwa imekuwa na mtandao mkubwa kuanzia Vijijini mpaka ngazi ya juu. Naomba kuchangche machache kuhusu rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ngazi ya Wilaya rushwa imeshamiri sana, kwenye ngazi mbalimbali hasa fedha za Serikali Kuu ambazo zimefikishwa Halmashauri zote. Kwenye fedha ambazo zinatumwa Halmashauri za Afya, Elimu, Barabara hizo ni kero sana kwa wananchi kwani kila huduma unayohitaji hupati mpaka utee chochote. Kudai rushwa kwa watu wagonjwa au kununua haki yao ni mbaya kabisa. Tume isaidie kupambana na watu hao. Kule vijijini wananchi wamezoeshwa kutoa rushwa kwa ajili ya kuhitaji huduma. Watu wakinyimwa haki kwa ajili ya kudaiwa rushwa kuna siku ambayo watafanya mageuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuipongeza *TASAF* kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye maeneo ambayo inafanyika. Wananchi wanasifu kati yao nzuri na ya uhakika. Jambo ambalo wananchi wamewapongeza kwa kazi yao ni kuwapa wananchi wachague mradi wanaoutaka, muda wa kufanya mradi huo ambao unaendana na muda waliopanga na kukamilisha miradi bila kuacha viporo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza kwa kazi nzuri, naomba watendaji waigwe kwa kazi nzuri. Naomba *TASAF* sasa waingie kwenye Halmashauri zingine hasa pale ambapo bado wako nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waendelee na kazi nzuri ambayo wanafanya.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri kwa ufanuzi mzuri na wa kina unaohusu Idara Kuu ya Utumishi na asasi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TASAF*. Kwa kuwa mradi wa *TASAF* umefanya vizuri sana na napenda kuipongeza Serikali kwa kusimamia mradi huu vizuri na pia wananchi kushirikiana na Serikali ili kujiletea maendeleo. Nashauri mradi huu wa *TASAF* ungesambazwa nchi nzima ili wananchi wengi waweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa uamuhi wake wa busara wa kuongeza mishahara. Hata hivyo nashauri mishahara ya watumishi iendelee kuboreshwa mara kwa mara ili iwe motisha kwa watumishi wake kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri Dr. Mary Nagu, kwa kiongoza Wizara hii kwa ufanisi mkubwa hii ni pamoja na Makatibu Wakuu wote, Ndugu Lumbanga na Ndugu Rugumyamheto na Mweisumo pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mapendekezo machache yafuatayo:\_\_

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kuwepo na uhamisho kwa maofisa usalama wa Wilaya kwani wamekaa sana katika maeneo yao kama yule wa Wilaya ya Chunya. Hii ni hatari sana katika utendaji wa kazi. Tumekwishesema sana hapa hakuna lolote linalofanyika. Yeye sasa anafanya kazi kama sio mtendaji ana majungu, anafanya biashara ya mbao na kadhalika. Leo naandika siku nyingine nitasema moja kwa moja kwa sababu yeye anajidai hawezi kuondolewa analindwa na Ofisa mmoja wa Ikulu. Sasa aendelee kumlea na itakapofikia tutamwambia Rais pengine ndipo ataondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara hii hasa Waziri mwenye dhamana hii kwenda kuangalia haya ninayoyasema ni kweli au la. Mtendaji haendi Wilaya ya Chunya kufanya biashara na kuendeleza majungu. Havikatazwi mtumishi kufanya biashara lakini iwe halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba kuanzia sasa Wakurungezi Watendaji wa Wilaya kuomba na kutangazwa nafasi yake isiwe kama ilivyo sasa anavyoajiriwa na wafanyiwe *interviews* na wawe na *contracts* ya miaka isiyozidi kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuwepo kwa makusudi uhamisho kwa makatibu Tawala wa Mikoa kama mnavyofanya kwa Wakuu wa Mkoo. Hii itasaidia sana utendaji kazi wa Makatibu Tawala mipango endelevu na ile mifupi, inashhindikana kukamilishwa kwa ufanisi mkubwa na hasa kwa sababu utekelezaji wa shughuli za Mkoo. Unashangaa kuona watawala hawa wamekaa sana Mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Wabunge ili kutekeleza utawala bora wawekwe kwenye Kamati za Usalama za Wilaya na Mkoo. Angalau hata kama hawataingia Wilayani basi wawepo ile ya Mkoo ili kufuatilia vizuri sana matatizo ya msingi yanayotokea huko Wilayani. Yapo mambo ya msingi sana yangeweza kutatuliwa, kimsingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Waziri wa Utawala Bora, Chunya yapo matatizo ya msingi ni bora akayamalize. Tunashukuru kuona *DC* amebadilishwa lakini watendaji wake wa usalama nao wangebadilishwa.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa hotuba nzuri na pia kwa kazi wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa jinsi *TASAF* ilivyoanza, ilianza kwa ubunifu wa mwongozo wake Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, ni Mfuko ulioanzishwa na yeze Mheshimiwa Rais. Utumishi ni kioo cha Serikali na iko chini ya Rais. Sasa, Mfuko huu, kuhusishwa na Utumishi kwa maoni yangu ni kama misplaced. Bajeti yote hii iko chini ya Rais na Wizara zote zipo chini ya Rais. Hivyo mahali ambapo *TASAF* inge-fit kiutendaji ni ama TAMISEMI ama Ofisi ya Makamu wa Rais, Kuondoa Umaskini. Unaweza kusema TAMISEMI inayo majukumu mengi sana, lakini Ofisi ya Rais Utumishi kweli haikai vizuri hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii isipokuwa naomba maelezo kwa suala la *TASAF*.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Waziri wa Utumishi, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Utawala Bora, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Katibu Mkuu Utumishi na Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri na ya kihistoria kwa nchi yetu kuwa na utaratibu ulio wazi wa kuongeza na kuratibu shughuli zote za uendeshaji wa Serikali kwa misingi iliyo bora, yenye utawala wenye lengo la kutufikisha kwenye Serikali bora. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala Bora ni pamoja na kuhakikisha kuwa mipango yetu ya maendeleo haiegemei upande wowote ule wa nchi. Mipango ya hivi sasa baada ya sensa ya 2002, itajibu matatizo yaliyojitekeza katika kila eneo la nchi. Upungufu wa elimu, utapiamlo, umaskini, afya ya mama na mtoto, kasi ya ongezeko la watu, miundombinu na kadhalika ni vitu ambavyo hivi sasa vinajulikana ni wapi kuna upungufu na ni wapi kero kubwa ya Wananchi inahitajika nguvu zaidi na Serikali. Uongozi wa aina ipi unatakiwa sehemu ipi na majukumu ya *NGOs* zipo ziendeshe shughuli zake wapi, ni mambo ya kuzingatiwa. Tungependa kuona kuwa Waziri wa Utawala Bora anasimamia mambo yake hayo kwa kuzingatia takwimu za kisayansi zilizopo nchini bila ya upendeleo. Sera ya haki kwa wote iwe ndiyo dira ya maendeleo yetu mkae kuwa washauri Wakuu kwa Wizara zote husika katika mipango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la baadhi ya Watumishi kukataa kwenda sehemu fulani za nchi kutokana na sababu zao wenyewe. Je, isingekuwa wakati muafaka kwa sasa tukajulishwa rasmi ni hatua zipo zimeandalowi ili tabia hii iliyoanza kujengeka miaka ya hivi karibuni isiruhusiwe kuota mizizi?

Je, suala la kuanzisha *hardship allowances* limefikia wapi hivi sasa? Ni budi tuangalie vivutio muhimu kwa ajili ya Watumishi wanaopelekwa kwenye maeneo maalum na yenye matatizo maalum. Binadamu wa sasa ni tofauti na wa jana. Tujue hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa makusudi kabisa kuwa ione uwezekano wa kusambaza miradi ya *TASAF* nchi nzima, kwa sababu hii imekuwa ni ukombozi mkubwa kwa Wananchi wengi wenyе miradi hiyo. Naungana na Kamati yetu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu ushauri wao juu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kupandisha viwango vya *pension* kwa wastaafu. Ningombaa Waziri atusaidie kuelezea ni kwa nini baada ya viwango hivi kupandishwa Serikali isianze kuwalipa kila baada ya miezi mitatu (*quarterly*). Wazee wengi katika Jimbo langu wameniomba hivyo. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuliambia Bunge hili nini uzito wa gharama za kuwalipa wastaafu *pension* ya kima cha chini cha mshahara? Gharama itakuwa kiasi gani ukilinganisha malipo ya mishahara kwa Watumishi walioko kazini? Je, ni kweli kuwa kuna uwezekano kwa hivi karibuni gharama ya walipwa *pension* inaweza ikafikia nusu ya gharama ya mishahara ya Watumishi waliopo kazini? Kama hilo lipo, ni nini maandalizi ya Serikali hasa baada ya muda mfupi ujao? Kwani wengi watafikia umri wa miaka 60 na kuanza kulipwa pension.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uongozi wa wananchi una sura nyingi, upo ule wa kulazimisha ingawa watu hawakutaki. Upo wa kukubalika sehemu fulani, je, katika zama za Utawala Bora, si ingekuwa vizuri kuanza kuchuja na kutoa ushauri kuhusu sifa zinazohitajika na kutoa ushauri kwa *appointing authority* juu ya baadhi ya Viongozi ambaa wanaonekana hawafai ili warekebishe kasoro hizo? Kumbuka *Peters*

*Principle*, inayosema kuwa: "Syo kila mtu anayefanya vizuri katika ngazi ya chini anaweza kuwa Kiongozi mzuri pia katika ngazi ya juu." Ni vizuri kutafakari masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda niendelee kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, asimamie suala la rushwa kwa mapana yake. Asikubali kuchukua hatua zozote bila ya yeze mwenyewe kuridhika na uchunguzi wake. Wapo watu kazi yao ni kuchafuana majina. Wapo wengine wanaendeleza nia yao ya kisiasa ya kukomoana. Kazi iliyopo mbele bado ni kubwa sana. Endeleeni kusimamia kwa haki bila kumuonea mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamuomba Mheshimiwa Waziri, kila mara nafasi inapopatikana uandaliwe utaratibu kwa baadhi ya Viongozi wa zamani (waliostaafu), waliobadilishwa nyazifa zao (mfano Wakuu wa Mikoa wa zamani, *RDDs* - Mawaziri na kadhalika) kuendeleza uzoefu wao wa uongozi katika kuboresha hayo yanayofanywa hivi sasa na Wizara yake. Tupo, tunaweza kusaidiana na kushauriana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitakia Wizara pamoja na Watumishi wake kheri na fanaka ili tufaidi matunda ya utawala utakaoimarisha demokrasia na uhuru wa kweli katika kuleta ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOHN P. MAGUFULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nitamke wazi kuwa naunga mkono hoja. Aidha, napenda kumpongeza Waziri wa Utumishi, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Utawala Bora, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu Utumishi, Katibu Mkuu Ikulu na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayofanya. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hotuba ya Waziri ni nzuri, lakini nimegundua kuna umuhimu wa kuelezea mafanikio mengi yanayohusu Utawala Bora. Suala la Utawala Bora linagusa Wizara nydingi, mfano mfanyakazi katika mizani au Mkandarasi na kadhalika akifukuzwa, hilo moja kwa moja ni jambo la Utawala Bora. Hivyo, kwa maoni yangu nafikiri siku za usoni pawe na bajeti tofauti itakayokuwa inawasilishwa na Waziri wa Utawala Bora. Hii itasaidia kuonyesha kazi nzuri inazofanywa na Waziri mhusika wa Utawala Bora. Hayo ni maoni yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala Bora unakuga maeneo mengi sana na kila Mtanzania anataka aelewe Utawala Bora unafanya nini. Fedha zipo kwa ajili ya Utawala Bora, Waziri wa Utawala Bora yupo, Katibu Mkuu yupo na watendaji wengine wapo, kuna ubaya gani wahusika hawa wakawasilisha Bajeti yao na Bunge likapata nafasi kubwa ya kupata kazi nzuri zinazofanywa na wahusika? Kwa njia hii Serikali itaonyesha kuwa inazingatia suala la Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PCB* ni chombo kinachofanya kazi nzuri na ninapongeza sana kwa kazi nzuri wanazofanya. Ningependa kutoa ushauri kuwa wale raia wanaopeleka taarifa *PCB* na baadaye zikaonekana ni za uongo na kwa vile uongo ni kosa la jinai, basi wahusika wawe wanachukuliwa hatua mapema. Hii itapunguza majungu na utapeli unaofanywa na baadhi ya raia kwa kupo leka taarifa za uongo. Aidha, ni watu wangapi hadi sasa wamechukuliwa hatua au hata wamepelekwa mahakamani kwa kutoa taarifa za uongo na uzushi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawapongeza wote kwa kazi nzuri wanazofanya na Mungu awajaalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuunga mkono hoja.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ndugu Joseph Rugumyamheto, Katibu Mkuu (Utumishi), pamoja na Viongozi wengine na Watumishi wa Wizara hiyo na Tume zake mbalimbali kwa hotuba nzuri na kazi nzuri sana wanayoendelea kufanya kuendeleza mageuzi na maboresho ya utumishi wa umma kwa mafanikio makubwa, kwa manufaa ya umma kwa jumla na kwa uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo ya jumla, napenda kuchangia kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kutukuza utaalam na utendaji bora. Ni jambo la kusikitisha kwamba wataalam wanaochukua muda mrefu kusoma masomo magumu kama vile udaktari wanashindwa kimshahara na kimaslahi na watumishi wa ngazi za chini kama vile wahudumu wa baadhi ya Taasisi kama vile Benki Kuu (*BoT*) na Mamlaka (*TRA*).

Aidha, wataalam kama hawa hopata mishahara na marupurupu makubwa zaidi kwa jumla katika sekte binafsi na katika nchi jirani. Hali hii inawakatisha tamaa wataalam kama hawa na kuwafanya wasipende kuhudumia sekte ya umma au hata kuihama nchi kabisa. Nashauri Serikali ichukue hatua thabit ya kurekebisha dosari hii ili Taifa lisiendelee kuwakatisha tamaa wataalam hawa na umma uliowaandaa kukosa huduma zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada inazofanya Wizara kufundisha na kuendeleza watumishi pamoja na kuboresha taratibu za kuwaajiri, kuwathibitisha na kuwapandisha vyeo watumishi wa umma, bado ipo haja ya kubuni mbinu na mikakati ya kuhamasisha watumishi wa umma kwa vigezo vya kisayansi ili kuhamasisha zaidi na kuongeza ari yao ya utoaji wa huduma bora. Zawadi maalum na tuzo kama vile nishani na hati za heshima ni mionganoni mwa yale ambayo yangweza kuwa vichocheo mahsusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu taratibu za ajira na wataalam wa kigeni. Pamoja na utandawazi na haja ya kutoa uhuru kwa wawekezaji wa Idara au Taasisi za Serikali kuajiri wataalam kutoka nje ya nchi, kuna umuhimu wa kusimamia taratibu za ajira ya wataalam wa kigeni kwa uchambuzi wa kina na umakini mkubwa zaidi. Mara nyingi Tanzania inakuwa na hazina kubwa ya wataalam wa Kitanzania wenye ujuzi na uzoefu unaolingana au hata kupita wataalam wa kigeni wanaoidhinishwa kujua kufanya kazi hapa nchini na kuwanyima wataalam wa Kitanzania nafasi za kazi ambazo wangeweza kuzitekeleza vema zaidi. Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Simu ni mfano hai. Hatuna budi kujamini na kuamini pamoja na kuwapa moyo zaidi wataalam wetu wenyewe. Kinyume cha hivyo, tunawanyima ajira wanayostahili na kuwakatisha tamaa wataalam wetu pamoja na kuendeleza utegemezi usio wa lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni kuhusu kupiga vita rushwa. Wananchi wengi bado hawana imani kwamba Serikali yetu inapiga vita kero ya rushwa kwa kiwango kinachostahili. Kwa vile bado hapajawa na hatua thabitilizobainisha hatua za kudhibiti na kupambana na rushwa katika ngazi za juu, Wananchi wanaona vita dhidi ya rushwa kuwa kama wimbo tu. Ipo haja ya kupambana na kero hii nzito kwa uzito zaidi na katika hali ya uwazi unaokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Waziri tena kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya mkutano ofisini kwa Waziri, mimi, *DED* wa Karatu na Mwenyekiti wa Hal mashauri ya Wilaya ya Karatu kuhusu soko la Karatu ambalo limetekwa nyara na *DC*, *DED* alikiri kasoro hiyo kuwepo. Kwa bahati mbaya jiwe la msingi la soko hilo aliweka Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

Kwa kuwa Katibu Tarafa ndiye anayefanya ugawaji wa *plot* na vitalu katika soko hilo badala ya Hal mashauri kama Sheria inavyotaka na kwa kuwa *DC* aliagiza wasilipe ushuru, jambo ambalo ni kinyume na Utawala Bora, je, sasa Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani hasa kwa vile sasa ni miezi miwili tangu agizo litolewe na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa? Isitoshe waliokuwepo kwenye soko hilo yaani wafanyabiashara wadogo waliachwa na vigogo kujigawia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jibu la kina ili tujue kweli nchi hii inaendeshwa kwa Sheria na Utawala Bora kama tunavyosema kila siku. Kama sitapata jibu kwa kweli nitatoa Shilingi katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia japo kwa maandishi hotuba ya Mheshimiwa wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri mno, yenye ufanuzi wa kina kwa Wizara hii na inayojenga matumaini makuu kwa Watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 11 kuhusu rushwa, hakika juhudzi zimefanywa kuwabana watoa rushwa na wapokea rushwa. Napendekeza iongezwe juhudzi zaidi ya kushirikisha vyombo vya umma vyenye uwezo wa kuwabana watoa na wapokea rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 14 kuhusu ajira, ni vyema kufuata utaratibu wa kuajiri wanaohitimu mashulenii na vyuoni ili kuondoa manung'unico na kukatishwa tamaa wanapomaliza mafunzo yao na kutofahamu hatima ya maisha yao. Wanaoajiriwa na watu binafsi ni hiari yao kwa utaratibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mishahara, Serikali ndiyo ina utaratibu wa mishahara na nyongeza za mishahara kwa Wizara zote hapa nchini. Mtumishi yeote wa Serikali anayelalamika kuwa mshahara ni mdogo aondoke akafuate mshahara mkubwa anakotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwe ni marufuku kuanzia leo kwa Wabunge kulalamika kuwa Watumishi wa Umma kama vile Polisi na Wanajeshi (Ulinzi na Usalama) wanapata mshahara mdogo. Hii inawapa mori wa kujiona kuwa Serikali yao inawadhulumu na kwamba cha kufanya ni kutaka rushwa kwa hali yoyote ile, mradi wasikamatwe. Kudai mshahara mkubwa Serikalini ni kuilazimisha Serikali kusema: "Benki Kuu print more money," kama alivyokuwa anafanya aliyekuwa Rais wa Uganda, Idd Amini Dada. Askari alipouliza, yeye alijibu: "Si mna silaha, mshahara wa nini?" Matokeo yake wizi na ujambazi ulikithiri Uganda kwa miaka hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilema hicho kimetuangikia. Serikali ndio inajua ni lini itapandisha mishahara na marupurupu yake na siyo kupigiwa kelele Bungeni.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipaji wa mishahara mizuri kwa Watumishi wa umma nchini ni hatua moja ya kuboresha Utawala Bora katika nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yapo malalamiko mengi kuhusu mishahara midogo sana kwa wafanyakazi hasa hasa Walimu wa Shule za Msingi na Walimu wengine kwa jumla. Tunaomba Serikali ilipe suala hili kipaumbele cha aina yake ili isiwe tu kuboresha Utawala Bora, bali pia kuondokana na kero sugu kwa Walimu na Wafanyakazi wengine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojuu kwamba kule Visiwani Zanzibar kilitokea vitendo vikubwa vya uvunjwaji wa haki za binadamu ambapo watu wengi waliuwawa, wengine kujeruhija vibaya na wengine wakaikimbia nchi kwenda Shimoni Kenya kama wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliunda Kamati ya kuchunguza tukio hilo chini ya uongozi wa Brigedia Mstaafu Hashim Mbita. Ni muda mrefu sasa umepita toka Kamati hiyo ikabidhi taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais, lakini ni jambo la kushangaza kuwa hadi hii leo wale waathirika wa matukio hayo hawajapatiwa fidia yao ambayo ilipendekezwa na Kamati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni katika kifungu gani katika Bajeti hii ambacho kinalezea fidia za waathirika hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utumishi, Watumishi waliotumikia zaidi ya miaka 20/22 wa ngazi ya OS 1 - 5 na TGS 1 - 3 Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia 1/3 ya mafao yao mapema. Mfano, maofisa wanashindwa kuandaa maisha yao, matokeo yake wameng'ang'ania nyumba za Serikali au wameshindwa kurudi Mikoani kwao, Wilayani au Vijijini walikotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kugundua kwamba mafao waliyopata mwishoni hayatawatosheleza kujenga, wanaamua kubaki eneo wanaloishi kiutumishi. Madhara yake ni kwamba wanazua usumbufu wanapouguua au wanapofariki, wanazitenga familia, jamaa na koo zao huko makwao na utumishi wa wazazi wa familia hizo husambaratika na kukosa mwelekeo wa mila na desturi za makabila yao na uzalendo hutoweka, pia mazingira ya kiimani hutoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haki za binadamu, Serikali imekuwa ikipiga kelele sana kuhusiana na suala hili, hata ikafikia kuundwa Kamati inayoshughulikia jambo hili. Pamoja na hilo, lakini bado haki za binadamu zinaendelea kuvunjwa kwa mfano kuwa kwenye cheo kimoja kwa miongo miwili, kudai malipo ya uhamisho kwa muda mrefu na wastaa fu kusumbuliwa na kufuatilia mafao yao kwa muda mrefu. Huko ni kuwadhalilisha Wananchi na kuvunja haki za binadamu ambazo Serikali iliridhia Kimataifa kwa hiari yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la rushwa limekuwa linapigwa sana kelele hapa nchini, lakini inavyoonekana bado suala hili linashamiri kile leo. Hii ni kwa sababu wengi wanaocheza mchezo huu kwa rafu ni wakubwa na hivyo ni vigumu suala hili kumalizika kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa kama kweli Serikali imekusudia kulimaliza suala hili ni lazima iondokane na kuoneana haya na iweze kuwajibisha wale wote ambao wamegundulika kuchochea mchezo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa *TASAF* ni suala zuri tu kwa kuleta maendeleo katika nchi yetu, lakini tunaomba uongozi wa mfuko huu kuzingatia sana juu ya uwiano kuhusu fedha wanazozitoa maana baadhi ya mawakala hupewa fedha kiasi kidogo sana kiasi kwamba hata ule mradi waliokubaliana haumaliziki kikamilifu. Kwa hiyo, tunaomba hali hii iangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali ichukue tahadhari kubwa katika kutumia fedha nyingi za walipakodi kwa masuala ambayo pamoja na umuhimu wake, lakini si vyema kupewa kipaumbele kuliko kuzingatia umaskini na kero za Kitaifa. Suala la kutumia mabilioni ya fedha kukarabati Ikulu ni jambo la kuangalia sana. Ni afadhali zitengwe fedha kidogo kidogo kwa awamu ili fedha nyingine ziende katika kuhudumia Wananchi kama vile matengenezo ya barabara, madawa hospitalini, vifaa, huduma za elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, maomba kuwasilisha. Ahsanteni sana.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, iko haja kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi) kuangalia upya viwango vya mishahara na posho kwa Waheshimiwa Wabunge ili vilingane na kupanda kwa gharama ya maisha. Ni vema basi angalau vikaongezwa kwa asilimia 30 - 40 kulingana na uwezo wa Serikali. Kwa kuwa ukimuongezea Mheshimiwa Mbunge mshahara maana yake ni kumwezesha kuweza kutoa huduma nzuri zaidi kwa Wananchi wa Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, utaratibu wa sasa wa kumpa uwezo na madaraka ya mwisho Mkurugenzi wa *PCB* kuweza kukubali au kukataa mtu yoyote kuchunguzwa kwa tuhuma za rushwa unaweza kukwamisha azma nzima ya kutetea haki kukosekana; kwani itakuwa ni rahisi huyu Mkurugenzi mwenyewe kupewa rushwa ili mhusika asichunguzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Wizara ya Utumishi itueleze hatma ya ripoti ya Tume ya Mheshimiwa Mbita iliyo husu matukio ya tarehe 26 na 27 Julai, 2001 na Serikali ina mpango gani kutoa fidia kwa walioathirika katika matukio hayo?

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kuwa naunga mkono hoja hii ila napenda kuchangia machache kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu Mfuko wa *TASAF*. Utaratibu wa kushirikisha jamii katika kuibua miradi inayowafaa katika maeneo yao, napendekeza utumike vile vile na Wizara na Mamlaka nyingine ndani na nje ya Serikali, *NGOs* na kadhalika. Hii itasaidia sana kuoanisha miradi katika maeneo

fulani ili iweze kutekelezwa kikamilifu zaidi ikichangiwa na sekta nyingine zote husika. Mfano mradi wa elimu basi uchangiwe na Wizara ya Elimu, Halmashauri husika, watu wa maji na umeme, barabara na kadhalika. Hivyo, mradi unakamilika siyo *piecemeal*.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu suala la rushwa. Kuna hii Sheria inayosema kuwa mtoaji na mpokea rushwa wote ni wakosaji. Sasa suala ni kuwa utampataje mpokea na mla rushwa kama atakayetoa pia atakamatwa? Nashauri kuwa iwepo nyongeza kuwa kuwe na *suggestion boxes* katika kila eneo nyeti la huduma ili mtu atakayedaiwa rushwa aweze kutoa ripoti humo. Lakini vile vile, napendekeza watoa huduma wote wawe wanavaa alama ya utambulisho mfano jina lake na namba ya kazi kifuani pake ili anayetaka huduma aweze kumtambua anayemhudumia (*conspicuous*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema tena naiunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. OMAR S. KWAANGW:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), Mheshimiwa Rais amekuwa akitoa mfano mzuri wa utendaji wa Mfuko huu. Nami pia nakubaliana na kauli ya Mheshimiwa Rais kuwa utendaji kazi wa Mfuko huu umekuwa shirikishi na matunda yake yanaonekana waziwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, mradi huu upo kwenye baadhi ya Wilaya, hivyo napenda kufahamu vigezo ambavyo vimekuwa vikitumika kuchagua maeneo hayo. Kama vigezo ni maeneo yaliyo nyuma kimaendeleo, basi eneo la Tarafa ya Mbugwe Wilayani Babati lipo nyuma sana kielimu kuanzia Shule za Msingi hadi Sekondari. Eneo hili pia ndilo lenye matatizo sugu ya maji. Mradi wa *TASAF* unaweza kuwa jibu sahihi la kusaidia kutatua matatizo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naona kuna haja ya mradi huu kuweka kiwango cha miradi kwa kila Wilaya ili kuondoa malalamiko ya baadhi ya Wilaya kuwa na miradi mingi na mingine michache na Wilaya nyingine kama Babati hakuna hata mradi mmoja

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa nitapata maelezo ya kina na kufahamu kama maombi yangu ya kuingiza Babati ili Tarafa ya Mbugwe ipate msaada wa Mfuko huu wa Maendeleo ya Jamii. Nitaomba maelezo wakati wa vifungu au majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakutakia kila la heri.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na Viongozi wote walioshiriki kuandaa hotuba hii bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuelekeza mchango wangu katika eneo la miradi ya *TASAF*. Kwanza naomba pia kuwashukuru Viongozi wote waliowezesha Wilaya ya Muheza kuingizwa katika awamu ya kwanza ya mpango wa *TASAF*. Matatizo ya utekelezaji wa miradi ya *TASAF* katika Wilaya ya Muheza imetokana kwa kiwango kikubwa kwa ucheleweshaji wa kuandaa tathmini ya gharama za miradi hasa ya ujenzi na maji. Wahandisi wa Ujenzi na Maji katika Halmashauri wamekuwa wakichelewesha tathmini za miradi na hivyo kuchelewesha upatikanaji wa fedha za miradi kutokana na ukubwa wa Wilaya, upungufu wa watendaji katika Idara husika na uhaba wa usafiri kwa watendaji hao, kazi zimekuwa zikienda taratibu sana. Hali hii imeanza kubadilika baada ya Kitengo cha *TASAF* kupewa gari lao la Idara. Baadhi ya matatizo mengine ni pamoja na *Steering Committee* kuwa na kikao kimoja tu kwa mwaka. Kikao ambacho kinaidhinisha uteuzi wa Vijiji na Bajeti ya mwaka. Inafaa Wenyevitii wa *Steering Committee* washauriwe kuitisha vikao vya ufuutiliaji utekelezaji wa miradi.

Pia baadhi ya miradi ya wananchi kutokbalika kama miradi ya jamii licha ya kuwa ya gharama za kati isiyozidi shilingi milioni 30. Baadhi ya miradi hii ni miradi ya maji ya bomba na barabara. Miradi ya aina hii inatakiwa kuingia katika mradi ya ujenzi. Kwa kawaida miradi ya ujenzi huwa michache sana kati ya miwili au mitatu kwa Wilaya nzima kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza mfumo huu ubadilike ili tuweze kuondoa kero badala ya kuahirisha kero kutokana na taratibu tunazojiwekea wenyewe. Vinginevyo idadi ya miradi ya ujenzi iongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo Wahandisi wa Ujenzi au Maji katika Halmashauri wanapokuwa na majukumu mengi na hivyo kuchelewesha kutayarisha tathmini za miradi basi kazi hiyo ifanywe kwa kutumia vyombo vingine kwa ku-subcontract kazi hizo kwa Taasisi nyingine zenyenye uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza marekebisho kadhaa ambayo tayari yamefanyika katika utekelezaji wa miradi ya *TASAF*. Hata hivyo niliyoyataja hapo juu ni baadhi ya maeneo yanayohitaji kuangaliwa upya ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazipongeza Wilaya zote ambazo zimetekeleza miradi mingi katika mpango huu wa *TASAF* hasa katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi. Pongezi nyingi kwa kazi nzuri zinazofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumeona juhudini mbalimbali zinazofanywa katika kuboresha utumishi wa umma nchini. Hata hivyo, kinachoonekana ni kuwa uboreshaji huu unaeleweka zaidi kwa wafanyakazi katika ngazi ya uongozi na si wa ngazi ya chini. Hakika hawaelewi kinachoendelea! Ukifika ofisini hata mapokezi yao yanaonyesha hivyo. Wataendelea kuongea tu, wamenuna na kama anaongea na simu ataendelea hadi anapojisikia kumaliza. Hii si ofisi moja bali nyingi tu. Nashauri elimu iendelee kutolewa zaidi.

Mhehimwa Mwenyekiti, pia naomba kujua, je, maboresho haya yako katika kutoa huduma tu? Je, usafi wa majengo, ofisi na kadhalika ukoje? Sielewi iwapo tunahitaji fedha za kigeni au wafadhilli kutoka nje ili waje kusaidia kuweka mazingira ya ofisi zetu katika hali nzuri. Ofisi ni chafu, wanafagia chini tu, yumbi kila sehemu, baadhi ya ofisi zinanuka vyakula vinavyoliwa bila mpangilio wowote. *Documents* mbalimbali zimetupwa ovyo ovyo. Wakati umefika wa kutoa ajira ya watunzaji ofisi kwa wale waliosomea katika fani hiyo ya utunzaji wa ofisi au walipo wakasomee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge kwa sasa lina Tume, inakuwaje maslahi ya watumishi wa Bunge bado yako chini ya Wizara ya Utumishi? Mbona Mahakama wanajitegemea? Wafanyakazi wanajisikia wanyonge kwani hata marupurupu yao hayaongelevi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ajira kwa ajili ya *replacement* ya mtumishi aliyefariki, iwe katika ngazi ya ofisi inayohusika au Halmashauri zitumike zenyewe kupata mfanyakazi bila kulazimmo kupata kibali Utumishi kwani hali ilivyo sasa kuna ucheleweshaji na hivyo utendaji kazi kulegalega. Inawezekana akifa mfanyakazi ajira ni *automatic*, lakini ofisi nyingi hazina taarifa hizo, basi nashauri waelezwe kwa waraka.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza sana hotuba nzuri ambayo imewasilishwa asubuhi hii na Mheshimiwa Dr. Mary Nagu. Naunga mkono hotuba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee kuhusu mafunzo ya Viongozi wetu, hasa wa Kitaifa wanaopewa madaraka ya kuwa *Public Servants*. Pamoja na mafunzo yote, napendekeza kuwe na semina za *sensitivity control* yaani semina maalum inayolenga kuwaandaa Viongozi kuhimili vishindo vyta lawama, kashfa na tuhuma mbalimbali ambazo watakumbana nazo wakiwa madarakani. *Sensitivity control seminars* zinawapa Viongozi dawa ya kuondokana na aibu, kuondokana na shinikio la damu na kuondokana na hali ya kutopata usingizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza hivyo kwa sababu kwa maoni yangu *Media onslaught* au mashambulizi ya Waandishi wa Habari kwa Viongozi mbalimbali yanaweza kabisa kuathiri utendaji wa kazi wa Viongozi wetu. *Sensitivity seminars* zinafundisha Viongozi namna ya *ku-shape public opinion* na siyo kila mara kufuata *public opinion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kuwa tunao Viongozi wazuri katika Serikali yetu. Wakiongezewa uwezo wa kuhimili vishindo vyta kisiasa ndani ya vikao na kwenye Vyombo vyta Habari wataimarika zaidi na watachapa kazi zao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Utumishi na wa Utawala Bora kwa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya mwaka uliopita 2002/2003 na mpango mzuri wa mwaka ujao 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa iliyotapaka nchini na hasa rushwa inayowahusu Viongozi wa ngazi mbalimbali katika ofisi za umma na Taasisi zake, ninapenda kutoa ushauri kuwa pamoja na juhudzi zinazofanyika za kuzuia na kufuatilia *at source (offices)* za *anticorruption* katika Mikoa na kadhalika kuna haja ya kuchukua pia hatua za kusimamisha kazi, kuhamisha na kushushwa vyeo. Njia hii ni muhimu sana hasa ukizingatia kuwa mahakama zetu zina utaratibu mrefu na pia *corrupt* wa kutoa haki. Kwa namna hii umma unaiona Serikali haifanyi *enough*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afisa anayetuhumiwa itoshe, aondolewe katika wadhifa au kushushwa cheo. Njia hii inajenga imani (ambayo ni muhimu sana) ya umma kwa Serikali yake. Njia ya kutegemea tu mahakama peke yake kwa wakati tulio nao ni hatari kwa Serikali. Njia zote mbili zitumike. Tukiwa *too lenient* kama Viongozi, jamii itaangamia na huko mbele tutapata tabu sana kama nchi. Katika hili, kama Wananchi wa Kenya wana imani sana na Serikali yao si kwa sababu labda rushwa itakwisha siku za usoni bali *combination of measures and action* zinazotumiwa kuikabili rushwa. Wanaotuhumiwa na wengi na wanaonaswa na vyombo vilivypopo waondolewe au kupata *demotion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mishahara ni kubwa katika nchi nyingi za dunia ya tatu (*poor developing nations*). Lakini kazi zinatofautiana katika mazingira haya ya kiumaskini. Huduma ya Walimu, Madaktari na kadhalika ni muhimu na *exceptional*. Kwa maoni yangu, hawa ni lazima watazamwe kwa jicho tofauti na sisi wengine tuelewe hivyo. Naipongeza Wizara hii kwa hotuba hii iliyotanabaisha kuwa katika Bajeti yao ijayo makundi haya yametazamwa. Tusichoke kuwaenzi Walimu kwa kuwalipa vizuri na kuwajengea mazingira mazuri ya kutenda kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni matumaini yangu kuwa ifikapo 2005 kweli asilimia 30 ya Wanawake katika ngazi za Viongozi itakuwa imefikiwa. Wizara hii ikishirikiana na nyingine ihakikishe lengo hili linafikiwa kwani Wanawake wanaostahili wanaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpungeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Dr. Mary Nagu, kwa hotuba nzuri ambayo imeeleza kwa uwazi shughuli anazosimamia. Nawapongeza pia Maofisa wote walio chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchangia kuhusu ajira ya wataalam wa kigeni. Nashauri Waziri awe makini sana katika zoezi hili maana siku hizi ukienda katika Mashirika na Makampuni yaliyobinafsishwa, unashangazwa kuona wageni wakifanya kazi ambazo Watanzania wapo wengi wanaoweza kuzifanya! Nenda katika mahoteli na viwanda, utaona wageni hawa wakifanya kazi ambazo wanafundishwa na Watanzania! La kushangaza ni kwamba mishahara ya hawa wageni ni mikubwa sana. Mishahara hiyo ni mikubwa sana kiasi ambacho inaonekana kuwa ni hila za wawekezaji hawa katika kurudisha fedha nyumbani kwao. Nashauri kuwa nafasi hizi ambazo wageni wanazichukua zitangazwe kwa uwazi katika magazeti ili tujihakikishie uhalali wa kupata wageni hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie suala la ucheleweshaji wa upandishwaji vyeo wa wafanyakazi Serikalini, maana hii ni haki ya msingi ya Watanzania hawa. Tuwaonee huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongozi za dhati kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii na hotuba nzuri iliyotolewa leo asubuhi. Hongera hizo ziende kwa Mheshimiwa Waziri na kwa wataalam wake wote. Nawatakia afya njema na maisha marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya mishahara ni duni kwa namna yoyote utakayoitazama. Hata *World Bank* wanatambua hilo kwa vile wakitaka programu fulani ifanyike wataunda chombo na kukipa mshahara mkubwa. Kama *PSRC, LART, Reform* ya Utumishi na kadhalika. Nashauri tu-revisit *Addu Report* ya 1960s, tufanyie marudio na kuipa sura ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *stop* tuliiweka kwenye ajira sasa itolewe hasa katika sekta ya masomo ya juu na sekta nyeti badala yake tutoe miongozi ya ajira kuliko vibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwanza kabisa napenda kukushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi nisimame mbele ya Ukumbi huu kuungana na Mheshimiwa Waziri mwenzangu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi) au Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kuwasilisha maombi ya fedha kuhakikisha kwamba mwaka ujao wa fedha tunaendeleza utekelezaji wa majukumu ambayo Bunge hili Tukufu litaafiki. Kwa hiyo, nianze kwa kusema sisi lengo letu ni kuomba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kama Mheshimiwa Waziri mwenzangu alivyowasilisha asubuhi hii kwa ufasha kabisa na nampongeza sana kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kwa niaba ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma. (*Makofi*)

Pili, napenda kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Athumanji Janguo na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano na ushauri ambao tumeupata mimi na mwenzangu wakati wote tunapokuwa mbele ya Kamati hiyo kuwasilisha maombi au Taarifa za utekelezaji wa majukumu ambayo tumepangiwa na umma na tatu, napenda kutoa pongozi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliotangulia kuwasilisha hotuba zao za Bajeti na maombi ambayo kwa heshima kubwa tumepokea kwa furaha idhini ya Bunge hili kuyatekeleza.

Nne, natoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Kwa kweli muda wote ambao nimekaa ndani ya Bunge hili nimeshuhudia Waheshimiwa Wabunge katika michango yao wameishauri Serikali, wamekosoa na mwisho kutoa baraka ili tuendelee na uchapaji wa kazi. Kwa hiyo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata fursa ya kuchangia kwa kuzungumza au kwa maandishi.

Tano, natoa shukrani kabisa za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani na hii iungane na pongozi za dhati kwa walioshinda uchaguzi katika uchaguzi mdogo uliopita, Chama Cha Mapinduzi na *CUF*. Mjadala ndani ya Bunge hili umedhiihirisha kwamba kwa kweli kuna mshikamano ndani ya Bunge hili. Kuna kutofautiana bila kupigana. Tunapingana bila kupigana na wanaozidiwa hoja hawatoki nje na chuki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima niseme kwamba nimekaa Bungeni humu tangu mwaka 1995 lazima tukiri kwamba kama kumbukumbu za Bunge hili zitachukuliwa sawa sawa, hakuna Bunge katika Afrika naweza kusema hata Ulaya ambalo linajadili masuala nyeti ya Kitaifa kutofautiana na hatimaye kufikia muafaka kama la kwetu. Wapinzani wameunga mkono Bajeti yetu. Hoja za Wizara wanaunga mkono, wanasema wanashauri, watafiti watatusaidia. Maana tuna Watafiti wengi Chuo Kikuu na ndani ya Bunge hili, kama lipo Bunge linaloendeshwa kama hili nitashangaa sana, kama yatakuwepo mawili tena hapo ndiyo nitashangaa zaidi. Tutakuwa wa kwanza hata kama likiwepo lingine kwa jinsi tunavyoendesha mambo yetu na hiyo ndiyo ushahidi wa Utawala Bora. Huwezi kuutafuta kwingine. (*Makofi*)

Labda nisisahau, naomba nitoe salaam za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Jaji Rugakingira, kwa msiba uliotufika, Jaji wa Mahakama ya Rufaa ametutoka. Lakini tunawaombea familia yake na yeze mwenyewe Mwenyezi Mungu ailaze roho yake Marehemu Jaji Rugakingira mahala pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya jumla niseme kwamba jukumu letu ni kuomba fedha za kutekeleza majukumu yaliyoko chini ya Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti Utumishi wa Umma na tunajenga hoja hiyo kwa kutoa maelezo au ufanuzi kwa hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge mmezileta. Muda ni mfupi, nimepangiwa dakika 30 nimetumia tano sasa. Nitaenda kwa haraka haraka na zile hoja ambazo nitashindwa kuzigusia Mheshimiwa Waziri Mary Nagu, ambaye ametoa hotuba akihusisha hoja yetu atamalizia zile hoja ambazo zitabaki na nitakazosahau atazijibu, zikisahaulika kabisa tuvumilieni, tuandikieni tutazijibu kwa maandishi.

Kwanza, tumepata maelezo ya maandishi tukitakiwa tueleze chini ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kwamba kuna jengo bovu na vitendea kazi vina matatizo. Napenda kulitarifu Bunge lako Tukufu kwamba ni kweli jengo la Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kwa kweli liko kwenye hali mbaya na vifaa vyake havitoshelezi. Lakini tumeshapata *Lab Top* saba, *Desk Top* 10 na *Heavy Duty Photocopier* mbili. Ukarabati wa majengo hayo unatarajiwa kuanza kufanya hivi karibuni katika kukamilisha kuweka katika viwango vya kisasa Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uteuzi wa viongozi, hili limezungumziwa na Mheshimiwa Karim Said Othman Mbunge wa Chambani. Napenda kulitarifu Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba kufuatana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 37, Fasili ya Kwanza, Mheshimiwa Rais ana uhuru wa kuteua viongozi au kiongozi yeyote na halazimiki kufuata ushauri atakaopewa na mtu yeyote isipokuwa tu pale anapotakiwa na Katiba au Sheria nyingine yoyote kufanya lolote. Kwa hiyo, katika kuzingatia Utawala Bora, Mheshimiwa Rais ameipa kuheshimu Katiba na sisi Wabunge vile vile tungependa hizi *Prerogative Powers* za Rais ziheshimike. Tuaminiane ili aweze kufanya uteuzi kadri Katiba inavyoolekeza na Sheria inavyomlinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya Tume ya Mheshimiwa Hashim Mbita, kwa sasa ni Balozi. Balozi wetu au *High Commissioner*, Zimbabwe. Haya yamezungumziwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ambaye ameteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba wangependa kupata maelezo ya utekelezaji wa ripoti hiyo.

Napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir. Hii Tume iliundwa na Mheshimiwa Rais, haikuundwa na Bunge na Tume ya Mheshimiwa Hashim Mbita, imewasilisha ripoti yake kwa Mheshimiwa Rais. Napenda kulitarifu Bunge hili kwa sababu ndiyo chombo chenyé wajibu wa kuisimamia Serikali na vyombo vyake vyote, Bunge likishirikiana na Mheshimiwa Rais ambaye na yeze ni sehemu ya Bunge hili kwamba taarifa hiyo inaenda kufanyiwa kazi. Ushauri ambaa hata Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, amekubali kwamba imefanya kazi nzuri. Tunaendelea kuufanya kazi na subira itasaidia sana ili tuweze kuepusha madhara ambayo yanaweza kutokea tena kutokana na tukio la kusikitisha. Tunaomba Mwenyezi Mungu apishe mbali lisitokee tena huko Pemba.

Kuhusu ushiriki wa watumishi wa umma katika siasa, ushiriki wa watumishi wa umma na hapa Mheshimiwa Waziri, Mary Nagu, atanisaidia kufanya ufanuzi zaidi, unaongozwa na Waraka Na. 1 wa mwaka 2000. Katika Waraka huo watumishi wa umma wanaruhusiwa kushiriki siasa kama wakipenda na wanaruhusiwa kuwa wanachama wa chama wanachopenda. Hili limeulizwa na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya. Kwa hiyo, ni vizuri watumishi wa umma na wenyewe kama Watanzania tuwape upeo mkubwa wa maamuzi kushiriki kwenye siasa na hata kama wanatishia viti vyetu, tuongeze nguvu kabla hawajaja tuwashughulikie. (*Kicheko/Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri kutembelea Mikoa, Wilaya na Vijiji kwa shughuli ambazo zinaonekana ni za kisiasa au chama kwa kutumia nyenzo za Serikali. Napenda kueleza kwamba kwa mujibu wa masharti ya kazi za Mawaziri, kila mwaka Waziri yoyote anaruhusiwa kutembelea Jimbo lake mara nne kwa kutumia nyenzo za Serikali. Safari hizo zinaruhusiwa kwa siku 14 kabla ya kikao cha

Bunge. Sasa Waheshimiwa Mawaziri ni Wabunge na wana wajibu na haki ya kutembelea majimbo yao kuwaona wapiga kura wao, wakisikiliza matatizo yao kabla hawajaja Bungeni humu. Ndio maana mnasikia hata sisi Wabunge Mawaziri tunachangia kwa maandishi. Tunaeleza masuala ya jimboni, kama Mawaziri, tunaenda kama Waziri, nawakumbusha na Mawaziri wenyewe, na hili halina utata. Nilitaka kufafanua kabisa ni zama za uwazi na ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutohamishia Makao Makuu Dodoma, Mheshimiwa Grace Kiwelu, anasema sera zetu hazitekelezeki. Napenda kueleza kwamba kama Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilivyoeleza kupertia kwa *Chief Whip*, Mheshimiwa William Lukuvi, kwa kweli tukiendelea kueleza ni kuimarisha kumbukumbu tu, lakini ni kweli kwamba hatua za kuhamia hapa kwa awamu zinatkelezwa na kuna dalili kabisa. Baadhi ya Wizara ziko hapa, Bunge liko hapa na tatizo ni uwezo wa kifedha. Itachukua muda mrefu lakini sera hii uzuri tunaujua na una manufaa kwa Tanzania, sio wananchi wa Dodoma peke yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji kazi wa Idara ya Usalama wa Taifa. Kimsingi Idara ya Usalama wa Taifa inatekeleza majukumu yake kulingana na Sheria Na. 15 ya mwaka 1996 iliyounda chombo hicho na mwenye jukumu la kusimamia Idara hii kama majukumu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, ni Rais mwenyewe na kwa hiyo anatambua uzito kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge hata wa Kambi ya Upinzani wamebaini kwamba ni Idara nyeti na ni vyema iheshimike na iwezeshwe kufanya kazi kikamilifu na inafanya kazi kikamilifu. Huwezi kufanikisha usalama wa raia bila Usalama wa Taifa na wakisaidiana na vyombo vyote vya dola, Polisi na Majeshi. Sasa Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Bwana Apson kwamba haonekani. Wanaomtafuta sijui wanamtafuta wapi? (*Kicheko*)

Napenda kusema kwa heshima kwamba huyu Mheshimiwa Apson amekuja mara nyingi hapa Bungeni, labda tuweke vipaza sauti kwamba akiingia Bungeni kwamba Apson kaingia, anayetaka amwone. Lakini napenda kuhahakikishieni kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge nimeenda naye. Anafika pale anawajibika mbele ya Bunge. Hayuko juu ya Bunge wala hayuko juu ya Rais. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile ana wasaidizi wake, wakati mwingine anakuja mwenyewe, asipokuja mwenyewe anatumwa wasaidizi wake. Vivyo hivyo Katibu Mkuu Kiongozi, hayuko hapa, lakini anatumwa wasaidizi wake. Sasa huyo huyo anatafutwa afanane na wa Marekani, kule wana *Television, CNN* wanaweka. Sasa za kwetu hazimweki Apson. Labda mtusaidie kuwaambia *ITV*, kila anapoonekana Apson amulikwe na magazeti yamwandike. Hajafika huyu na Wasaidizi wake akina Lilungulu wako hapa. Hawa hawafichwi, hata ma-*RSO* watafuteni wakijificha tuambieni, ma-*DSO* wapo wote wamejazana, ukiwatafuta tu tutakuonyesha, sio kwamba tunawaficha. Sisi tunawazidi Marekani na Marekani wamekiri hivyo kwamba vyombo yetu vya dola vinafanya kazi kwa kushirikiana na wananchi ndiyo maana tumefanikiwa. Wananchi wanawajua, ukimtaka unamwona, usipomtaka humwoni na wasio na matatizo ya usalama hawamtafuti. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamisho wa Maafisa Usalama wa Taifa ambaa wamekaa kwa muda mrefu kwenye vituo vya kazi. Napenda kuwashakikishieni kwamba uhamisho unafanyika. Mwaka 2002/2003 watumishi 178 walihamishwa kwa misingi hiyo ambayo Waheshimiwa Wabunge mnazungumza kukaa kwa muda mrefu, kadri hali ya fedha itakavyoruhusu watawakuwa wanahamishwa. Ni vizuri Waheshimiwa Wabunge mkatushauri, mkamshauri Mheshimiwa Rais kupertia Ofisi ya Rais kama kuna Afisa Usalama mnadhani amekaa kwa muda mrefu, miaka 15 au 20 amesahaulika, atahamishwa tu kwa sababu kuhamishwa si adhabu ila anakwenda kutoa huduma sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira ya Idara ya Usalama wa Taifa. Ajira Idara ya Usalama inafanya kwa kufuata Sheria iliyoundwa na chombo hicho. Kwa hiyo, tunapenda Waheshimiwa Wabunge muishauri Serikali kama mtabaini wameajiriwa wasiostahili kuwa watumishi katika Idara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa madaraka, mijadala sasa idhibitiwe na watendaji, ameshauri Mheshimiwa Njelu Kasaka. Hilo la ajira ya Idara ya Usalama wa Taifa limezungumziwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando. Mheshimiwa Njelu Kasaka ametoa ushauri na sisi tunasema kweli majibidhano ya viongozi wa kisiasa na watumishi wa vyombo vya dola kwenye *uniform* kwa kweli si ustaaarabu na si utawala bora na ushauri wake unazingatiwa. Tutapenda hilo

tulichukue kama mlivyolileta. Napenda kuwahakikisheni kwamba mambo haya yanahitaji ushirikiano kati ya Waheshimiwa Wabunge na Serikali au na vyombo nya dola ili kuepusha majibishano ambayo yanaweza yakafedhehesha utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, DC Chunya kurejesha mbao kwa Bwana Kadu. Hili limeletwa na Mheshimiwa Njelu Kasaka, tena amesisitiza kwamba lazima nijibu sasa hivi na ametoka nje nadhani, samahani yupo anaafutilia pale kwenye nafasi ya mwisho. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taratibu Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Ofisi yake ambayo ina Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Mashtaka (*DPP*), wakishatoa maelekezo kwamba Serikali au Jamhuri haina nia ya kuendelea na mashtaka, taarifa hiyo huwa inapelekwa Mahakamani siyo kwa Mkoo wa Wilaya, inaitwa *Nolle Prosequi* maana yake hakuna nia ya kuendelea na mashtaka ya huyo bwana. Wakihitaji wataanza tena yaani Jamhuri. Maelekezo hayo Mahakamani huwa yanaheshimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi karibu miaka 20 iliyopita nilikuwa Mahakamani, tulikuwa tunaheshimu kabisa na hajadiliki, ikiishafika tu *Nolle Prosequi* akiiwasilisha *DPP* au *Public Prosecutor (PP)*. *PP* mwenyewe kwa niaba ya *DPP* au Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali, ni kumwachia au *kum-discharge* yaani humwondolei tuhuma *unam-discharge*, wakitaka warudi. Sasa baada ya hatua hiyo kuchukuliwa, tumejaribu kuwasiliana na Chunya, Chunya wanasema wana nia ya kuanza upya katika kupambana kwenye kesi hii. Lakini Kisheria *status quo* ya sasa yaani hali halisi, ni lazima huyu mtu apewe mbao zake. Kama watakuja kulalamika baadaye wakishinda mbele ya safari huo ni utaratibu mwingine wa kurekebisha hali hiyo.

Kwa hiyo, kwa niaba ya Serikali nasema Mwanasheria Mkoo wa Serikali aliyeko Mbeya awaelekeze viongozi wetu wa Serikali. Haya mambo yanahitaji kuvumiliana, kueleweshana kwamba *Nolle Prosequi* ikishafika Mahakamani ikaheshimika, DC hana uwezo wa kuijadili na kwa hiyo utekelezaji uanzo mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziway, amezungumzia utaratibu wa sasa wa kumpa uwezo wa madaraka mwisho Mkurugenzi wa *PCB* kuweza kukubali au kukataa mtu yejote kuchunguzwa kwa tuhuma za rushwa. Tunaendelea kupokea ushauri juu ya marekebisho ya Sheria ya kuzuia rushwa ya mwaka 1971. Madaraka ya Mkurugenzi Mkoo wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa ni ya kiutawala ndani ya Taasisi lakini haina maana kwamba amepewa uwezo juu ya Taasisi na juu ya Serikali nzima na juu ya vyombo vyote kwamba huwezi ukalalamika kwingine. Unaweza ukalalamika kwingine na hatujasikia malalamiko ya mtu yejote kwamba huyu mtu alistahili kushitakiwa kwa kosa la kuzuia rushwa lakini akashitakiwa. Ndiyo maana mnasikia hata mwenye dhamana hiyo Mheshimiwa Rais anasema, kama unadhani hujatimiziwa mahitaji yako ndani ya Taasisi mwone yeje au nenda kortini, unaweza ukafungua kesi Mahakamani halafu utaratibu wa Sheria utasimamiwa chini ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mbunge Viti Maalum, anasema rushwa inayowahusu viongozi mbalimbali wa Ofisi za Umma na Taasisi zake, anashauri kwamba Maofisa wachukuliwe hatua haraka iwezekanavyo kwa kusimamishwa, kushushwa cheo au kuondolewa kazini. Hili ndilo linalofanyika mara tu inapobainika kwamba kuna sababu za msingi. Kwa hiyo, tunamshukuru Mheshimiwa Salome Mbatia, kwa ushauri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja za Mheshimiwa Remidius Kissassi, alisema kuwa kuna hoja nyingi sana. Unajua mambo yanayohusiana na mambo haya ya Utawala Bora ni mengi sana. Niseme tu kwa kifupi kwamba nyingi zinafanana hivyo kwamba uimarisaji wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa kwenda Mkoani, Wilayani na sasa tunakwenda Wilaya zote, baada ya kwenda Wilaya 46 sasa tunakwenda Wilaya zote. Tunaomba ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge kwa kweli kuendelea kushiriki, sisemi kuanza ila kuendelea kushirikiana. Hapa Chama cha Wabunge wanaopambana na rushwa (*APNAC*) wameisaidia sana Serikali kushauri na kusimamia kwa nguvu sana mapambano dhidi ya rushwa na kwa hiyo sisi tunaona kuna mafanikio makubwa sana na ndiyo maana hata nje na ndani ya nchi watu wanakiri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano mtu akisema tangu mwaka 1995 rushwa bado ni ile ile na inapanda, mimi huwa nashindwa kuelewa kwa sababu nikichukulia mfano, mimi siyo Mpelelezi ila ni Kamisaa wa Siasa kwenye masuala haya, lakini kwenye Jimbo langu mambo yamepungua sana haya rushwa. Kwa sababu gani? Tuseme ambayo tunaweza tukakubaliana hapa mengine ukisema mtasema hayo ni yako labda una mabavu. Ukiondoa ada ya shule ya msingi na michango, sasa mwenye mtoto shule ya msingi atakwenda kumuhonga nani, haijapunguza rushwa kweli hiyo? Hilo la kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, ukiondoa kodi ya maendeleo iliyokuwa inawabughudhi watu, pesa ya kiatu, pesa ya kwato la ng'ombe, sasa imefutwa na michango yote ya ushuru, sasa rushwa haijapungua uko kweli? Tunabaki na Mahakama za Mwanzo na Polisi. Sasa wewe kama unakwenda kortini kila mara si mmpungua, mnaopenda kwenda kortini, mimi sjawahi kwenda kushitaki kortini na miaka yangu hii. Sasa wale wenye matatizo Polisi na Mahakamani wawaone Waheshimiwa Wabunge, rushwa inapungua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *grand corruption*, ile imebaki ni ya kisiasa. Tunaita ya kisiasa kwa sababu mimi binafsi labda kama siaminiki kwamba ninaweza nikafikisha taarifa hizi kwa Bunge au kwa Mheshimiwa Rais, sina jina la mtu ye yote mwenye *account* nje, mwenye mali nje au mwenye kushiriki *grand corruption*, sina na hata Ofisi kwangu haipo. Yanakuja malalamiko ya ubadhirifu, malalamiko ya madai ya pensheni na kutofuatiila mambo yao, mambo ya Utawala Bora ni yale ambayo tunaweza tukayamaliza sisi kwa sisi na nje ya nchi kama alivyosema Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, tunaheshimika sana na hata kwenye *SADC* tunaheshimika sana.

Sasa sisi tukisema kwamba mambo hapa yanaharibika ndiyo watu wanaanza kutafsiri, hivi ni kwa sababu ya mwaka 2005 unakaribia nini? Kwa hiyo, mimi napenda kusema kwamba rushwa bado ipo lakini tunaizunguza kwa kasi sana na dunia inakiri na wananchi wanakiri na hata tukiitisha uchaguzi sasa hivi twende kuchuana mimi kwenye Jimbo langu sina matatizo, sijui wenzangu huko, narudi tu labda Kamati ya fitina iweke mizengwe mingine lakini na yenyewe nitaivunja. Kwa hiyo, ni kwa sababu ya utekelezaji mzuri wa sera za Chama cha Mapinduzi za Utawala Bora ndiyo tunapambana navyo. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba ni mambo mengi hapa ya kujadiliana mengine tutaendelea kujibu kwa maandishi. Napenda niliseme hili la Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Napenda nimshukuru Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Naibu Waziri Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, ameleezea kwa kiswahili kizuri sana na mimi nina matatizo ya kiswahili, mnanifahamu, kiswahili alichokitumia siwezi kukirudia. Lakini nataka kusema kwa maneno machache tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwapongeze *opposition*, kwanza wamenichanganya mara mbili. Msemaji wa Kambi ya *opposition* ameweka mwishoni ushauri mahsus kama binafsi hivi kwamba, "Mheshimiwa Waziri Mkuu atumie ujasiri wake ajiuzulu," ni wastaarabu siku hizi tunakwenda vizuri, hajasema ajiuzulu amesema awajibike. Nikasema anataka awajibike kwa namna gani? Huyu mtu ambaye ni jasiri wanamfahamu, wanampenda na kweli kura hapa alipata nyingi na huyu ni mtu ambaye anasimamiwa na Bunge kwa mujibu wa Katiba hakuna hoja mahsusidhidi yake, nikasema labda ngoja tusubiri watashauri nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani mdogo wangu Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, akasema anafunga mjadala, kabla hatujajibu akasema: "Sasa hili la Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba tulifunge." Sasa na majibu yangu niliyokuwa nayaandaa nikawaza kwamba sasa nijadili au nisijadili. Lakini nikasema hapa inawezakana ndiyo aliyyosema Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, ni chenga za kisiasa, mtu akulambe chenga, ulala huko huko uachie goli liingie.

Sasa Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, amekwishazuia mpira huko katikati sasa na mimi nasema hivi tunaendelea kucheza. Kwa kweli suala la Mheshimiwa Waziri Mkuu kuletwa Bungeni ni vichekesho na tunajadili katika vichekesho ndiyo maana na mimi nimeweka mwishoni. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilimsikiliza huyu Mtikila kwenye vyombo vya habari kwa sababu nikiri mbele ya Bunge hili, nawajibika kwa viapo. Sina barua ya Mtikila na anajua mimi siyo mpelelezi labda anaona siwezi kusaidia, sina malalamiko yoyote dhidi ya tuhuma hizi. Simsemi kwa sababu yuko mbele yangu na ni bosi wetu, ni Waziri Mkuu. Tunajibu kwa niaba ya Serikali hapa.

Walisema Mheshimiwa Waziri Mkuu anamiliki *Africa One Airline*, ana shares mle. Tukaenda kuchunguza quickly bila yeye Mheshimiwa Waziri Mkuu kuturuhusu kwamba hivi Mheshimiwa Waziri Mkuu kumbe ni tajiri sana mpaka amenunua ndege hii. Wakasema hata kumjua hawamjui kule, tukasema sasa huyu Bwana Mtikila kapata wapi?

Tukakimbilia ile ya *Uganda Avenue*, walisema ana nyumba kubwa sana *Uganda Avenue*, mimi ninakaa karibu na maeneo hayo hayo, nikaingalia nyumba ni nzuri kweli, nikauliza hii nyumba ni ya nani? Tukamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, akasema hiyo nyumba ni ya *National Housing*. Sasa tukasema hawa ni sawa na watu wanaouza Misikiti kwa utapeli nini? Nyumba hiyo anakaa Mzee Salim Ahmed Salim, kwa kupanga wala hata siyo yake. Wakasema tena ile barabara ya Kitonga ya kwenda Iringa Mheshimiwa Waziri Mkuu amemleta Kandarasi wake kwa rushwa, akampa ile. Tukachunguza, wala hata ile siyo ya Serikali, inagharamiwa na grant ya Japan na tender zimeendeshwa huko huko. Jamani, labda kama Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu ni Mjapan. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuseme, hivi kweli hata kama unachunguza, sisi siyo wataalam wa uchunguzi, unaweza ukaanza kuchunguza halafu ukamtaka Waziri Mkuu ajiuzulu? Hivi Mtikila sasa baada ya Waziri Mkuu akijiuzulu akisema Mawaziri wote tuna tuhuma, tujiuzulu wote, kwanza akitoka Waziri Mkuu tunakwenda sisi wote. Baadae anakwenda kwa Waheshimiwa Wabunge ni kawaida yake, “Wabunge wote ni wala rushwa,” je, tunajiuzulu? Sasa hii tutakwenda wapi? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kushauri kwamba haya siyo masuala ya kutetea, ni suala la kujenga umoja na heshima kwa viongozi wetu. Kama una taarifa peleka ndani ya Bunge au mpelekeee Mheshimiwa Rais. *PCB* wale ukiwapelekea wanapokea lakini hawawezi kabisa kumwajibisha Mheshimiwa Waziri Mkuu na kila mtu akaridhika kwamba amewajibishwa na *PCB*, si Bunge mna madaraka chini ya Ibara ya 55(a)?

Sasa kazi yenu imewashinda kweli mpaka twende kwa wapelelezi, imewashinda ninyi? Mmempigia kura ninyi kwa kuletewa jina na Mheshimiwa Rais halafu mnaiachia *PCB*, tuna uwezo wa kumdhhibit Mheshimiwa Waziri Mkuu yeyote tutakayemchagua, kwa sasa hakuna ushahidi wa kutosha. Nataka kusema kwamba kwa sababu hatuna ushahidi wa kutosha lazima tuwaheshimu viongozi wetu halafu tufuate taratibu za Kikatiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuhusu *globalization*. *Globalization* siyo kwamba Mheshimiwa Rais anakwenda tu kama Mwenyekiti Mwenza, tumesikia mambo mazito sana.

Napenda niwaambie tu kwamba mmesikia mwezi huu, katika wiki hii, Rose Gandi Kuijila anakuwa *Commissioner* wa *Rural Economic and Agricultural Commission* ya *African Union*, huyu ni Mtanzania. *Advocate* Nyanduga, amechaguliwa kuwa mjumbe wa *Human and People's Rights Commission of the AU*. Ni Mtanzania, Dr. John Monyo, ameteuliwa kuwa *Deputy Director General for Rural Participatory Development Planning* ya *Food and Agricultural Organization (FAO)* of the United Nation na Dr. Geofrey Mrema, ambaye anakuwa Mkurugenzi Mkuu (*Director General*), *Agricultural and Development Department, FAO*. Ni hawa wanachaguliwa kwa heshima.

Tumemsikia na Betty Mkwasa, si wa *IPP* huyu? Ni matokeo ya Utawala Bora nchini kwetu, ni ushahidi wa Utawala Bora, ukiwa na vijana ambao wanaweza wakakubalika nje ya watu na hata kwenye familia, kama watoto wako hawaolewi familia hiyo husemwa. Ndivyo watu wanavyosema kwamba wakiolewa wasifu. Lakini unaweza ukawa una matatizo kwenye familia watoto wasiolewe kwa sababu wanaume ni wachache, wanawake ni wengi. Lakini wakiolewa wanawake katika familia tunasema ni kigezo cha ukoo unaopanuka wenye heshima. Tunapata wawekezaji kutoka nje, vijana wetu wanaajiriwa nje na wengine wengi, Salim Ahmed Salim ametoka *AU*. Bado tuseme Tanzania sisi ni wala rushwa, wachafu. Ni watu wa kulia peke yetu. Hapana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia napenda kuunga mkono hoja na kusema Utawala Bora hapa umejikita lakini kazi bado iko mikononi mwetu kwa sababu watawala ni Bunge hili siyo Serikali peke yake. Waheshimiwa Wabunge, mnatushauri na mnatusimamia kwa mujibu wa Katiba na kutushauri. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. Mwenyezi Mungu awalinde. *Amin.* (*Makofsi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa moyo wa dhati nikushukuru wewe na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uongozi wenu mahiri kwa jinsi mlivyoongoza majadiliano ya leo ya Bajeti ya Ofisi ya Rais na asasi zake. Kwa moyo huo huo napenda nimpongeze Mheshimiwa Ramadhani Hashim Khalifan, Mbunge wa Bagamoyo, kwa kuwasilisha kwa ufasaha maoni na ushauri wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kamati ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Athumanji Janguo, Mbunge wa Kisarawe. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa vile vile niihakikishie Kamati hii kwamba wametushauri, wametuonyesha nimi la kufanya na wametuonyesha ushirikiano mkubwa sana hadi kufikia mawasilisho ya leo ambayo Bunge lako Tukufu hakuna hata mmoja ambaye amepinga jambo na ninategemea sana kwamba hawatatu-grill sana wakati wa vifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, wote ninyi ni mashahidi jinsi Mheshimiwa Waziri, Wilson Masilingi alivyoweza kujibu hoja nyingi sana na kwa hiyo kunipunguzia kazi nyingi. Lakini vile vile ningependa kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Naibu Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa kuweza kuweka uzito mkubwa sana kwenye hii hoja yetu na kuweza kulichangamsha Bunge hili zima pande zote mbili, Waheshimiwa Wabunge wa Chama Tawala na wale wa Upinzani. Nafikiri mtakubaliana na mimi kwamba amejaribu kuonyesha umuhimu wa ushirikiano ndani ya Bunge hili kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Kambi ya Upinzani kwa maoni yao. Yale yote ambayo yanachangia katika kuboresha utendaji wa Serikali tutayazingatia ipasavyo na yale ambayo yana nia ya kutudhoofisha tutajaribu kuyakwepa na kwa nguvu zote. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyo mazuri na ambayo yanaongezea ubora wa uendeshaji wa shughuli za Serikali tutayachukua na ninapenda kuwashakikishia ya kwamba sisemi tu kisiasa ya kwamba tutayachukua, lakini napenda kurudia tena kwamba yale ya kutudhoofisha sisi Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kweli hatutayakumbatia bali tutayakimbia kweli kweli pamoja na kututafuta makosa pale ambapo hatuna makosa, tunajua hizo ni chenga za mwili kama ukiwa kiwanjani inabidi umkwepe adui yako ili na wewe uweze ku-score zaidi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa vile vile kuwapongeza na kuwashukuru Wabunge wenzangu waliochangia kwa maandishi na kwa kusema katika hoja hii ya Ofisi ya Rais na asasi zake. Waliochangia kwa kweli ni wengi, ni zaidi ya 80 na wamekuwa wengi kwa sababu Ofisi hii ni ya msingi katika shughuli za Serikali, hakuna sekta hata moja ambayo haina ulhusiano na Ofisi yetu kwa hiyo sikushangaa kuona kwamba michango ni mingi, nilikuwa nahesabu majina mpaka nikafika mahali imepita 80 nikasema sasa nisiedelee kwa sababu muda ulikuwa mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wingi wa michango yenu imeonyesha jinsi ambavyo mmeonyesha *interest* katika kufuatilia utendaji wa Serikali na hasa utumishi wa umma. Ninyi wote Waheshimiwa Wabunge upande wa CCM na upande na Upinzani, mmesema kwamba watumishi wa umma ndiyo Serikali yenye, wakifanya kazi vizuri Serikali inafanya kazi vizuri, wasipofanya kazi vizuri kila mmoja wetu anaathirika kwa namna moja au nyiningine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba miaka ya 1980 mambo yalikuwa magumu sana, nchi ilikuwa haina fedha na kwa hiyo, utumishi wa umma ulikuwa umeathirika sana kiuendeshaji kwa sababu nyenzo za kufanya kazi zilikuwa ni duni sana. Lakini vile vile mishahara ilikuwa duni jambo ambalo sasa hivi tunaanza kulisahihisha. Kutokana na uduni ule basi, utumishi wa umma ulikuwa umeathirika na kwa hiyo wale ambao hawakuwa na moyo walianza kupoteza ari ya kufanya kazi. Jambo ambalo kwa kweli lilifanya ikawa ni mazoea sasa kwa watumishi wa umma kutokutimiza wajibu, lakini ninyi wenye ni mashahidi kwamba sasa mambo yameanza kubadilika, tumeanza kuongeza mishahara,

tunaboresha nyenzo za kufanya kazi na kwa hiyo watumishi wa umma kwa vyovytote vile hali zao zimeboreka na watafanya kazi zao kwa bidii sana. Lakini tukumbuke ya kwamba mazoea nayo ni taabu kuyaondoa, kama ubovu ulikuwa umeingia katika utumishi wa umma, kwa sababu mbalimbali inachukua muda mrefu kuwaondoa. Kwanza, inabidi mifumo yenewe ibadilike kwa kadri miaka inavyobadilika lakini vile vile na usimamizi lazima uimarishwe. Nikiendelea kusema zaidi juu ya utumishi wa umma nitasahau kuwashukuru wale ambaao wamechangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuwashukuru wale ambaao wamechangia hoja yetu kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Ramadhani Khalfan, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge na Mbunge wa Bagamoyo, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Wilfred Lwakatire, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir na bila kumsahau Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni wengi vile vile na kwa kweli hii orodha ni ndefu sana labda nijaribu tu kuwataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Halimensi Mayonga, Mheshimiwa Abdulkarim Shah tena, Mheshimiwa Profesa Talala Mbise, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi na wengine wote ambaao nitakuwa nimewasahau waniwie radhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hoja ya kuboresha utendaji kazi chini ya programu ya kuboresha utumishi wa umma. Mheshimiwa Fatma Said Ali, alichangia hoja hii na Mheshimiwa William Shellukindo naye vile vile alichangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati mzima wa programu wa umma, ni kuongeza utoaji wa huduma kazi katika ngazi ya kuboresha utumishi wa umma, ni kuongeza utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa kuboresha utendaji mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine muhimu ya programu hii, ni uanzishaji wa Wakala wa Serikali chini ya mpango huu. Baadhi ya Idara za Serikali zinabdalishwa kuwa Wakala na zinafanya kazi katika misingi ya kibiashara chini ya Wizara Mama. Lengo ni kuongeza ufanisi wa utoaji huduma wa vyombo hivi kwa kuviondoa kwenye urasimu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya kuboresha utumishi wa umma, ni matumizi ya mikataba ya huduma kwa mteja. Ni mkakati mwininge chini ya programu ya kuboresha utumishi wa umma. Chini ya mikataba hii kila Wizara, Wakala na Idara inaanisha majukumu yake na kuifanyia tathmini na kila mwananchi anapaswa kujua majukumu ya asasi hizo. Mikataba hii inatoa uelewa zaidi kwa wananchi kuhusu aina ya huduma na muda wa kuzitoa kwa kila Taasisi husika na kwa hiyo unapokuwa sehemu za mahospitali, ni vema watumishi wale wakawa na kitambulisho kusudi inapotokea kwamba hawatoi huduma ipasavyo basi yule mgonjwa aweze kwenda mahala ambapo

anatakiwa kulalamika na msimamizi wa sehemu hiyo ya kazi anapaswa kuchukua hatua zinazotarajiwa kuchukuliwa.

Kwa mujibu wa Sheria Na. 8 ya Utumishi wa Umma, kama msimamizi wa kazi anapata malalamiko na asichukue hatua zinazotakiwa, basi Tume itakayoundwa ya Utumishi wa Umma itamfuatilia yule msimamizi wa kazi na kuchukulia hatua jambo ambalo halikuwepo awali. Kwa hiyo, katika maboresho ya utumishi wa umma, tunalolisisitiza ni usimamizi wa kazi, badala ya wasimamizi wa kazi kugeuka kuwa wanasiwa kama wale tunaoomba kura, wanapaswa kuwaangalia wale wanaofanya kazi chini yao, wale wanaofanya kazi vizuri wawasifu lakini wale ambao hawafanyi kazi vizuri lazima wachukuliwe hatua. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine katika kuboresha utendaji wa kazi Serikalini, inahusu jitihada za Serikali za kuwaongeza mishahara watumishi wake. Suala la mishahara linahusu raslimali na Serikali si Serikali choyo. Tumesema Serikali inaundwa na watumishi wa umma na watumishi wazuri lazima wapewe ujira unaostahili. Sasa kila tulipopata uwezo Serikali haikusita kila mwaka kuongeza ujira wa watumishi wa umma. Lakini bado hatukufikia pale ambapo tunataka kufika. Kwa mujibu wa sera ya mishahara ya muda wa kati kwa kweli tuko mbali na kufikia pale ambapo tunataka. Lakini wote mnajua kwamba chimbuko la kuweza kulipa mishahara bora ni *productivity* au tija na ufanisi wetu sisi wenywewe. Sio tu wa watumishi wa umma bali vile vile wa sekta za uzalishaji na za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa umma wakiweza kutoa leseni kwa ufanisi, watumishi wa umma wakiweza kutoza kodi kwa ufanisi na kwa haki na pia watumishi wa umma wakiweza kutoa huduma mahospitalini na mashuleni, wananchi katika uzalishaji na katika kilimo na biashara kwa vyovoyote vile wataongeza jitihada. Jitihada hizi ndizo zitakazowenza kuongeza mapato ya nchi yetu. Mapato ambayo yataongeza mapato ya Serikali na mapato ya Serikali ndiyo chimbuko la kuweza kulipia mishahara ya Serikali. Kwa hiyo, kwa hili hatuna kwa kweli njia ya mkato, ninasema kwamba kama tulivyoboresha mapato ya Serikali tuendeze tija na tuendeze ufanisi katika uchumi na katika kuzalisha ili mapato ya Serikali yaongezeke na mishahara yetu iongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilitaka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba, sasa sio *automatic* tena kupata nyongeza na pia sasa sio *automatic* tena kupata *promotion, promotion* itatokana na bidii ya yule mfanyakazi na tutafuatilia wasimamizi waweze kutenda haki kwa kuona wale ambao wana bidii waweze kutunzwa na wale ambao hawafanyi kazi waonywe au ikiwezekana waondolewe ili wale wanaopenda kufanya kazi wachukue nafasi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia hoja hii ni pamoa na Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Aisha Kigoda, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Joel Bendera na wengine ambao pengine nitakuwa nimewaruka lakini lililo muhimu zaidi ni hoja yenewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri wa Elimu akiwasilisha hoja yake, kuna Waheshimiwa Wabunge waliuliza juu ya kuchelewesa mishahara ya Walimu wanapoanza kazi. Hoja kubwa ni pale ambapo tunachelewa kupata taarifa za wale ambao wanaanza kazi. Kwa hiyo, natoa rai kwa Serikali za Mitaa hasa Halmashauri kuhakikisha kwamba taarifa za wale wanaanza kazi zinatufikia Utumishi ili zipelekwe Hazina ili wanaanza kazi wasichelewe kupata maslahi yao. Sisi kwa upande wa Utumishi tumejitahidi sana na tutaendelea kujitahidi ili kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kumekuwa na hoja ya kwamba kuna wimbi la makampuni na viwanda vya wawekezaji wanaoajiri kutoka nje. Hoja hiyo imeletwa na Profesa Henry Mgombelo na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro. Ninaloweza kusema tu ni kwamba kadri tunavyoendelea na kadri tunavyotoa elimu tuna Watanzania wengi ambao wanaweza kufanya kazi nchini mwetu. Lakini kuna sehemu zile ambazo ni nyeti ambazo bado tutahitaji wataalam kutoka nje na hao ni wachache sana. Kila tunapokuwa na wataalam tunakuwa na utaratibu wa kuwa na watu chini yao ambao watajifunza na baadaye wale wa nje waondoke na wananchi wa Tanzania wachukue nafasi yao. Nitashirikiana na Waziri wa Kazi kuhakikisha kwamba sheria na utaratibu wa kuajiri wataalam kutoka nje tunaufuatilia kwa karibu sana ili

tusiwanyime Watanzania nafasi wanazostahili lakini vile vile ni vema tusiinyime Tanzania utaalalm ambao haupo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni watumishi wa Serikali kukosa kueleweshwa wanapopandishwa cheo na pale ambapo hawalipwi maslahi kutokana na kupandishwa kwao cheo. Serikali itajitahidi kuwaarifu pale ambapo mtumishi anapopandishwa cheo. Kuna wengine ambao kwa kweli *arrears* zao hazijalipwa, tutajitahidi sana kuboresha taarifa ili hao nao wapate haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyoharibika kwa muda mrefu hayawezi kurekebishwa katika kipindi cha mwaka mmoja. Tunajitahidi sana kuboresha taarifa za Serikali ili tuweze kuwalipa haki yao watumishi wetu na wao waweze kutimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni ya watumishi wanaonyanyaswa kazini kwa kukoseshwa haki zao wanapostaafu au wakiugua. Hoja hii ililetwa na Mheshimiwa Esha Stima, Mbunge wa Viti Maalum. Hatua mahsusizi za kusimamia na kufuatilia watumishi wanaonyanyaswa kazini zitazingatiwa kwa utaratibu ambao uko na malalamiko yatafuatiliwa. Idara Kuu ya Utumishi ina sehemu ya maadili ambayo inapokea malalamiko mengi na malalamiko yakipokelewa yanapelekwa kwenye sekta mbalimbali na yanapocheleweshwa Idara Kuu ya Utumishi inafuatilia kuhimiza wale ambao wanapaswa kujibu malalamiko haya au kutekeleza yale wanayotakiwa kuyafanya, tunawafuatilia ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niongelee kuhusu marekebisho ya Kifungu Na.6(6) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 na Sheria hiyo hiyo Na.6(1). Tumepokea hoja ya *ALART* na hoja ya Waheshimiwa Wabunge na tumeona kwamba kuna tatizo. Kwa muda muafaka na kadri itakavyowezekana tutajaribu kuangalia marekebisho yanayotakiwa kufanyika ili tuweze kuyafanya na kwa vyo vyote vile tutayaleta hapa. Kwa mujibu wa Sheria Na.8 ya Utumishi wa Umma lengo na madhumuni makubwa kwa kweli ni kupeleka madaraka karibu na wananchi na watumishi sehemu za kazi. Sasa ikitokea kama kuna *section* moja imekosea kufanya hivyo basi ni vizuri tukiambiwa na sisi tutakuwa wasikivu tutafanya marekebisho yanayotakiwa na tutafuata utaratibu unaotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo niliipokea ni kutoka kwa Mheshimiwa Paul Kimiti anauliza kwa nini pensheni isiwe sawa na kima cha chini cha mshahara cha Serikali. Hoja hii tumeipokea na kama mnavyojua na kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliposema wakati wa kuwasilisha Bajeti, kima cha chini cha pensheni kimeongezeka hadi kufikia 20,000 tunajua kwamba hakitawenza kukidhi mahitaji ya lazima ya mstaafu. Lakini nia ya Serikali iko pale pale na kila inapowezekana tutafanya hivyo kama sio kesho au kesho kutwa na sisi tutastaafu kwa hiyo hatuna sababu kwa kweli kuwanyanyasa wastaafu wetu ila ni kwa sababu tu uwezo wa Serikali ni mdogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kulikuwa na hoja ya kulipa kwa mkupuo au kutokulipa kwa mkupuo. Rai tumeisikia, Serikali itaifanya kazi na tutafanya yale ambayo tunafikiria kwamba yataleta tija na maslahi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo niliipata ni upungufu mkubwa wa watumishi wa umma kwenye Halmashauri hasa kwenye zile sekta nyeti kama za afya, ualimu na kadhalika. Katika hoja yangu nilieleza kwamba kwa sekta zile ambazo ni nyeti na kuna upungufu mkubwa sasa tumeanzisha mtindo wa kuwapeleka wahitimu moja kwa moja wanapomaliza shule kwa hiyo, hatutaondoa huu upungufu mara moja. Pamoja na ari yetu ya kupeleka madaraka karibu na Halmashauri kuna Halmashauri ambazo zikitangaza kazi hazipati watumishi kwa hiyo kila wakati Serikali itakuwa inaingilia kati pale ambapo kunakuwa na matatizo kwenye Halmashauri zetu lakini nia yetu iko pale pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kaka yangu hapa ambaye ananipenda sana...

**WABUNGE FULANI:** Aah! (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Na huyu si mwininge ni Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu kaka yangu na mimi wote ni Wabunge wa sehemu moja yeye ni Mbunge wa Jimbo mimi ni Mbunge wa Viti Maalum. Kila kunapokuwa na matatizo kwenye eneo letu la uwakilishi basi halitamhusu yeye peke yake litanihusu na mimi. Kwa hiyo, pale ambapo pana tatizo mimi na yeye tutashirikiana kulifatilia tatizo hilo kwa nia ya kuliiondoa. Kwa hiyo, hoja aliyoleta tutaipeleka TAMISEMI mimi pamoja na yeye kuona ni njia gani sahihi ya kuweza kukabiliana na hoja yenyewe. Lakini akiniletea kama dada yake, mimi sitaweza kusaidia ila kama Mbunge mwenzake, basi tutaipeleka huko ambako inatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyininge zilijibiwa vizuri na moja ya hoja hizo ni kuhusu *Vote* ya Uhamiaji. Kama alivyoelezea Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tutashirikiana kuona kwamba *Vote* hiyo inapatikana lakini vile vile wanaohusika *Immigration* wasifikirie tu kupata *Vote* peke yake wangojee kuwjibika kwa kuzisimamia fedha hizo. Kwa hiyo, sisi tutajitahidi kwa kila njia kuweza kuona kwamba *Vote* hiyo inapatikana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Muafaka limeelezwa vizuri na sina haja ya kulirudia, suala la uhamiaji nimeliongelea, kulikuwa na suala moja ambalo alileta Mheshimiwa Membe, nimelipokea, tutalifanyia kazi ni ushauri ambao anataka kutusaidia watumishi na viongozi wa Serikali ili wawewe kutenda kazi zao vizuri, tutazingatia Mheshimiwa Membe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyininge ambayo napenda kuisemea kwa ufupi na ambayo Mheshimiwa Masilingi ameiongelea ni kuhusu ushiriki wa watumishi wa umma katika siasa kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi Na.1 wa mwaka 2000. Sidhani kama nina la kuongeza. Kama ni ushiriki tu watumishi wa umma watashiriki lakini kama ni *ku-participate* kwenye uongozi nafikiri Waraka umeeleza itakuwaje. Serikali nzuri ni ile ambayo inaweka utaratibu mzuri na wananchi wazuri ni wale ambao wanafuata utaratibu uliowekwa ili kusiwe na fujo ndani ya nchi. Kwa hiyo, suala la ushiriki halina mjadala lakini utaratibu lazima ufuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mawaziri kufanya shughuli za Vyama wakienda kwenye kazi zao, Mheshimiwa Masilingi amelielezea vizuri lakini Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani hawataninyima mimi Mama Nagu saa kumi na moja nikimaliza kazi za Serikali kwenda kufanya kazi za Chama changu na ni namna hiyo ndiyo tunaweza kujenga nchi yetu. Kama mimi niko tayari kufanya kazi mpaka saa tatu ya usiku Wabunge wa Upinzani wasininyime nafasi hiyo.

Lakini nasema kwamba kwa wakati ule ambao ni wa kazi za Serikali tutafanya kazi za Serikali lakini kama alivyoeleza sisi nasi tuna maeneo yetu ya uwakilishi kama ninyi itabidi twende tukafanye kazi hiyo na hatutauvua Uwaziri wakati huo. Tukifanya mambo ambayo ni kinyume cha Uwaziri ninyi mtapiga kelele ikitokea tukiyafanya vizuri na ninyi mtusifie ili tuweze kwenda pamoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la utaratibu, sheria, kanuni na umuhimu wa kufuatilia taratibu, sheria na kanuni. Katika kutuhumu wananchi, watumishi, viongozi lazima tufuate taratibu na sheria. Tukiwa nje ya taratibu tutakuwa tumeleta vurugu. Kwa kweli kutofuata taratibu katika kumtuhumu mtu ni pamoja na kumsingizia kosa ambalo hajalifanya.

Kwa hiyo, ni vema kabla mtu hajapelekwa Mahakamani kosa hilo lithibitishwe na kuna utaratibu wake. Kwa hiyo, mimi kama Waziri wa Utumishi, napenda kuhimiza Waheshimiwa Wabunge tuwe mstari wa mbele kama wawakilishi wa watu tulioletwa hapa kutunga sheria tuone kwamba sheria na taratibu zile zinafuata na tukifanya hivyo tutakuwa tumpunguza fujo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea, kujadili na kuzingatia taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inayohusu Ofisi ya Rais na Asasi zake, kwa mara nyininge naliomba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Rais na Asasi zake na bila ya kushika kifungu au mafungu yoyote kwa sababu tumejaribu kujibu hoja zote ambazo mmetuletea. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 20 - State House**

Kif. 1001 - *Administration and General* ..... Sh.3,496,209,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 30 - President's Office and Cabinet Secretariat**

Kif. 1001 - *Administration and General* ..... Sh.43,669,870,900/=

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Napenda niipongeze hatua ya Serikali ya kuagiza kwamba mtu ambaye alikuwa amenyang'anywa mbao zake arudishiwe. Ninaamini kabisa kwamba agizo hilo la Serikali litafikishwa kwa wahusika kwa kuandikiwa barua ili waweze kutekeleza agizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, iwapo itaonekana mbao hizo si kamilifu ni hatua gani itachukuliwa na vile vile hao ambao wanakaidi maagizo ya Serikali kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndio Serikali yenye wanapoagiza kwamba jambo hili liende hivi wanakaidi kuna hatua gani zitachukuliwa? Napenda tu wanipe maelezo hatua zaidi ambazo zinaweza kuchukuliwa kwa hawa wanaokaidi maagizo ili wasiendelee kurudia kukaidi maagizo ya Serikali ambapo hapo awali nilisema ndio ukosefu wa nidhamu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Njelu Kasaka, ambaye ana uzoefu wa utumishi ndani ya Serikali kama Naibu Waziri na Mkuu wa Mkoa kwamba agizo likishaahidiwa ndani ya Bunge hatua inayofuata ni utekelezaji. Nitashirikiana naye na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mamlaka ya uongozi ndani ya Mkoa wa Mbeya kuhakikisha maagizo ya juu yanatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mbao zitakuwa zimepungua kwa wizi au kwa kuoza hayo ni masuala ya ushahidi na masuala ya utekelezaji, tutashirikiana kuhakikisha kwamba haki inatendeka. (*Makofsi*)

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naelekeza kwa Utawala Bora na niko kwenye *Vote 30*, kifungu 1001, nilikuwa nimetoa hoja hapa Bungeni kuhusu Serikali za Mitaa na chaguzi zake na kuhusu hukumu ya Jaji ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikuwepo. Leo ni mwezi wa tatu sijajibwi leo nimeitoa hoja hiyo tena nikifikiri labda ningepata jibu leo, sasa nataka Serikali inijibu kuhusu suala hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulipata hoja ya Mheshimiwa Ngawaiya isipokuwa kama nilivyo sema muda ulikuwa hautoshi kujibu kila hoja lakini kwa vile ni masuala ambayo yanahusiana na uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao unasimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tuliamini kwamba tutashauriana naye kukaza hukumu kama haikukatiwa rufaa maana yake mambo ya Mahakama yanaenda Kimahakama. Mahakama Kuu uamuzi wake sio wa mwisho kuna Mahakama ya Rufaa hatuna taarifa kama kuna rufaa yoyote kwenda Mahakama ya Rufaa lakini kama hakuna rufaa na maagizo ya Mahakama Kuu yanaagizwa kutekelezwa kwa mujibu wa sheria lazima tushirikiane na Mheshimiwa Mbunge na waathirika kuhakikisha

kwamba haki inatendeka. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge atupe muda tushirikiane kama alivyo tuahidi na yeye.

**MHE. THOMAS NGawaiYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri lakini nataka kujuia muda sasa kwa sababu ni miezi mitatu na nataka nimhakikishie haikukatiwa rufaa na iko kwenye hoja yangu ya mwanzo Serikali walikubali. Sasa nilitaka majibu yao kwa sababu matatizo hayo yanaendelea kutuumiza huko mitaani.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimebahatika kukaa karibu na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kumbe suala hili linashughulikiwa na ameshaahidiwa kwamba linafanywa kwa *speed*. Taarifa atafikishiwa na *Chief-whip* atataarifiwa na hata utaratibu wa kuwalishwa Wabunge wote utafanyika kwa sababu jambo hili linahusu maeneo yote ya nchi yetu kwa sababu ni suala la haki ya msingi ya kidemokrasia ya kuchagua na kuchaguliwa. Kwa hiyo, awe na subira sio muda mrefu litashughulikiwa. (*Makofsi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ..... Sh.556,657,500/=  
Kif. 2001 - *Cabinet Secretariat* ..... Sh.621,778,700/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 32 - President's Office - Civil Service Department**

Kif. 1001 - *Administration and General* ..... Sh.3,138,016,200/=

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina sababu ya kumwumiza dada yangu maana yake aliomba sana. Lakini pamoja na ombi lake, kwanza naomba anihakikishie lile suala kweli tutalipeleka mimi pamoja na yeye kule TAMISEMI kwa sababu ni muda mrefu sana suala hilo limetokea tumekaa Ofisini kwake mimi na Mkurugenzi, ametoa maelekezo kwa Mkurugenzi mpaka sasa hakuna kinachofanyika, hakuna hatua iliyochukuliwa na hakuna taarifa iliyotolewa na athari inaendelea kutokea na Halmashauri inazidi kukosa mapato. Nilitaka uhakikisho wa hilo tu. Pamoja na hilo, napenda nimalize maswali yangu yote ili ajibu kwa pamoja. Ni kweli Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba amepokea malalamiko ya *ALART* na malalamiko yetu...

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Sawa, Mheshimiwa Anne Makinda.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kama Mheshimiwa anazungumza na Waziri wakati sisi tumekaa kama Kamati ya Matumizi kusudi tushiriki mambo hayo, sasa anasema kile kitu, kile kitu wakati sisi hatujui ni kitu gani. (*Kicheko/Makofsi*)

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa Dr. Slaa umeelewa kwamba Wabunge wangependa wajue kile kitu ni kitu gani mnachoongea na dada yako hapa, karibu sana Mheshimiwa Dr. Slaa, taja kile kitu. (*Kicheko*)

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri maelezo yangu yalikuwa kamili kwa Waziri kwa sababu yalikwenda kwa maandishi, Waziri ndiye alifupisha hivyo na mimi nikafupisha hivyo. Nafikiri wakati wa kufafanua jibu langu Waziri ataweza kueleza kwa kirefu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeomba kwamba kwa kuwa tatizo lililotoka katika marekebisho ya Sheria Na.8 imeonekana kwamba ni tatizo zito na limeathiri utendaji wa Halmashauri,

kuna uwezekano kwamba kuanzia tarehe 1 ambapo Kanuni ya Utumishi inaanza kutumika hasa kwa upande wa Halmashauri mgongano unawenza kutokea kutokana na kwamba sio watu wote wataelewa jinsi Serikali inavyoolewa. Kwa hiyo, wale wenye nia njema wanawenza kutekeleza vizuri lakini inawezekana pia kuna wasio na nia njema. Waziri nilimwomba kwanza asimamishe kwa kuwa suala limeonekana na yeze amekiri kwamba lina utata mkubwa. Lakini pili nikamwomba kama tutaendelea na utekelezaji basi inawezekana basi yeze akubali atoe maelekezo kwa njia yoyote ya kiutawala iwe ni Waraka iwe kwa njia yoyote ile ili mgongano huu unaowenza kutokea uweze kuepukwa hadi pale atakapoleta mabadiliko ya sheria. (*Makofî*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa kwa kutaka ufanuzi zaidi juu ya Sheria Na.8 *section 6(6)* na *section 6(1)*. Kwa Kanuni hizo hizo ambazo tunaanza kuzitekeleza tumeeleza wazi kwamba Wakurugenzi kabla ya kuajiri watumishi kwenye Halmashauri ni sharti kwanza wapate kibali cha Halmashauri yao.

Kama kutakuwa na haja ya kutoea Waraka mwingine tutafanya hivyo lakini Kanuni zenye zinaelekeza hivyo. Naomba tuendelee kutekeleza Kanuni kwa sababu Kanuni hizo ndizo zinazopeleka sasa madaraka kwa Halmashauri na sekta nyingine ili tusiendelee ku-refer masuala ya utumishi kwingineko badala ya mahali pale pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja yake ya kwanza nimesema wakati nikijibu hoja awali kwamba suala linalomhusu Mheshimiwa Dr. Willbrod kwenye Jimbo lake kwa sababu mimi ni Mbunge wa Viti Maalum basi nalo linanihusu mimi na kwa pamoja tutashirikiana kulipeleka na kufuatilia suala hilo TAMISEMI. (*Makofî*)

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa suala lile la kwanza la kufuatilia, Mheshimiwa Makinda alitaka kujua na kuna Waheshimiwa wengine huku naona wananiuliza ni kitu gani hicho kinachosimamishwa. Naomba nisieleze mimi kwa sababu muda wangu hautoshi lakini ni matatizo yaliyoko kwenye Halmashauri ambayo Mheshimiwa Waziri alikuwa anayajua kwa manufaa tu ya Mheshimiwa Makinda aliyetaka kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba kama kuna mahitaji ya kupeleka Waraka basi lifuatiliwe. Naomba Waziri akubali kwa kuwa kwenye Kamati iliyojadili Muswada huu mimi mwenyewe nilisimama na nikakataa marekebisho ya kipengele kile na leo *ALART* imeleta barua nzito kwamba kwa kweli matatizo yatakuwa makubwa. Naomba Waziri atoe Waraka ambaa utatekeleza au uthagiza na kukazia kwamba mgogoro usitokee basi aweze kuelekeza na kama Waziri atakubali mimi sina tatizo na hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoleza nasema kwamba nitafanya kila ninaloweza ili mgogoro usitokee.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi sipendi kuchukua muda mrefu lakini naomba ufanuzi wa vitu viwili. Wakati nilipota hoja juu ya taarifa ya Mheshimiwa Hashim Mbita, nilipata maelezo ya Mawaziri wawili.

Mheshimiwa Muhadhir alisema hii ni taarifa ya Rais na haistahili kuleta hapa Bungeni. Mheshimiwa Masilingi akasema kwamba Rais ni sehemu ya Bunge, kwa hiyo, vyombo hivyo vyote anavisimamia Rais. Sasa taarifa hizi mbili zinagongana moja inakubali nyingine inakataa kauli ya Serikali hasa ni nini juu ya jambo hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kadri nilivyomskiliza Mheshimiwa Mbunge anazungumza hakuna mgongano wa taarifa ni ufanuzi wa taratibu za usimamiaji kwa sababu mimi nimesema ambapo anakiri na ni sahihi kwamba Mheshimiwa Rais ni sehemu ya Bunge lakini Tume iliundwa na Mheshimiwa Rais na taarifa imepelkwa kwa mamlaka iliyounda Tume. Mwenzangu akawa anazungumza kwamba haiwezi kuleta kwa sababu haijaombwa na haikutakiwa kuleta huku.

Kwa hiyo, ni masuala ya utekelezaji kwa mujibu wa taratibu lakini hakuna mgongano wowote. Kama tuliviyosema inashughulikiwa na sio kwamba Bunge halitapaswa kujua tunachosema wakipenda kujua wakati muafaka na tuna muafaka mzuri katika uendeshaji mambo kati ya Bunge na Mheshimiwa Rais watajua ushauri unatekelezwa vipi.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri kwa hiyo naomba taarifa hiyo itakapokuwa tayari atuarifu kwamba Bunge linalokuja italetwa katika Bunge hili.

**WABUNGE FULANI:** Aah!

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa Waziri hakumaanisha hivyo. Napenda tufuate kauli ya Waziri, naomba ielewewe hivyo.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata mwongozo.

**MWENYEKITI:** Eeh, Mheshimiwa Mudhihir.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata mwongozo wako ni wapi jina langu litarekebishwa baada ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kuniita Muhadhir, badala ya Mudhihir? (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Nalirekebisha mwenyewe kwamba wewe ni Mudhihir, sio kama alivyotamka ye. Limerekebisha Mheshimiwa Mudhihir. Hivyo hiyo hoja imeshapita.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Hoja imepita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tufuate taratibu, nilikupa nafasi Mheshimiwa Dr. Slaa umemaliza mambo yako nikahamia kwa mtu mwingine sasa ameuliza tu. (*Makofsi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ..... Sh. 91,681,700/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kifungu hicho kimeshapita. Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyo zoea inatakiwa kuamka haraka sana. Kwa bahati mbaya tukishasema ndio, basi.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatusikii.

**MWENYEKITI:** Basi sasa utasikia.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Katibu Mezani ananong'ona.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, haya tunaendelea, soma kwa sauti Katibu.

Kif. 2001- *Policy Development* ..... Shs. 284,993,500/=

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati...

**MWENYEKITI:** Taja kifungu.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Ndiyo hiyo kifungu cha 2001, hiyo *Policy Development*. Wakati Waziri alipokuwa anasoma hotuba yake na mimi nilichangia kwa maandishi kuhusu suala la *Policy* ya *TASAF*. *Policy* ya *TASAF* ni kwamba wananchi ndiyo wanapanga miradi, wanaibua na kuweka *priority*

yao ya kwanza, ya pili na ya tatu na kupitisha katika vikao. Baada ya kupitisha katika vikao halali zinakwenda Makao Makuu ya *TASAF* na wanahehishimu.

Lakini nilipokuwa nikichangia nilisema Wilayani kwangu wananchi wanapitisha miradi kama inavyotakiwa, lakini *DC* ambaye ni Mwenyekiti wa kikao cha *TASAF* cha Wilaya anachukua madaraka ya wananchi kukataa miradi na kusimamisha hiyo miradi. Niliandika nilitaka majibu na wananchi wangu wanaumia kwa suala hili. Sasa tuchukue *Policy* ipi ya *DC* wa Kiteto ambaye anazuia miradi au tuache *Policy* ya *TASAF* na tuna uhakika na tuna ushahidi kamili ambayo ameizua.

Sasa tunataka kuelewa kwa sababu leo *TASAF* ipo hapa na Ofisi ya Ikulu, sasa watuambie *Policy* ipi ni sahihi, hii ya *TASAF* inayoendelea katika nchi nzima au hii ya *DC* ambayo sasa hivi anaitumia? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mara nyingine niombe radhi kwa Bunge hili, tulisema muda hautoshi na maeneo ya *TASAF* kwa kweli tuliyaweka kwa misingi ya kuyajibu kwa maandishi kwa sababu *TASAF* imepongezwa kwa kazi nzuri inayofanya na sisi tunapokea pongezi hizo.

Pia *specific case* ya Kiteto ambayo Mheshimiwa Losurutia ameieleza imetushangaza sana kwa sababu inapingana na sera za *TASAF* ambazo ni ushirikishwaji na kupeleka mamlaka kwa wananchi na Waheshimiwa Wabunge wote wamesikia taarifa ya Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ya kila mwezi, mwezi uliopita akieleza mwongozo mzima na misingi ya *TASAF* yenyewe ambaa ni mfuko ulio chini ya Ofisi yake. Sasa naomba Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ameleta taarifa na ni rasmi tufuatilie ili kurekebisha kasoro hii. Ni mambo ya ajabu sana *DC* kuchukua mamlaka ya wananchi. Tutafuatilia na kuamua. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2002 - *Management Services* ... ... ... . Shs. 115,722,800/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2003 - *Establishment* .....Shs. 312,638,600/=

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuhusu kifungu hicho cha Establishment. Ningombaa Mheshimiwa Waziri atoe tamko juu ya ahadi ya walimu na kama hakuna uwezekano kwenye establishment kuwapa masharti tofauti na bora zaidi ya kazi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu leo asubuhi nilieleza, asilimia 54.4 ya wage bill imepewa walimu na walimu ni asilimia 49 ya watumishi wote wa Serikali. Sasa katika ile asilimia 54.4 basi tutajaribu kuona ni namna gani sehemu hiyo itagawanywa kwa walimu kwa kadri ya uzito wa kazi ya walimu na hili litakuwa ni kazi ya Wizara ya Elimu.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2004 - *Ethics Division* ... ... ... ..... Shs. 88,103,600/=

Kif. 3001 - *Human Resources Development* ... Shs. 284,477,400/=

Kif. 3002 - *Civil Service Training Centre* ..... Shs. 52,284,800/=

Kif. 3003 - *Tabora Secretarial College* .....Shs. 39,386,300/=

Kif. 3004 - *Gender* .....Shs. 32,420,100/=

Kif. 4002 - *Management Information System* Shs. 118,242,800/=

Kif. 4003 - *National Archives* ... ... ... ... ... Shs. 367,203,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
bila mabadiliko yoyote*)

**FUNGU 33 - SEKRETARIETI YA MAADILI YA  
UONGOZI NA UMMA**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... Shs. 501,374,900/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
bila mabadiliko yoyote*)

**FUNGU 36 - TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... Shs. 642,329,800/=

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Katika kifungu hicho nilikuwa naulizia kwamba katika kuchangia nilizungumzia matumizi ya magari ya Serikali. Kuna utaratibu ulioletwa kwamba watumishi watendaji na hata viongozi wakopeshwe magari yao ili wakati ambapo hawapo kazini watumie magari yao kubana matumizi ya Serikali lakini bado kuna baadhi ya watendaji hata baadhi ya viongozi wanatumia magari hayo hata katika mazingira ambayo si ya kikazi.

Je, Serikali ituhakikishie hapa inachukua au inaandaa utaratibu gani utakaohakikisha kutenganisha huku ili kupunguza matumizi ya Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Magufuli kwa hatua alizochukua kuhusu magari. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikumbushe kwamba utaratibu ni kama ulivyoolezwa kwamba kwa wale waliokopeshwa magari kwa ajili ya kutumia wao binafsi wanapaswa kutumia magari hayo kwenye shughuli ambazo ni za binafsi na gari za umma zinapaswa kutumika kwa shughuli za umma.

Kama kulikuwa na uvunjaji wa utaratibu huo basi wakuu wa sehemu za kazi tunawakumbusha tena kwamba wachukue jukumu hilo na kama nilivyosema sheria ya utumishi wa umma sasa inajielekeza kwa wasinamizi wa kazi ambao hawatimizi wajibu wao na majukumu yao. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wote ambao sijapata kujibu hoja zao wanisamehe, hii ilitokana na ufinyu wa muda nimeshindwa. Nitatoa maelezo ya maandishi mapema.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
bila mabadiliko yoyote*)

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 30 - IKULU**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... Shs. 33,122,000,000/=

## FUNGU 32 - OFISI YA MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA

Kif. 2001 - Policy Development ... .... Shs. 3,575,379,100/=  
Kif. 2002 - Management Services ... .... Shs. 4,123,380,000/=  
Kif. 2003 - Establishment ... .... Shs. 610,200,000/=  
Kif. 2004 - Ethics Division ... .... Shs. 167,690,000/=  
Kif. 3001 - Human Resources Development ... Shs. 603,300,000/=  
Kif. 3002 - Civil Service Training Centre ... Shs. 249,856,000/=  
Kif. 3004 - Gender ... .... Shs. 224,439,000/=  
Kif. 4002 - Management Information System ..Shs. 1,207,550,000/=  
Kif. 4003 - National Archives ... .... Shs. 575,700,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)  
T A A R I F A*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba baada ya Bunge lako Tukufu kuketi kama Kamati ya Bunge zima na kupitia kifungu kwa kifungu Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2003/2004 kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote, naomba kutoa hoja kwamba makadirio haya sasa yakubalike na nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora  
Kwa Mwaka 2003/2004 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kazi za leo zimeishia hapa na kwa muda muafaka. Sasa naliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.42 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano  
Tarehe 16 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*

